

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 1 Novemba, 2012**

(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)

**D U A**

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae! Katibu tuanze!

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Kwa bahati nzuri Kiongozi wa Kambi ya Upinzani yupo, tulimsikia huko kwao Hai, lakini kumbe amerudi.

Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA UPINZANI**  
**BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kumwuliza Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tangu wakati wa Bunge la bajeti ilitolewa taarifa rasmi ndani ya Bunge ya kuwepo kwa mabilioni ya fedha za kigeni ambazo zimehifadhiwa katika akaunti za viongozi waandamizi wastaafu na wasio wastaafu katika mabenki ya Uswisi, na Serikali ilitoa kauli kwamba italifanyia kazi jambo hili ambalo ni *sensitive* sana na hadi hatua ya sasa hatujasikia tamko lolote la Serikali au mkakati wowote wa Serikali wa kujua ukweli wa taarifa hizo, pili, ku-*disclose* majina ya wahusika na tatu kuchukua hatua za *recovery* kwa sababu ya faida ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, una kauli gani ya kuliambia Bunge na kuwaambia Watanzania kuhusu Serikali unayoiongoza ina mkakati gani?

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbowe kwa swali lake na ninaomba nirudie niliyoyasema. Niliahidi kwamba hili jambo kwa sababu ya uzito wake na ukubwa wake na *involvement* ya mambo yaliyokuwa yamejitokeza kwenye vyombo tukasema tutahitaji na sisi kulifanyia uchunguzi wa kina ili tuweze kubaini ukweli na ni hatua stahiki za namna gani zinaweza kuchukuliwa. Sisi hiyo kazi tumekwishaanza kuifanya kwa hiyo tutakapokuwa tumemaliza basi tutatoa kauli kama ilivyo kawaida yetu.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mbowe! Labda wewe una majina tayari. (*Kicheko*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, fedha zilizotoroshwa nchini na kuhifadhiwa katika benki za nje hazipo Uswisi peke yake, kuna mabilioni ya dola yamehifadhiwa katika akaunti za nchi za nje katika visiwa mbalimbali ambavyo havitozi ushuru wanaita ni *tax havens*, kwa mfano Luxemburg, Mauritius, Dubai, British Virgin Ireland, Jews kule Chaim Ireland pamoja na vingine vingi kama Grenada, Mauritius na kadhalika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, na hizi fedha ni fedha nyingi za Watanzania ambazo zimepelekwa na wafanyabiashara na vilevile zimepelekwa na viongozi wastaafu na viongozi waliopo Serikali leo na mashirika yake, katika pamoja na mambo mengine dhamira ya kukwepa kodi kwa sababu katika visiwa hivi kodi hazitowzi.

Waziri Mkuu, Benki ya Dunia ina kitengo kinachoitwa *Assets Recovery Unit* ambacho kinasaidia mataifa mbalimbali kujua ukweli kuhusu fedha za nchi ambazo zimehifadhiwa katika mataifa ya nje. Ni kwa nini mpaka leo Serikali yako haijatumia kitengo hiki? Ni kwa nini basi kwa sababu kitengo hiki kipo na kwa sababu uchunguzi umesema hili ni jambo zito, tuwaachie basi *World Bank* kitengo hiki Serikali iombe kibali cha kusaidia ku-*recover* fedha hizi na kujua wahusika badala ya kuwaachia vyombo vya ndani ambavyo pengine vinaonekana vinashiriki katika kuhifadhi wale wahalifu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante! Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbowe anaweza akalirudia swali hili mara mbili au tatu na mimi bado nitakujibu hivyohivyo, kwamba jitihada zinafanyika na zitakapokamilika tutatoa maelezo. Sasa haiwezekani mambo makubwa haya au *allegations* nyingi kiasi hiki ukategemea kwamba ndani ya wiki moja au mbili au tatu itakuwa imekamilika, hata kidogo! Yes! Kwa hiyo, tukishakamilisha tutalirejesha.

**SPIKA:** Ahsante, sasa kama wanajua wawe wanasaidia pia.

Sasa tunaendelea na swali lingine, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali lifuatalo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye Bunge la Bajeti la mwaka huu wa fedha mwezi wa nane, nikichangia hotuba ya ofisi yako nilihoji namna ambavyo Bodi ya Kahawa imeundwa bila kuzingatia sheria lakini pia na kanuni zake kutungwa bila kushirikisha wadau.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe mwenyewe katika maelezo yako na baadaye Waziri wa Kilimo akitoa maelezo ya nyongeza mlieleza kabisa kwamba ni kweli mmebaini kwamba sheria ya Kahawa ya mwaka 2001 Namba 23 imekiukwa na kwa maana hiyo mtaivunja au kurekebisha ile Bodi. Leo ni miezi mitatu tangu nimezungumza hapa Bungeni hakuna hatua iliyochukuliwa.

Je, unawaeleza nini Watanzania na wadau wa zao la Kahawa kuhusiana na jambo hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwenye Bunge lililopita suala hili lilijitokeza na kusema kweli baada ya pale tumefanya kazi kubwa ya kuchunguza kwa sababu kulikuwa na madai mengi lakini moja ilikuwa ni suala hili la mgongano wa kimaslahi ambalo lilidaiwa kwamba limekuwa likijitokeza dhidi ya Mwenyekiti wa Bodi lakini kulikuwa na madai vilevile ya baadhi ya wajumbe wa Bodi ile kuwa wameingia au wameteuliwa bila kuzingatia misingi ya kikanuni na kisheria lakini vilevile kulikuwa na madai mengine ya jumla jinsi ambavyo Bodi ilikuwa inaendesha shughuli za Kahawa.

Kwa hiyo, tumelifanyia kazi. Naweza nikasema ni kama tumemaliza kwa maana ya kupata maelezo kutoka pande zote zinazohusika lakini tulichofanya tumelazimika sasa kumshauri mwenye mamlaka ambaye ndiye anafanya uteuzi wa Mwenyekiti ili yale mengine yaweze ku-flow bila matatizo makubwa. Kwa hiyo, tunaamini akishatupatia maelekezo yake basi zoezi litakamilika.

**SPIKA:** Ahante, Mheshimiwa Zambani, swali la nyongeza!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, swali la nyongeza ni kwamba nilipokuwa nauliza swali la msingi nilizungumza masuala mawili ya msingi na la kwanza umelijibu vizuri nashukuru kwa hatua za Serikali ambazo zinaelekea kuchukuliwa.

Lakini sehemu ya pili inahusiana na kanuni za mwaka mwaka 2012 ambazo zimeruhusu ununuzi wa Kahawa mbichi au *Cherry* na bila kuzingatia maamuzi ya wadau wa zao la Kahawa lenyewe na tunakwenda karibu kwenye msimu mwingine wa zao la Kahawa kwa maana ya mwaka 2012/2013.

Waziri Mkuu, unawahakikishia nini wadau wa zao la Kahawa kwamba mpaka msimu unaofuata wa Kahawa kanuni hizo zitakuwa zimesharekebishwa tayari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli lakini hilo niseme tu nilipitiwa kulieleza vilevile.

Tulichofanya baada ya mjadala Bungeni sisi tulikaa Serikali na tumepitia kanuni zote zinazodaiwa za miaka ya tangu 2009 mpaka 2012, tumejaribu kutazama vilevile namna wadau wakubwa walivyoshirikishwa katika zoezi lile na kubaini maeneo ambayo tunafikiri yawekwe kwa namna ambayo itaweza kweli kusaidia kujibu maslahi ya Watanzania.

Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Zambi kwamba tunakwenda na mazoezi yote mawili kwa wakati mmoja, imani yangu ni kwamba kabla ya msimu ujao hili zoezi juu ya kanuni na hili la Bodi pamoja na wajumbe wengine wa Bodi tutakuwa vilevile tumeyakamilisha.

**SPIKAI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Habibu Juma Mnyaa!

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa masikitiko ni kwamba nchi yetu hivi karibuni imeingia katika .....

**SPIKA:** Sauti, halafu muwe *brief*, naomba muwe *brief*!

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Nchi yetu imeingia katika machafuko ambayo kumetokea uvunjifu wa haki za binadamu. Kwa mwezi mmoja tu uliopita wa Oktoba tumeshuhudia kwa kesi ya kuuawa kwa RPC Barlow Mwanza, kijana Koplo Said Abdulrahman kule Bububu Zanzibar, kijana Salum Hassan Mhaju Amani wa Feshi Zanzibar na hivi juzi siku ya *Eid el Haji* itakuwa tarehe 26 akakamatwa kijana Hamadi Ally Kaini, Nyerere Zanzibar na Polisi pamoja na vikosi vingine wasiopungua 20. Baba yake mzazi kwenda kuuliza akafukuzwa na Polisi.

Lakini kijana yule baadaye siku ya pili baada ya Baba yake kufukuzwa kwenye vituo vyote vya kesho yake akaambiwa mtoto wake amefariki nenda Mochwari katika hospitali ya Mnazi mmoja na akaonekana na madonda makubwa, kafariki mikononi mwa Polisi.

Je, ni kwa nini Jeshi la Polisi linashiriki katika uvunjifu wa haki za binadamu mkubwa nchini na mauaji makubwa, na nini hatua za Serikali itakazochukua kukomesha mambo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kutoa maelezo kidogo tu kuhusiana na swali zito la Ndugu yangu Mheshimiwa Mnyaa.

Mauaji yoyote yanapotokea ni mauaji, na kwa hiyo taratibu za kisheria ni lazima zizingatiwe na kama kutatokea kama upo ushahidi wa kutosha kuonyesha kwamba mauaji yale ni ya makusudi wote tunajua kwamba sheria zinataka kitu gani kichukuliwe dhidi ya mhalifu huyo. Kama itatokea kwamba ni mauaji ambayo yataelezwa kwamba hayakuwa ya kukusudia vilevile hatua za kisheria ambazo ni lazima zichukuliwe na mtu apate adhabu stahiki.

Sasa kwa kila tukio la mauaji linalotokea kubwa ni uchunguzi unaofuatia baada ya hapo. Umetaja *RPC* Mwanza na yako mengine mengi ambayo vilevile hukuyataja lakini yametokea, na kila hilo lina maelezo yake na hatua ambazo zimechukuliwa kwa kila moja. Sasa bahati mbaya hili la Zanzibar ambalo umelieleza la juzi sikuwa na taarifa nazo mimi. Lakini tunachoweza kuahidi tu ni kwamba kama limetokea uchunguzi stahiki utachukuliwa na kama wapo ambao wamehusika na jambo hilo ni dhahidi kabisa hatua zinazostahili zitachukuliwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyaa kwa kifupi swali la nyongeza!

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:**  
Mheshimiwa Spika, nashukuru!

Mheshimiwa Waziri Mkuu, uchunguzi wa kisayansi ulifanyika na watu wakakamatwa katika kesi ya Mwanza,



na Zanzibar kuna watu wakakamatwa katika kesi ya Bububu na wengine wakakamatiwa Tanga.

Kinachoshangaza hapa ambacho ndiyo nahitaji Serikali itoe ufafanuzi wa kutosha kwamba ni kwa nini inatumika *capital punishment* kama ile iliyotokea Shereyuu, Piki na sasa hivi inatokea Bububu na maeneo mengine ya Zanzibar.

Kwa nini itokee *capital punishment* na wakati kuna mauaji makubwa yaliyotokea ambayo yalitusikitisha Wazanzibar wote ya Rais wetu wa kwanza Marehemu Abeid Aman Karume na haikutokea *capital punishment*, ulitafutwa utaratibu wa kisheria, wauaji wakakamatwa na wakapelekwa Mahakamani. Kwa nini yatokee haya leo katika karne hii ya Sayansi leo na Serikali iyanyamazie kimya?

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, si hoja nani kua, si hoja hata kidogo! Kama ameua ni Askari na upo ushahidi unaoonyesha kua kwa makusudi hatua za kisheria zitachukuliwa. Kama ameua ni mwanasiasa kama mimi, si hoja bali hoja hapa ni kwamba hakuna mwenye haki ya kuchukua uhai wa binadamu mwenzake.

Kwa hiyo, mimi nataka nikuhakikishie tu kwamba hili kama limetokea kwa maelezo uliyonipa uchunguzi utafanyika na hawa wanaohusika watachukuliwa hatua zinazostahili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Antony Gervas Mbassa!

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Awali ya yote napenda kushukuru kauli ya jana ambayo ilitolewa hapa Bungeni ya kurejesha fao la kujitoa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa, Mifuko hii ya Hifadhi za Jamii imeanzishwa kwa mujibu wa sheria na kwa kuwa, Mifuko hii inachangiwa na mwajiri na vilevile mfanyakazi mwenyewe. Lakini kumekuwepo na malalamiko kwamba baadhi ya watu wakistaafu wanalipwa fedha kidogo sana na hususani katika mfuko wa *NSSF*.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, na kwa kuwa, leo hii kuna watu wamechangia tangu mwaka 2008 mpaka mwaka 2010 lakini pesa zao hazionekani katika mfuko huu. Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu mifuko hii ambayo haitunzi fedha za wanachama wao?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa hili kidogo linakwenda kwenye sekta.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nafikiri nimemwelewa lakini *of course* yapo mambo mengi ameyaingiza pale, lakini moja kubwa ambalo limejitokeza ni kwamba kwa nini mtumishi anapokuja kustaafu anachokipata kinaonekana

ni kidogo kuliko pengine ambavyo mfuko ulidhaniwa ungeweza ukatoa.

Sasa, kwa upande wa Serikali mifuko hii yote imetungwa kwa mujibu wa sheria ambayo tuliipitisha hapa Bungeni, lakini ni kweli kwamba mimi na wewe hata Watanzania walio wengi hilo unalolisema linaonekana ni kweli lipo. Kwa hiyo, tulichofanya Serikalini tumejaribu kukaa na mifuko hiyo yote kwa mujibu wa taratibu zilizopo sasa za sheria ili kuona ni namna gani hizi *Pension Schemes* zinavyoweza kukaa sasa na kutazama upya namna ya kuboresha mafao kwa ajili ya wafanyakazi wao. Sasa wengine wamekuja na mifumo midogomidogo mbalimbali ambayo inaweza kumsaidia mfanyakazi lakini bado itabidi kwa kweli kufanyike uchunguzi wa kina (*actuarial study* kubwa) ili kuweza kuona ni namna gani tunaweza kwa kweli tukaboresha mafao ya mtumishi anapokuja kustaafu ili anachopata kimwezeshe pengine kumudu maisha katika uzee wake.

Kwa hiyo, nadhani zoezi hilo tunaendelea nalo na wao wenyewe wanalifanyia kazi, tunaamini watafika mahali pazuri tunaweza tukapata pengine mwanga mzuri zaidi.

Lakini tumeruhusu vilevile ushindani ndani ya mifuko hii makusudi tu ili tuweze kuchochea mwelekeo mzuri wa kila mfuko kufanya kazi ya ziada ili kuboresha mafao yao.

**SPIKA:** Pia kesho kutakuwa na semina kuhusu haya masuala kama hayo kwa Dkt. Mbassa yatakuwa ni mazuri zaidi.

Swali la nyongeza!

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru!

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu hili sasa limekuwa kero na hususani hata kwa baadhi ya waajiri na watu wanaotoa huduma, kwa mfano, hospitali zilizopo chini ya Makanisa. Watumishi wengi wamekuwa wakikimbia na kwenda kutafuta ajira Serikalini kwa sababu wanajua baadaye watapata mafao mazuri na kwa sababu hospitali hizi nyingi zipo chini ya mfuko wa hifadhi wa *NSSF*, ndiyo malalamiko yao makubwa na hospitali yangu ya Wilaya ya Biharamulo ikiwemo.

Je, unawahakikishiaje Watanzania au watumisni hawa kwamba sasa mafao yao yataweza kurekebishwa pamoja na kauli uliyoitoa hapo mwanzoni?

Ahsante sana!

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Waziri Mkuu! (*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, si rahisi kwa Serikali kutoa kauli ya namna hiyo moja kwa moja kwa sababu kwa mujibu wa sheria kila mfukouna utaratibu

wake wa namna ya kuingiza mafao na kuboresha mafao kutegemea na uchunguzi utakaokuwa umefanywa kitaalamu ili kuweza kuona ni namna gani wanaweza wakaongeza.

Mimi imani yangu ni kwamba baada ya kuwa tumefungua mwanya sasa kwa mifuko hii kushindana, kila mfuko utajitahidi kuboresha mafao yake hata *NSSF* hawatakubali kubaki nyuma kwa sababu hiyo.

Kwa hiyo, mimi nadhani tufanye subira tuone hizi jitihada mpya zitazaa mwelekeo wa namna gani katika siku za usoni, itakuwa ndiyo suluhu ya kweli kwenye jambo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante, sasa nimwite Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumekushuhudia wewe hapa Bungeni wakati mwingine unatoa ufafanuzi kwa baadhi ya maswali anayoulizwa Waziri mwingine. Je, ni wakati gani sasa Makamu wa Pili Rais ambaye pia ni Mbunge mwenzetu humu ndani atasimama na kuweza kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maswali yanahusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar?

**SPIKA:** Hilo rahisi kweli, Mheshimiwa Waziri Mkuu!  
(*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimjibu Mheshimiwa Rukia swali lake kama ifuatavyo:-

Unajua kinachotokea kwani nini? Ni kwamba nchi ni lazima ijipangie utaratibu wake wa namna ya kuendesha shughuli zake na mara nyingi utakuta shughuli hizo zimeainishwa kwenye Katiba ya nchi na kwenye sheria zinazohusika. Sasa kwa mfumo ulivyo hivi sasa, Waziri Mkuu ndiye anayeshughulika na masuala ya ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama Kiongozi wa Serikali.

Sasa, natambua na ninakubali kabisa kwamba Ndugu yangu Makamu wa Pili wa Rais kwa upande wa Zanzibar kwa maana ya Serikali ya Zanzibar ni kama Pinda alivyo kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini kwa bahati sijui niite mbaya, kwa mfumo ulivyo, uwepo wake hapa Bungeni siyo kwa sababu ya nafasi yake ya Makamu wa Pili wa Rais, bali ameingia kama Mbunge wa Jimbo upande huo kuja hapa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hata kama ingekuwa ni lazima tumuombe na yeye atoe ufafanuzi unaweza ukajitokeza lakini katika sura ambayo itabidi pengine ama tuombe ridhaa ya Spika mwenyewe kama atakubali lakini utakuta mara nyingi itabidi aseme siwezi kufanya hivyo kwa sababu Katiba yenyewe haikusema hivyo. Kwa hiyo, pengine ni suala la Kikatiba zaidi kuliko tu la kutaka liwe au lisiwe.

Lakini kwenye vikao vingine ndiyo maana huwa tunampa nafasi kwenye *briefing* na kwenye maeneo mengine kwa sababu ni vikao *informal* hivi vingine ambavyo vinakwenda kikatiba na kisheria inawezekana

pengine tatizo lipo hapo lakini mimi naheshimu sana utaratibu na ndugu yangu na rafiki yangu pale tunaheshimiana sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Rukia kweli una swali la nyongeza?

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, ni kwa nini yeye yupo hapa kama ni Mbunge kama tulivyo Wabunge wengine, akawa yeye ananyamaza tu hawezi kuuliza swali wala kutoa ufafanuzi hata pale alipoombwa jana na Mbunge mwenzake kujibu swali wakati Kanuni za Bungeni zinaruhusu?

**SPIKA:** Kanuni nilisema haziruhusu, siyo kweli hiyo. Mheshimiwa Waziri Mkuu! (*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sisemi tusimwonee ndugu yangu Makamu wa Pili wa Rais, lakini ninachosema ni kwamba mimi nina hakika na yeye ana mtihani mkubwa sana kwa sababu upande mmoja yaani upande wa Zanzibar ni kiongozi, kuna wakati nina hakika anatamani sana kuniuliza mimi kama Mbunge lakini akikaa akajikuta ni Makamu wa Rais anamhoji Waziri Mkuu nadhani anapata kigugumizi na yeye, *okay!*

Sasa hii yote unaweza ukaona jinsi jambo hili lilivyo, kwa hiyo unaweza ukaona jinsi jambo hili lilivyo, kwa hiyo,

nadhani linahitaji pengine kwenye marekebisho ya Katiba au katika Katiba mpya inayokuja pengine tulitazame tuone ni namna gani liwekwe lakini liwekwe bado likitambua nafasi hiyo. Ndiyo maana umeona sisi tumeona katika mazingira ya kawaida tukasema Mzee utatuvumilia, kaa na sisi lakini ujue kwamba kuna mtihani huo ambao kusema kweli kwa sasa hivi hatuna jibu la moja kwa moja.

Kwa hiyo, twende na hili lakini nadhani baada ya muda kwenye Katiba mpya pengine litakaa vizuri zaidi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante. Mimi nilipata tatizo la wapi kwa kumweka, lakini nimeshinda, si anakaa pale? Nilipata tatizo la wapi namweka Makamu wa Rais lakini, anakaa pale! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrew Kigwangala, swali lingine!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ili niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, waasisi wa Taifa letu wameturithisha tunu moja kubwa ambayo imekuwa ni tamaduni ya nchi yetu nayo ni amani, utulivu, upendo na mshikamano wa kitaifa. Katika siku za usoni yaani katika miaka hii ambayo mimi naweza nikasema nimeingia kwenye *active politics* za nchi yetu, nimeshuhudia uvunjifu mkubwa sana wa amani, hali ambayo inatishia usalama wa taifa letu.



Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa *precedence* hiyo wenzangu wamenukuu baadhi ya mifano mbalimbali ambayo inaashiria upotevu wa amani ambayo tumeirithi na tumeendelea kuwa nayo kwa muda mrefu.

Mimi naomba nielezee tu kitu kimoja kinachohusiana na udini kwa sababu unanitisha sana inapotokea hali ya mpasuko ambao unatokana na mtangamano wa dini zetu na hii imekuwa ikihusishwa sana na baadhi ya vyama vya siasa na hapo ndipo kitisho kinapokuwa kikubwa sana kwangu.

Ninapenda kujua kwamba Serikali inachukua hatua gani kuweza kudhibiti vuguvugu la upotevu wa amani ambao unahusishwa kwa ukaribu sana na dini mbalimbali hususani majuzi tumeshuhudia makanisa yakifanyiwa vurugu na Waislamu lakini pia msahafu ukikojolewa na kumekuwa na *background* ya masuala ya dini kwenye siasa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba maelezo yako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza niombe nikubaliane na Dkt. Kigwangalla kwamba tunu tuliyo nayo ya amani na utulivu ni silaha muhimu sana kwa Watanzania kwa maendeleo yake na ndiyo maana utakuta viongozi wengi tunalisimamia kwa nguvu sana katika kuwaasa Watanzania kila mmoja kwa nafasi yake atambue hilo.

Sasa, ni kweli yamekuwepo matukio ya hapa na pale ya uvunjifu wa amani, mengine ni mazito na hata tunavyozungumza hivi si kwamba yametulia lakini bado jitihada za vurugu zinajengwa kila siku. Ni kweli vilevile kwamba wakati mwingine zinachukua sura ya dini, lakini wakati mwingine haina sura ya dini. Sasa nini tufanye?

Juzi mimi nimejaribu kukaa na baadhi ya wenzangu tukasema pengine iko haja kwa Taifa, kwa hapa tulipofika pengine tuwe na mjadala wa kina kwa Watanzania wote juu ya umuhimu wa jambo hili la kuenzi amani na utulivu na wala tusianzie kwenye ngazi ya Taifa bali twende tukaanzie ngazi ya chini kama njia mojawapo ya kuhimiza Watanzania kutambua jambo hili zito tuje tufike juu.

Na inawezekana kabisa mwisho wa yote tunaweza tukawa na maelewano ya pamoja juu ya umuhimu wa jambo hili na kila mmoja kutambua.

Lakini pili, wakati mwingine napata picha au hisia tu, na ni mara nyingi viongozi wote tu hasa sisi tulioko Serikalini, wakati mwingine tunasahau kwamba tuko hapa kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye ametuweka na ametupa kazi ya kuhakikisha kwamba tunaongoza Watanzania wenzetu kwa njia ya amani na utulivu. Tunadhani tupo tu kwa sababu tumejiweka wenyewe na kwa hiyo hatuna wajibu wa kuenzi hili jambo kwa uzito unaostahili.

Mimi nadhani tusifanye hivyo, kila mmoja aelewe kwamba analo jukumu la msingi.

Lakini tatu, katika muda huu wakati tunaendelea sasa kulizungumza kwa pamoja, kulijadili kwa pamoja, kutafuta

mustakabali wa nchi hii kwa pamoja, sisi kama Serikali tutaendelea kutumia kila lililo ndani ya uwezo wetu kuhakikisha tunasimamia amani na utulivu. Sasa katika hili, yako mambo mengi mnaweza mkayatumia, wakati mwingine ni subira, lakini subira nayo inapofika ukomo inabidi mchukue hatua zinazostahili.

Kwa hiyo, tutajitahidi kwa kadri tutakavyoweza kwenda na jitihada zote zenye mchanganyiko wa namna ya kukabiliana na jambo hili ili kuhakikisha tu kwamba, Watanzania wanaendelea kufanya kazi kwa amani, waishi kwa amani na kila mmoja aweze kujiona kwamba ana haki stahili kila upande.

Lakini wakati huu vilevile niombe sana hasa viongozi wetu wa dini wote, wajaribu nao katika maeneo yao kulizungumza jambo hili kwa moyo wa dhati ili kuweza kuhakikisha kwamba jambo hili linakuwa ni sehemu yetu ya maisha ya kila siku. Tunajua viko vikundi vya watu wachache ambao wao hata ukifanya nini wanaona njia pekee ya wao kuishi ni fujo na vurugu. Haya tumesema hatutayaachia. (*Makofi*)

Hivi vikundi vidogo vidogo kwa sababu ya fujo zao tumesema hapana, na kwa kweli katika hili itabidi tuwaombe radhi Watanzania pale watakapoona tumechukua hatua pengine zinaonekana kali ni kwa sababu ni lazima tulinde amani na utulivu kwa nguvu zetu zote. Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa jambo hili, lakini nadhani mwisho wa yote mdahalo au mjadala wa pamoja kuanzia ngazi ya chini mpaka ya Taifa ili kusaidiana

kuelimishana wenyewe pengine itakuwa ni njia nyingine ya kusaidia kama nchi tuweze kujiona kwamba ni wamoja bila kujali itikadi zetu za kidini, kisiasa, kikabila na maeneo mengine.

**SPIKA:** Bado swali la nyongeza Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo!

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza viongozi wa Mashirika ya Kikristo kwa tamko walilolitoa.

Nililisoma kwa kweli lilikuwa limejaa diplomasia, hekima na busara iliyotukuka, nikapata picha kwamba hivi kama Wakristo ambao Mekanisa yao yamechomwa wameweza kuwa wavumilivu kiasi cha kutoa tamko la kidiplomasia kama lile.

Ni kwanini busara isitumike pia kuwataka Waislam nao waseme, hasa yale ambayo yanawasibu, kile kikundi kidogo ambacho anakizungumzia hapa na ikiwezekana kuliko kuli- *handle* suala hili kisheria, likawa *handled* kisiasa ili ukapatikana muafaka wa mezani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba maelezo yako kuhusiana na hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme kwamba nimeliona tamko hilo vilevile, lakini sitaki na mimi nionekane natoa picha kana kwamba, kwa upande wa dini ya Kiislam Waislamu wote jambo hili la vurugu linalojitokeza kutokana na vikundi vichache vichache wanaliafiki, hapana! Wako ambao wametoa maelezo na kwa kweli wamesisitiza sana juu ya umuhimu wa jambo hili na wanawajua kabisa ni nani wanafanya vurugu hizi na pengine kwa malengo ambayo si lazima yakawa yanahusiana moja kwa moja hata na dini. Kwa hiyo, wanajua na tuko nao katika kujaribu kuona namna gani tupate suluhu ya kweli katika jambo hili. Hilo nilifikiri ni vizuri tukaelewana hivyo.

Lakini kubwa unalolisema ambalo na mimi ninaliafiki kabisa kwamba, lazima madhehebu ya dini haya kwa pamoja, kwa umoja wao, wamekuwa wakikutana mara nyingi sana kama madhehebu, wakati huu pengine wanahitajika kukutana zaidi kuliko wakati mwingine wowote ili wawe na kauli ya pamoja kuhusiana na matukio, lakini kubwa hasa mwelekeo wa uvunjifu wa amani unaojitokeza sasa.

Kwa hiyo, nataka niseme nawapongeza sana viongozi wa madhehebu ya dini yote ya kiislamu na kikristo, wanaoona umuhimu wa suala hili la amani na utulivu kwa nchi yetu na Watanzania kwa ujumla.

Kwa ujumla tulaani sisi wote kwa pamoja vitendo vya wale wote ambao wamejikita katika kujaribu kuvunja amani

ya taifa letu. Tukifika hapo nina hakika kabisa kazi yetu itakuwa ni nyepesi zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukushuru tena kwa maelezo mazuri, na pia ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maswali ambayo yalikuwa mazito. Tulikuwa na watu saba, bahati mbaya wawili wamekosa nafasi lakini ni kwa sababu ya uzito wa maswali yenyewe. Kwa hiyo, nawashukuru sana.

Tunaendelea, Katibu.

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 30

### **Hitaji la Maji Ludewa**

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wa Ludewa Mjini watapatiwa huduma ya maji safi na salama, hasa ikizingatiwa kuwa Ludewa Mjini ni Makao Makuu ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Ludewa unakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 12,646 wanaohitaji maji safi na salama kiasi cha meta za ujazo 1,561 kwa siku. Upatikanaji wa maji kwa sasa ni meta za ujazo 509 kwa siku kutoka katika vyanzo vya Nyalawale na Mkondachi. Kutokana na takwimu hizi ni dhahiri kuwa kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama kwa matumizi mbalimbali ya wakazi hao.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2010/2011, Serikali iliidhinisha shilingi milioni 54.1 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji ya kutegwa wa Mdongwa wenye uwezo wa kuzalisha meta za ujazo 100 kwa siku.

Kazi zilizofanywa ni pamoja na kujenga banio (*intake*), kufunga mabomba hadi eneo la tanki umbali wa meta 1,700, kufunga mabomba ya kusambaza maji umbali wa meta 3000 na ujenzi wa tanki la maji lenye meta za ujazo 75. Mradi huu ulikamilika Juni, 2011 na unafanya kazi. Hata hivyo, maji yanayopatikana hayatoshelezi mahitaji yaliyopo kwa wakazi wa mji wa Ludewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maji na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mkoa wa Iringa, imeajiri Wataalam Washauri, Kampuni ya *Don Consult* ya Tanzania kwa kushirikiana na Kampuni ya *PÖyry Environmental GmbH* ya Ujerumani kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa maji kutoka chanzo cha maji cha Mto Ilunga na

kuandaa makabrasha ya zabuni. Kazi ya usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika mji wa Ludewa imekamilika na kuwasilishwa kwa msimamizi wa mradi huo ambaye ni Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Iringa, Wizara ya Maji na Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali cha kutangaza ili kazi ya ujenzi ianze. Hivyo ni matarajio ya Serikali kwamba kukamilika kwa mpango huu kutasaidia kupunguza tatizo la maji lililopo kwa wakazi wa mji wa Ludewa.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kukiri kwamba mji wa Ludewa una tatizo kubwa la maji, mimi nilikuwa Ludewa wiki nzima nimerudi Jumapili, hali ya maji mjini Ludewa ni mbaya kuliko kasi ambayo Serikali inatueleza kwamba wanaendelea nayo, hasa ule mtaa wa Makanisa.

Hali ni mbaya sana hata mimi mwenyewe nilikosa maji ya kuoga, nimenunua maji ya chupa na ndiyo nimenawa uso na sehemu muhimu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hili suala la kibali lina tatizo gani? Kutokana na hali ilivyo ikibidi tuambiwe ni lini hiki kibali kitapatikana ili kutatua tatizo la maji ya Ludewa?

Swali la pili, hata katika mazingira yale ambayo yameishavuka kiwango cha upembuzi yakinifu, mambo ya vibali na hasa haya maji ambayo yanahusisha Benki ya Dunia kama ilivyo hapa bado fedha haziendi, unakuta hata visima vingine vimechimbwa tu na kutelekezwa hasa pale Bulamba, Magunga na Kalukekero, Mwibara na maeneo



mengine ya Tanzania. Tunataka Serikali itwambie kwa nini hata pale ambapo vibali vilishapatikana na maji yakachimbwa imetelekezwa na miradi haiendelei, tatizo ni nini? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Lwenge, eeh, leo nimemkumbuka Lwenge. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kuhusu matatizo ya maji katika mji wa Ludewa, ni kweli usanifu ulifanyika kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi na katika maswali niliyojibu juzi kuhusu miji midogo ya Tunduru na Ilula Mkoani Iringa usanifu ulifanyika na ulibaini kwamba katika huu mji wa Ludewa jumla ya shilingi bilioni 13 (Dola milioni nane) zinahitajika kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji pamoja na kuleta maji kwenye chanzo kipya kama kilivyoanishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanyika usanifu, kazi inayofanyika sasa ni kutafuta hizo fedha na jinsi fedha zitakavyopatikana basi zitaingizwa kwenye mpango na wananchi wa Ludewa watapata maji. Sasa hivi bado tunatekeleza mpango wa haraka. Ukiangalia kwenye mradi wa vijiji kumi (10) Ludewa tayari wanatekeleza mradi wa vijiji viwili; Ilunda na Mbila na wana fedha jumla ya shilingi bilioni 1.3 ambazo zitatumika kutekeleza miradi hii ya maji vijijini.

Swali la pili kwamba fedha haziendi, sina uhakika kama hilo ni kweli kwa sababu fedha zote ziko kwenye Halmashauri za Wilaya, kilichokuwa kinasubiriwa ni vibali. Kwa hiyo, baada ya vibali kutolewa, fedha zinaanza

kutumika mara moja. Tunao mfano, mpaka sasa hivi jumla ya Halmashauri 103 zimeshapata vibali na inatakiwa ziwe zimeanza ujenzi, ikiwa ni pamoja na mradi mmoja ambao nimeutembelea kwa Mheshimiwa Kange Lugola ambao tayari umeanza kutekelezwa na ujenzi wake unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, la msingi ni kwamba fedha ziko kwenye Halmashauri, vibali vikitoka kazi inaanza mara moja. Ninachowaomba baada ya vibali kutoka wafanye kasi ya utekelezaji wa ule mradi. Ahsante sana.

Na. 31

### **Matatizo ya Maji – Ukonga**

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA** aliuliza:-

Liko tatizo kubwa la ukosefu wa maji safi na salama Jimboni Ukonga hasa ikizingatiwa kuwa wananchi wa Jimbo hilo hawajapata fursa ya kutumia maji toka *DAWASCO*:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba visima virefu kwenye maeneo yenye huduma za jamii kama vile hospitali, shule na kadhalika ili kuwaepusha wananchi na magonjwa ya mlipuko?

(b) Kama kauli inayosema “Maji ni Uhai” ni ya kweli; je, kwa nini Serikali imeshindwa kuwa na mpango unaotekelezeka wa kupeleka maji Jimboni Ukonga kwa zaidi ya miaka 50 sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatekeleza Mpango Maalum wa kuboresha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. Mpango huo unalenga kuongeza wingi wa Maji kutoka lita milioni 300 kwa siku za sasa hadi kufikia lita milioni 710 kwa siku ifikapo mwaka 2014. Miradi ifuatayo itatekelezwa kupitia mpango huo:-

(i) Upanuzi wa mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini;

(ii) Kulaza bomba la ziada toka mitambo hiyo hadi kwenye matanki yaliyopo Kimara na Chuo Kikuu cha Ardhi;

(iii) Kuchimba visima katika Bonde la Kimbiji na Mpera;

(iv) Kujenga bwawa la Kidunda; na

(v) Kujenga mtandao wa kusambaza maji katika Jiji la Dar es Salaam likiwemo Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Spika, Mpango huo utakidhi mahitaji ya maji Jijini Dar es Salaam hadi mwaka 2032 na utagharimu jumla ya shilingi bilioni 564.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango huu maalum wa kuboresha huduma ya maji katika jiji la Dar es Salaam umeshaanza na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini umefikia asilimia 70;

(ii) Kazi ya kulaza Bomba kuu toka Ruvu Chini hadi matenki ya Chuo Kikuu cha Ardhi itaanza mwezi huu wa Novemba 2012; na

(iii) Tathmini ya kumpata mkandarasi wa uchimbaji wa visima 20 vya Kimbiji na Mpera imekamilika na taarifa ya tathmini imepelekwa Benki Dunia kwa ajili ya kupata kibali.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaendelea kusubiri kukamilika kwa Mpango Maalum wa kuboresha huduma ya maji katika jiji la Dar es Salaam, Serikali itaendelea kuchukua hatua za muda mfupi kuboresha huduma ya maji katika Jimbo la Ukonga ikiwemo hatua ya kuchimba visima.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kupata nafasi ili niweze kumuuliza maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba ina mpango wa muda mfupi wa kuchimba visima katika Jimbo la Ukonga. Je, Serikali sasa iko tayari mara moja kuchimba visima vitatu ambavyo niliviomba mwaka 2011 ambavyo vilikuwa vichimbwe katika Kata za Chanika, Msongola katika eneo la Mvuti ambalo halina maji kabisa ili wananchi waweze kupata maji mara moja?

Swali lingine la nyongeza, kwa kuwa mwezi uliopita nilifanya ziara katika visima vyote vilivyochimbwa katika Jimbo la Ukonga nikiwa nimefuatana na Maafisa wa Serikali na kwa kuwa niliweza kubaini ufanisi mkubwa sana katika visima hivyo unatokana na elimu ya mara kwa mara inayotolewa katika Kamati za Maji, je, Serikali iko tayari sasa kuendelea kutoa elimu hiyo kwa Kamati nyingine za Maji ambazo zinasimamia visima vingine ambavyo vimechimbwa na wafadhili mbalimbali ili kuweza kupata ufanisi unaostahiki? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Mwaiposa kwa sababu tarehe 25 alifanya ziara ya kutembelea visima vya maji vilivyopo kwenye Jimbo lake ambavyo ni jumla ya visima kama 21 na akajihakikishia kwamba kuna visima vinafanya kazi vizuri ambavyo viko 16. Hii ni hatua nzuri sana, nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijibu maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekubali, baada ya ziara yake yeye mwenyewe amependekeza visima vitatu vichimbwe ambavyo ni katika maeneo ya Mogo, Mlandege, Mvuti na Chanika. Wataalam wa DAWASA wameshafanya usanifu na hivyo ujenzi wa visima hivi utafanyika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, nakubali na tunashukuru kwa maoni yake kwamba inabidi tuendelee kutoa elimu jinsi ya kutumia visima hivi ili viwe endelevu na mahali pengine elimu hiyo tutaiendeleza na sisi sote humu ni wawakilishi tuwaeleweshe wananchi wetu waweze kutumia vizuri visima hivi ili hii rasilimali ya maji iwe endelevu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba Serikali imetenga shilingi bilioni 564 kwa ajili ya mpango wa kuboresha maji Dar es Salaam.

Majibu haya ni tofauti na Kauli za Serikali za huko nyuma ya kwamba Baraza la Mawaziri limepitisha mpango wa shilingi bilioni 653. Kwa hiyo, maana yake tunarudi nyuma kwenye uwekezaji wa maji Dar es Salaam.

Kwa kuwa hivi karibuni nilikuwa na ziara pamoja na Waziri wa Maji ya kuzindua visima ambapo amejionea hali halisi ya mradi wa mabomba ya Wachina ambapo maji hayatoki na maeneo mengi ya pembezoni ya Msumi,

Makabe na maeneo ya pembeni ya Malambo Mawili, Msiga na kwingineko hakuna kabisa mabomba. Je, Serikali iko tayari sasa kurudi kwenye ule mpango wa awali na kuhakikisha kwamba zinaongezwa fedha shilingi bilioni 82 kama zilivyokuwa zimepitishwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kutandaza mabomba ya maji kwenye maeneo yote ya Dar es Salaam yasiyokuwa na maji na kuhakikisha mtandao wa maji wa Wachina unatoa maji? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, inawezekana kweli kuna tofauti ya takwimu lakini la msingi fedha tunazoziongelea hapa ni zile ambazo tumepata mkopo wa nafuu kutoka India jumla ya dola milioni 178, tunaongelea fedha za ndani zilizotengwa na Serikali shilingi bilioni 117 kwa ajili ya bomba la Ruvu Chini na tunaongelea fedha kupitia MCC dola milioni 36 kwa ajili ya kuboresha chanzo cha maji Ruvu Chini na zile za Kimbiji na Mpera. Kwa hiyo, hizo zote kwa ujumla wake ndiyo zinazoleta utekelezaji wa miradi hii ya kuboresha maji Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sasa la msingi hapa ni kuona yale ambayo tumeyaainisha. Tumesema kwamba kwanza tunapeleka fedha kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa maji, hiyo ni kazi ya kwanza. Lakini kazi ya pili ni kwa ajili ya kusafirisha maji toka yanakozalishwa kwenda kwenye matenki Dar es Salaam. Kazi ya tatu sasa ndiyo hiyo ya kuweka miundombinu ya kuyapokea hayo maji ili yaweze kuwafikia wananchi. Kwa hiyo, kama itaonekana zinahitajika fedha zaidi ili kutekeleza jukumu hilo, lazima

utenge fedha za kiasi hicho ili wananchi wa Dar es Salaam nzima wapate maji. Kwa hiyo, nadhani limekuwa *taken care*, cha msingi ni kama huo mkakati upo.

Na. 32

### **Sera ya Madini ya Mwaka 1997**

**MHE. KABWE Z. ZITTO (K.n.y. MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI)** aliuliza:-

Moja kati ya mikakati ya Sera ya Madini ya Mwaka 1997 ni kuhakikisha wachimbaji wadogo wanapata uwezo wa kukopa katika taasisi za fedha:-

(a) Je, wachimbaji wadogo wa Almasi wanaozunguka Mgoji wa Mwadui na *New Almasi* wamewezeshwa vipi ili nao waweze kuwa wachimbaji wakubwa?

(b) Je, ni wataalam wangapi wa fedha hasa waliobobea katika sekta ya madini wanashirikiana na asasi zinazofanya kazi na wachimbaji wadogo ili kupata mitaji?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zitto anamwakilisha Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ambaye ameondoka kwa majukumu mengine. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-



Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester M. Kasulumbayi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya mwaka 1997 ilifutwa na Sera ya Madini ya mwaka 2009 ambayo ndiyo inayotekelezwa kwa sasa. Mabadiliko hayo ya sera yanalenga kuhakikisha kuwa sekta ya madini inaleta mchango mkubwa katika pato la Taifa pamoja na suala la kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini hapa nchini limepewa msisitizo ili shughuli za wachimbaji hao ziweza kuwa na tija na kuongeza mchango katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasulumbayi kama ifuatavyo:-

Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Madini ya mwaka 1997 moja ya hatua muhimu zilizochukuliwa na Serikali ni kuwawezesha wachimbaji wadogo wa Almasi wanaozunguka Mgodu wa Mwadui na *New Almasi*, ni kurasimisha na kuwapatia maeneo wachimbaji wadogo ili waweze kuyamiliki kisheria.

Jambo hili lilifanyika mwaka 2004 ambapo eneo la Maganzo, lenye ukubwa wa takribani kilomita za mraba 137.43 lilitengwa kwa wachimbaji wadogo na kupimwa viwanja zaidi ya 1000 ambavyo viligawiwa kwa wachimbaji wadogo wa madini ya Almasi. Wachimbaji hao waliendelea kupata huduma ya ugani kutoka katika ofisi ya madini ya Kanda ya Kati Magharibi iliyoko mjini Shinyanga.

Aidha, Serikali imeanzisha mpango wa kutenga fedha kwa ajili ya mfuko wa kuendeleza shughuli za uchimbaji mdogo nchini. Mpango huu unatarajiwa uwe endelevu ili wachimbaji wengi waweze kunufaika na mitaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina takwimu za idadi ya wataalam wa fedha waliobobea katika sekta ya madini ambao wapo nje ya ajira ya utumishi wa umma wanaoshirikiana na asasi zinazofanya kazi na wachimbaji wadogo kwa lengo la kuwapatia mitaji. Katika kuhakikisha kuwa kuna msukumo wa kutosha wa kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa ufanisi zaidi, Wizara yangu imewaelekeza wataalam wa madini wa Wizara na Taasisi zake wakishirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mamlaka ya Elimu ya Ufundi (*VETA*), Shirika la Viwanda Vidogo (*SIDO*) na Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*). Kwa kutumia ushirikiano huu wenye taaluma katika nyanja mbalimbali ikiwemo utaalam wa fedha, tutaweza kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowakabili wachimbaji wadogo nchini kwa lengo la kufanya uchimbaji mdogo kuwa endelevu na wenye manufaa kwa Taifa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maelezo hayo ya Serikali. Nina maswali madogo tu mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa mujibu wa Sheria mpya ya Madini, sheria ya mwaka 2010 tumesema kisheria kwamba hivi sasa madini yote ya vito kwa maana ya *Tanzanite* na mengine yatachimbwa na Watanzania tu na pale ambapo

itaonekana kwamba mitaji mikubwa inahitajika ndipo ambapo wageni wataweza kuhusishwa. Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa mapendekezo ya kuchimba *Tanzanite* kwa kutumia *Botswana model* ambapo Serikali inakuwa na asilimia 50 na wachimbaji wakubwa wanakuwa na asilimia 50?

Swali la pili, pale *Williamson Diamond* wakati tunafanya ubinafsishaji na kuuza hisa za Serikali, kuna Watanzania ambao walikuwa wanafanya kazi pale na mpaka leo bado hawajalipwa mafao yao. Serikali imechukua hatua gani mpaka sasa kuhakikisha wazee wale ambao walikuwa wanafanya kazi pale *Williamson Diamond* wanalipwa mafao yao inavyostahili kama jinsi ambavyo inatakiwa kwa mujibu wa sheria? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 inatambua hivyo na kwa hakika tunapaswa kusimamia sheria na Wizara iko kwenye mchakato wa kufanya maamuzi hayo na kwa kweli hatuna budi kufuata ile *Botswana model* ya *fifty by fifty* (50% - 50%). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchakato unaendelea wa kuona ni jinsi gani tunaweza kuitekeleza kwa sababu uwekezaji ule bado ni mkubwa. Wale watu wapo, tumefanya nao kazi vizuri, kwa hiyo kwa kweli tunapaswa kutumia busara katika kufanya maamuzi yale, lakini hatuepuki kutumia Sheria ya Madini iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na wafanyakazi wa *Williamson Diamond* ambao hawajapata mafao hadi sasa, ninaomba Mheshimiwa Mbunge akubali nikalifanyie kazi kwa sababu sina habari za kutosha juu ya jambo hili. Ahsante.

**MHE. RACHEL R. MASHISHANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na wachimbaji wadogo hawa wanaozunguka mgodi wa Mwadui na *New Almasi* na Maganzo kupewa leseni za uchimbaji kihalali kabisa, lakini kumekuwa na malalamiko ya kuvamiwa na wachimbaji wakubwa. Je, Serikali inazungumza nini kuhusu uvamizi huo wa wavamizi wakubwa kwa wachimbaji wadogo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kumejitokeza baadhi ya maeneo kwamba wachimbaji wakubwa wanawavamia wachimbaji wadogo, lakini wakati mwingine ni vizuri na wachimbaji hawa wadogo na wenyewe kujua taratibu za kisheria na kanuni zinazoweza kuwafanya wakawa wamiliki halali wa maeneo kuliko kuwa wako nyuma kila wakati wakingojea kusaidiwa.

Kwa sababu kwa kweli katika kutafuta mali, kutafuta uchumi mzuri ni vita kidogo, kwa hiyo, lazima wachimbaji wetu wadogo pamoja na msaada mkubwa ambao Serikali tunatoa kwao na tumeweka mkakati maalum wa kuwasaidia, lakini wajitihadi kuzijua sheria na taratibu ili

wasifanye makosa ambayo mara nyingi kwa hakika ukifuatilia jambo lolote mahali ambapo wamevamia unakuta walau walichelewa kuchukua hatua za kukamilisha umiliki wa maeneo yao.

Na. 33

### **Kuvipatia Umeme Vijiji vilivyopitiwa na Mkondo wa Umeme**

**MHE. NEEMA M. HAMID** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba vijiji vyote vilivyopitiwa na nguzo za umeme vinasambaziwa umeme huo kwa matumizi ya wananchi walio tayari kulipia gharama?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema M. Hamid, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa huduma ya umeme kuwa ni kichocheo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa dhana hiyo, Serikali inafanya kila jitihada za makusudi kusambaza umeme vijijini kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kutokana na vyanzo vyetu wenyewe na kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini inatekeleza mpango wa awamu ya pili wa umeme vijijini ambapo vijiji 364 vitakuwa vimepatiwa umeme ifikapo

mwishoni mwa mwaka 2012 na vingine 557 vinatarajiwa kupatiwa umeme ifikapo mwishoni mwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia washirika wa maendeleo inaandaa mkakati wa kuipatia umeme vijiji vilivyopitiwa na njia za umeme nchini mfano ni Iringa, Shinyanga ambako kuna mradi wa *Backbone transmission line* yenye urefu wa kilomita 667 ambapo SIDA na NORAD wameonesha nia ya kugharamia usambazaji yaani *distribution* ya umeme katika vijiji 51 ambapo *transmission line* inapita. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa katika mpango huu ni pamoja na ujenzi wa njia za umeme za msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 818 na ufungaji wa *transforma* 471 ambao shilingi bilioni 44.8 zitatumika.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilitoa ahadi katika vijiji ambavyo viko Wilaya ya Wanging'ombe kuwa vitapatiwa umeme na vijiji hivyo ni Dulamu, Palangawano, Makoga, Mambegu, Lubuga, Ituramba, Korinto na Kanana. Je, vijiji hivi viko katika hiyo *plan* ya awamu ya pili ya umeme ambayo amesema kwamba ikifikia mwaka 2012 vitapatiwa umeme? Kwa sababu ni takriban miaka mitatu sasa bado vijiji hivyo havijapatiwa umeme tangu ahadi hiyo ilivyotolewa.

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili, kuna vijiji vingine ambapo nguzo zimepita katika Wilaya hiyohiyo ya

Wanging'ombe vijiji hivyo ni lhanja, Ilebula Shuleni, Iponda na Mlangila, je, navyo kazi hiyo ya kuwapatia umeme itaanza lini?

**SPIKA:** Haya sijui ni vijiji vipi maana ni kibao.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, katika Ilani ni kweli tuliahidi kutekeleza miradi ya umeme katika Wilaya ya Wanging'ombe katika vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja. Lakini niombe tu kwamba Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kujiridhisha kwamba utekelezaji wake utakuwaje kwa sababu nimetaja hapa kwamba ni vijiji vingi sana takribani 557 katika awamu inayoishia mwaka 2013 ambavyo vitashughulikiwa ili tuweze kuona kama na vijiji hivyo vipi vimo lakini kama havipo tunaweza tukawasiliana tuone namna gani tunaweza tukafanya.

Mheshimiwa Spika, lakini nizungumzie tu kwa vijiji ambavyo ametaja umeme unapita lakini vijiji vyenyewe havijashushiwa umeme. Kama nilivyosema na mara zote nimekuwa nikisema hapa kwamba tutajitahidi sana kwa kadri tutakavyoweza kwa kupitia miradi ya *REA* na *TANESCO* tuweze kushusha umeme mahali popote pale ambapo nguzo zinapita ili wananchi waweze kunufaika na kichocheo hiki cha uchumi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Napenda kujua, Mheshimiwa Waziri

alifanya ziara karibu nchi nzima na amekuwa akitoa ahadi za umeme kushuka kutoka katika maeneo ambayo nguzo zimepita. Maelezo haya ambayo Serikali wanatoa, utekelezaji katika ngazi ya *TANESCO* Wilayani, Mkoani na hata *TANESCO* Makao Makuu ni tofauti na wamekuwa wakidhihaki wanasema hizo ni kauli za kisiasa. Je, Serikali inasema nini katika hili kwamba tunawaahidi wananchi mambo ambayo yanatekelezeka au ni kweli zinatoka ahadi za kisiasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mangungu yeye ni mwanasiasa na wanasiasa wote tunafahamu na hata wasio wanasiasa wanafahamu kwamba mambo yote yanayotekelezwa yanaanzia kuzungumzwa katika siasa. Sasa kama kuna mtu ambaye sisi viongozi tukitoa maelezo ya kisiasa ambayo ndiyo ni ya kisera halafu wanasema hayo ni maneno ya kisiasa nadhani hajui anachokisema.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Serikali ni thabiti kwamba tutashusha umeme na ndicho tutakachofanya na tumekwishafanya na tunaendelea kufanya. Kwa hiyo, anayesema hivyo ni kwamba anajifurahisha na nichukue nafasi hii kuwaomba sana wataalamu wetu ambao wanatekeleza Sera za Umeme nchini kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Muhongo kwamba tunachokisema ndicho kitakachofanyika, hatutakubali upinzani wa kishetani kuzuia maendeleo katika miradi ya umeme. *(Makofi)*



**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, nina swali dogo tu, tunaposema kwamba tushushe umeme kwenye hivyo vijiji, *experience* inaonyesha kwamba gharama ya kuvuta umeme Tanzania ni kubwa sana. Kwa nini Serikali isifike wakati iseme kwamba kwa sababu gharama ya kuvuta umeme na mtu ukijenga nyumba, nyumba ikaisha hata kwa miaka mia na nyumba unavyoenda kuishi mtu ulikuwa unalipa gharama ya umeme maana yake ni kwamba *TANESCO* watakuwa wanapata faida. Sasa kwa nini Serikali isione kwamba gharama ya mtu kuvuta umeme ukaingiza nyumbani kwako iwe bure kuanzia mwaka wa fedha unaokuja au kama haiwezekani basi wakati una-*apply* kuingiza umeme halafu ile gharama kubwa *TANESCO* wakae nayo kila jiji litakapokuwa linalipa bili inakuwa *charged* kidogo kidogo mpaka utakapomaliza yote hayo? Naomba maelezo ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Wenje anajaribu ku-*address* hapa jambo ambalo kwa hakika hata sisi Wizarani tumekuwa tukilijadili na kwa hatua ya awali tuliona tukitumia njia ambazo tumeweza kwa mjadala na kuangalia hali halisi ya gharama ya uingizaji umeme majumbani na ndicho tulichokisema wakati wa Bunge la Bajeti tukaweza kushusha kutoka takribani shilingi 400,000/= na zaidi hadi 177,000/=, mahali ambapo hamna umbali mkubwa.

Lakini tukaendelea hivyo kutoka shilingi 1,000,000/= kwa vitu wanavyoviita nguzo sijui waya, lakini nasema mteja wa umeme wa Tanzania hana haja ya kujua anahitaji nguzo, anahitaji waya na vitu vingine, yeye anachotaka ni umeme. Tunachohitaji ni kumpa umeme na tumwambie gharama ni kiasi gani. Kwa hivyo sisi tutajitahidi kusimamia hilo lakini ridhika na hatua ya awali hiyo ambayo itaanza kutekelezwa kuanzia mwezi Januari, gharama ya shilingi 177,000/= ambayo mimi naamini ni *affordable* inawezekana kwamba tutaendelea kuangalia *techniques* zingine na kweli hiyo ndiyo *modern way* ya kufanya *investment* na kuwawezesha watu waweze kupata umeme. Tutajitahidi sana kuhakikisha kwamba tunatafuta hizo njia zingine hasa kwenye maeneo ambayo yana gharama kubwa ili wananchi wetu waweze kupata umeme.

Na. 34

### **Fedha Kwa ajili ya Chakula cha Mahabusu**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibiwa suala langu Na. 34, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii kwa kutwaa fupa la U-NEC hapo jana na hii ni kutokana na umakini wake, uwezo wake, umahiri wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba uruhusu swali langu Na.34 lijibiwe.

(a) Je, Serikali inatenga kiasi gani cha fedha kwa mwaka kwa ajili ya huduma za chakula kwa mahabusu katika vituo vya Polisi Zanzibar?

(b) Je, Serikali ina taarifa kuwa Askari hulazimika kukopa au kutumia fedha zao kuwanunulia mahabusu chakula na huduma nyingine licha ya kuwa mishahara yao ni midogo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba nipokee pongezi lakini ni kazi kubwa inayofanywa na Wabunge na wapiga kura kwa ujumla. Kwa hiyo, Wabunge wa Vyama vyote walishiriki kutafuta ushindi wangu. Nawashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashimu Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya kulisha mahabusu kwa nchi nzima hutofautiana mwaka hadi mwaka kutegemea ukomo wa bajeti ya Wizara. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Vituo vya Polisi Zanzibar vilitengewa kiasi cha Tshs.130,000,000/= na mwaka 2010/2011 Tshs. 100,000,000/= zilitengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa kwamba Askari hulazimika kukopa ama kutumia fedha zao kuwanunulia mahabusu chakula na huduma nyingine, jukumu hilo ni la Serikali pekee.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imepanga kiwango hicho cha fedha, kuna taarifa hadi sasa vituo vingi vya Zanzibar vinaendelea kupata usumbufu huo hali inayosababisha baadhi ya watuhumiwa kulala na njaa. Je, Serikali inachukua hatua gani kupata ukweli wa tatizo hilo?

Pili, ikiwa Serikali inapeleka fedha hizo na kuna baadhi ya vituo hukosa hata maji ya kunywa. Je, anawaambia nini Wazanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza ni taarifa kwamba kuna baadhi ya vituo vinapata matatizo haya. Naomba baada ya majibu haya tuonane na Mheshimiwa Ayoub ili anisaidie kujua ni vituo gani na tujue hatua gani za kuchukua au kufanya utafiti.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo pamoja na kwamba agizo hili lipo, pia kuna maelekezo kwamba kwa yale maeneo ambayo kuna kantini za Polisi inapotokea kwamba hakuna chakula kabisa cha mahabusu basi maelekezo huwa yanatolewa ili waweze kuazima mpaka fungu litakapokuja. Lakini pia katika hali ya kawaida, hatutegemei Mkuu wa Kituo amwachie mahabusu afike

mahali pa kufa au karibu ya kufa bila ya kuchukua hatua ya kufanya mawasiliano ili tatizo hili liondoshwe.

Mheshimiwa Spika, hili swali la kwanza kwamba kuna tatizo hili kama alivyosema Mheshimiwa, tutachukua hatua ya kuchunguza, bajeti ni bajeti lakini bado busara zinaweza kutumika ili hili lisiwe tatizo.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ningependa kujua mahabusu na wafungwa wanatakiwa kula mara ngapi kwa siku na ni chakula cha aina gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, mahabusu na wafungwa wanatakiwa wale mara tatu kwa kila siku. Kwa wale ambao ni wafungwa, kunakuwa na ratiba kwenye Magereza yao kwamba kuna ugali na maharage, kuna wali na samaki na kadhalika. Wale ambao wako mahabusu, chakula chao kinaamuliwa pale kituoni na wanapewa chakula ambacho ni *very nutritious* na kinatosha.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamesimama kuomba kupewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza)*

**SPIKA:** Tunaendelea, tafadhali muda. Kiongozi wa Kambi ya Upinzani muda. Naomba muangalie muda kwa sababu *already* nina *five questions which I have not yet covered*. Haya Mheshimiwa Zitto!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali itamke rasmi kwamba kilichosemwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kwamba wafungwa na mahabusu wanapaswa kula milo mitatu kwa siku ndiyo amri ya Serikali. Naomba Serikali itamke hilo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, taratibu za namna ya kula na kuishi katika Magereza yetu zinaendeshwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ya Uendeshaji Magereza na hazitamkwi Bungeni.

Na. 35

### **Makosa Yanayopelekea Kifungo cha Maisha**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Je, ni aina gani ya makosa yanayoweza kumsababishia mtu kufungwa kifungo cha maisha?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mtu anaweza kufungwa kifungo cha maisha pale anapotenda kosa la jinai lenye adhabu ya kifungo cha maisha. Adhabu za makosa zenye kupelekea mkosaji kufungwa kifungo cha maisha zinapatikana kwenye Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 (*Penal Code, Cap. 16*) na Sheria nyingine zilizotungwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 na Jedwali la Kwanza la Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 (*Criminal Procedure Act, Cap. 20. R. E. 2002*), aina ya makosa ambayo yanaweza kumsababishia mtu kufungwa kifungo cha maisha ni pamoja na:-

(i) Makosa yanayotendwa kinyume na utaratibu wa Umma, mfano, kuficha uhaini, kuchochea uasi na uharamia;

(ii) Makosa dhidi ya utawala wa mamlaka halali, mfano, utorohaji wa wafungwa au mahabusu wa makosa ya kunyongwa au kifungo cha maisha;

(iii) Makosa dhidi ya binadamu, mfano ubakaji, kuzini na maharimu, kuua bila kukusudia;

(iv) Makosa dhidi ya mali, mfano, kugushi hati ya mirathi, kuchoma nyumba na kadhalika; na

(v) Makosa dhidi ya usafirishaji madawa ya kulevyo.

Mheshimiwa Spika, haya ni baadhi ya aina ya makosa yanayoweza kumsababishia mkosaji kifungo cha maisha.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza napenda kumpongeza Waziri kwa jinsi anavyotujibu majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Magereza ni eneo la adhabu na kurekebisha tabia za wafungwa, je, ni lini Serikali itaondosha adhabu hii ya kifungo cha maisha na badala yake iweke adhabu mbadala, kwa sababu mtu akifungwa anaenda kurekebisha tabia, mtu huyu atolewe, asifungwe maisha yake yote, arudi uraiani aweze kujenga taifa lake baada ya kurekebisha tabia zake. Je, ni lini Serikali itarekebisha sheria hii?

La pili, kwa kuwa nchi yetu inaendeshwa katika misingi ya kuthamini misingi ya haki za binadamu na kwa kuwa adhabu ya kifo inakiuka misingi ya haki za binadamu, je, Serikali ina mkakati gani wa kuondosha adhabu hii ya kifo na kuweka adhabu mbadala?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, katika suala la kwanza, alitaka kujua ni lini sasa Serikali itaondoa adhabu ya kifungo cha maisha na badala yake kuweka adhabu mbadala. Kwanza kabisa, kwa upande wa Mahakama na Serikali tunahamasisha sana adhabu mbadala na hata katika mwaka huu tulipokuwa tunaazimisha Siku ya Sheria, tarehe 1 Februari kaulimbiu yetu ilikuwa ni kuhamasisha adhabu mbadala kwa makosa ambayo yanaweza kukidhi adhabu mbadala. Lakini napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba si makosa yote unaweza kutoa adhabu mbadala, yako



makosa mengine ambayo ni mazito kama ambavyo nimeeleza katika mifano ya makosa ambayo yanapelekea kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Spika, lakini pili aliuliza pia ni lini Serikali sasa itaondoa adhabu ya kifo ili kuweza kuhakikisha kwamba tunathamini haki za binadamu. Ni kweli kwamba ziko baadhi ya nchi ambazo tayari zimeshafuta adhabu ya kifo, pia ziko nchi zingine ambazo hazijafuta lakini hazitekelezi adhabu hii ya kifo, Tanzania tunaangukia katika kundi hili la pili. Tunayo adhabu ya kifo katika vitabu vyetu vya kisheria lakini ukiangalia toka mwaka 1978 mpaka 1987 na kuanzia mwaka 1995 hadi hivi sasa hakuna mtuhumiwa mfungwa ambaye amenyongwa, lakini pia nipongeze juhudi za Marais wetu kupitia Rais Mstaafu Mkapa katika kipindi chake aliwapunguzia adhabu ya kifo wafungwa 100, lakini pia Mheshimiwa Rais Kikwete katika uongozi wake hadi sasa ameshawapunguzia adhabu ya kifo kuwa adhabu ya maisha watuhumiwa 75. Ahsanteni.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda tu kujua kwa kuwa katika nchi yetu lakini kwa majibu nilikuwa nataka kuuliza swali ambalo nafikiri kwa kiasi fulani yamejibiwa lakini niulize. Kwa kuwa nchi yetu bado tunayo adhabu ya kifo katika Sheria zetu za Jinai na nchi nyingine tayari wameshafuta na wengine wanatekeleza, je, ni makosa gani yanayopelekea mtuhumiwa kuhukumiwa adhabu ya kifo?

**SPIKA:** Mheshimiwa alijibu wakati anajibu swali la msingi. Swali lenyewe la msingi ndio linasema hivyo. Tunaendelea na Wizara ya Fedha.

Na. 36

### **Ukusanyaji Kodi Nchini**

**MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MHE. DAVID Z. KAFULILA)** aliuliza:-

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye uwezo mdogo sana wa kukusanya kodi ikilinganishwa na vyanzo vingi vilivyopo kwa sababu ya uadilifu mdogo wa viongozi tulionao na watendaji wengine:-

(a) Je, Serikali imetambua ni maeneo gani katika uchumi hayakusanyi kodi ipasavyo au yanakusanya chini ya kiwango kutokana na ulegevu wa Serikali?

(b) Kwa takriban miaka mitano Bunge limekuwa likilalamikia kuhusu mapato duni yanayokusanywa na Serikali kwenye Kampuni za simu, je, kwa nini Serikali imekataa kuhakikisha Kampuni hizo zinalipa kodi stahiki?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kabla sijamjibu Mheshimiwa David Kafulila, naomba kutoa *clarification* kuhusiana na swali la jana la Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwamba jibu ambalo tumelitoa hapa lilikuwa ni la mwaka 2010/2011. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba radhi kwa usumbufu wa hiyo *typing error* ambayo imetokea. Hata hivyo kama alivyosema Waziri kwamba taarifa zote zinapatikana pale Wizara ya Fedha na tutampatia kama tulivyokuwa tumeahidi jana.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kukumbusha kwamba Serikali haifanyi ulegevu hata kidogo katika ukusanyaji wa mapato. *Infact* hiki ndicho kitu cha kipaumbele na kama ataangalia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha ukurasa wa 89, 90, 91 hadi 92 ataona kwamba *trend* inakwenda juu katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yameonekana kuwa na upungufu katika kukusanya kodi ni pamoja na sekta isiyo rasmi, sekta ya mali ya asili na biashara za makampuni yenye mitandao ya Kimataifa (*Multinational Corporations*). Hata hivyo, Serikali imeendelea kuboresha weledi wa watendaji katika kusimamia Makampuni yenye mitandao ya Kimataifa na kubadilishana taarifa na uzoefu na mamlaka za nchi nyingine ambazo zinasimamia mapato.

(b) Mheshimiwa Spika, sekta ya simu ni miongoni mwa sekta ambazo zinakua kwa kasi katika matumizi ya sayansi na teknolojia na zinamilikiwa na makampuni yenye mitandao mipana. Usimamizi wa kodi katika sekta kama hii unahitaji kuwa na utaalamu na teknolojia ya hali ya juu. Hatua kadhaa zimeendelea kuchukuliwa na Serikali ili kuhakikisha zinapata mapato yake halali kutoka kwenye sekta hizo.

Hatua hizo ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania kupitia Idara ya Walipakodi wakubwa kuanzisha Kitengo cha Kodi za Makampuni ya Kimataifa "*Intenational Tax Unit*" kwa lengo la kubaini na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya aina hii.

Aidha, utaalamu katika usimamizi wa sekta hii unaendelea kuboreshwa ndani ya Mamlaka ikiwa ni pamoja na kuongeza ujuzi katika shughuli za ukaguzi, uchambuzi wa takwimu zitokanazo na uendeshaji wa Makampuni katika sekta na matumizi ya njia za teknolojia ya kielektroniki katika kusimamia mifumo ya uendeshaji wake kwa nia ya kupata takwimu sahihi. Sambamba na jitihada hizi, *TCRA* iko katika hatua za mwisho za kupata mkandarasi wa kufunga kifaa maalum kitakachoweza kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za mauzo za Makampuni ya Simu zitakazosaidia Serikali kupitia *TRA* kukusanya kodi halali na sahihi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza tangu mwaka 2007 tumekuwa tukisikia kwamba Serikali inafanya mpango wa kununua mtambo maalum kwa ajili ya kuweza kuratibu suala zima la Makampuni ya Simu ili iweze kujua kwamba wanapata mapato kiasi gani na hatimaye Serikali kuweza kukusanya kodi zake kikamilifu. Katika majibu yake ya msingi ameeleza kwamba *TCRA* wako katika hatua za mwisho za kumpata mkandarasi ili kuweza kukusanya kodi yake kikamilifu.

Napenda Serikali iweze kutupatia kauli leo, mchakato huu wa kumpata mkandarasi na hadi kuja kukamilika kwa kufungwa kwa mtambo huo na kuanza kutumika utakamilika lini?

Swali la pili, imekuja kuonekana kabisa kwamba kwa mujibu wa uchunguzi na utafiti ambao umefanywa kwa macho, Sera ya Ubinafsishaji imeweza kuathiri viwanda vingi hapa nchini ikiwemo Kiwanda au Mgodidi wa Chumvi Uvinza na hivyo kuisababishia Serikali ya Tanzania kuweza kupoteza kodi nyingi na hatimaye kuweza kususua kwenye suala zima la kupata haya mapato ya kutosha. Napenda leo hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini hasa wa eneo la Uvinza, Serikali ina mpango gani tofauti na ule wa kumfilisi mwekezaji ambaye alibinafsishiwa mgodi huu kwa thamani ya shilingi 90,000,000 na hatimaye ameng'oa mitambo ile na kwenda kuiuza nchini Iran kwa thamani ya shilingi bilioni 4.5. Serikali inatoa kauli gani na ni kwa nini isimfilisi na kuweza kumfikisha Mahakamani kwa sababu tumepata hasara? Leo kodi ambayo tuliyokuwa tunakusanya kupitia kuwepo kwa mgodi ule ingekuwa ni kubwa sana. Ningeomba kauli ya Serikali

**SPIKA:** Eeeh! Hotuba kabisa. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na *TCRA* kupata mtambo, tunakusudia mwaka huu wa fedha kupata huyo mtaalamu yaani kukamilisha ufungaji wa huo mtambo ambao utatupatia takwimu sahihi.

Kama unavyojua kwamba hii ni *international procurement* lazima tufuate taratibu zote za manunuzi, kwa hivyo hatujataka tu tukurupuke twende tutafute maana litazuka suala lingine. Kwa hivyo, tunafuata taratibu zote za manunuzi kumpata mtaalamu na hatimaye kufunga huo mtambo wa kuweza kupata takwimu sahihi. Lakini kama utafuatilia hotuba ya Wizara ya Sayansi na Teknolojia wanakusudia mwaka huu wa fedha kupata mtambo huo uwe tayari umeshawekwa.

Aidha, suala la Uvinza, nadhani hili Mheshimiwa Mbunge limeshafuatiliwa na taarifa ipo. Hata hivyo, kama atakuwa ana maelezo ya ziada *exactly* ya kitu ambacho anakitaka pale, naomba tu tuonane ili atupe *what exactly* anatakaje kwa sababu taarifa tayari zimeshatolewa na kwamba huyu mtu alifuata taratibu zote, amenunua mtambo mpya pale, ameuza ule mkongwe na taratibu zote tayari alifuata. Kwa hivyo, kama kutakuwa kuna maelezo ya ziada, naomba atupatie ili twende tukafuatilie tena maana tayari tumeshalifuatilia. Ahsante.

## **Bei Kubwa kwa Vifaa vya Ujenzi**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Bei ya vifaa vya ujenzi hapa nchini imepanda sana kiasi cha kuwafanya wananchi wengi kushindwa kuvinunua hivyo kuendelea kubaki kwenye makazi duni:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa VAT kwenye vifaa hivyo ili bei iweze kupungua na wananchi wamudu kununua vifaa hivyo?

(b) Je, inakuwaje vifaa vinavyotengenezwa hapa nchini kwa kutumia malighafi ya hapa nchini kama sementi, chokaa, vyuma bado ni ghali kuliko vile vinavyoagizwa kutoka nje?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mbunge Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, bidhaa zote zinatozwa kodi ya VAT kwa kiwango cha asilimia 18 kwa sasa ya thamani ya bidhaa husika bila kujali kwamba bidhaa imeagizwa kutoka nje ya nchi au imezalishwa ndani ya nchi. Bei za bidhaa zinatokana na gharama mbalimbali zikiwemo za uzalishaji

kama vile malighafi, upatikanaji wa malighafi, umeme, maji, nguvukazi, miundombinu na teknolojia, pamoja na faida ya mfanyabiashara mwenyewe. Kwa hivyo ukiunganisha vyote hivyo ndivyo ambavyo vina *constitute* ile bei ya bidhaa yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kama zilivyo bei za bidhaa zingine, bei za vifaa vya ujenzi hazipangwi kwa kutumia kigezo cha kodi ya *VAT* peke yake bali ni kutokana na msukumo wa nguvu ya soko yaani mahitaji ya bidhaa yenyewe na hali ya upatikanaji wake.

Hivyo basi, Serikali kwa sasa haioni sababu ya kuondoa Kodi ya *VAT* kwenye vifaa vya ujenzi kwa sababu *VAT* siyo kiashiria pekee kinachoongeza bei ya vifaa vya ujenzi.

(b) Mheshimiwa Spika, gharama za uzalishaji wa bidhaa hutofautiana kati ya nchi na nchi, kutegemea wepesi wa upatikanaji malighafi, gharama za uzalishaji na usambazaji katika nchi husika ambao kimsingi haulingani baina ya nchi na nchi. Gharama za uzalishaji na usambazaji nchini kwetu bado ziko juu ikilinganishwa na wenzetu, hivyo ni dhahiri bei za bidhaa zinazozalishwa hapa nchini zitakuwa juu kuliko zinazoagizwa toka nje ya nchi. Kodi ya *VAT* inaongeza bei ya bidhaa lakini changamoto kubwa ni gharama za uzalishaji pamoja na usambazaji. Aidha pia, gharama hizo zinajumuisha teknolojia duni pamoja na miundombinu ambayo tunayo sasa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.



Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bei ya vifaa vya ujenzi kwa Mikoa ya pembezoni ikiwepo Tabora, Kigoma na Mikoa mingine ni mara mbili ya bei halisi ya bidhaa kwenye Mikoa mingine kama ilivyo Dodoma, Dar es Salaam na maeneo mengine. *Cement* hapa Dodoma ni shilingi 15,000/- Tabora ni shilingi 25,000/- mpaka 27,000/- na bati na nondo ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeacha biashara huria kwa wafanyabiashara kupanga bei wanavyoona wao na mara nyingi wanapenda *super profit* yaani kuwe na faida kubwa kwenye biashara zao.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na Tume ya Udhibiti wa Bei kwa bidhaa mbalimbali ili wananchi wasiendelee kunyonywa na wafanyabiashara wanaopenda *super profit*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa kila nchi zina utaratibu wao wa kusaidia wananchi ndani ya nchi yao kuweza kumudu gharama kubwa za maisha na kwa kuwa maisha bora kwa Watanzania wote ni pamoja na kuwa na nyumba bora za kuishi. Serikali ina utaratibu gani endelevu wa kuhakikisha kwamba wananchi wote hata walioko pembezoni wanaishi kwenye nyumba bora kama ilivyo Watanzania wengine?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**

Mheshimiwa Spika, kwa Mikoa ya pembezoni kama nilivyokuwa nimesema hapo awali, bei inakuwa kubwa kutokana na gharama za usafirishaji. Kwa sababu kama tunavyojua, jioografia ya Tanzania ni kwamba viwanda vingi vimekuwa *centralized* hasahasa Dar es Salaam lakini hiyo

inatokana na kwamba wakisha-*produce* ina maana wavisafirisha kuelekea katika hiyo Mikoa ya pembezoni, kwa hiyo, ina-*constitute* gharama za usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, cha muhimu hapa, kama ulivyoona Serikali inajitahidi sana kuweka miundombinu ili gharama zile za usafirishaji kupeleka bidhaa katika Mikoa ziwe *very sufficient* na hivyo kumfikia mtumiaji wa mwisho katika bei iliyonafuu. Kwa hiyo, hilo sio jambo tu la Wizara ya Fedha *per se*, ni jambo la Serikali nzima kuweza kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu sahihi na ambayo iko *efficient* na *effective* kuhakikisha kwamba bidhaa zinapofika Mikoa ya pembezoni zinakuwa *affordable* kwa wananchi wanaokaa katika sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na suala la wananchi kuwa na *affordable accommodation*, nadhani hilo limo katika mipango ya Serikali na kama ameweza kufuatilia jitihada zinazofanywa, kwa mfano, Shirika la Nyumba limekuwa linatangaza kila mahali kwamba sasa hivi tunajenga nyumba zilizobora na *affordable* kwa mwananchi wa kawaida kuweza ku-*access*. Kwa hiyo, hilo limo katika mipango ya Serikali na tutahakikisha kwamba kila mwananchi anapata makazi bora kwa sababu sidhani kama Serikali kama yetu ilivyokuwa sikivu itataka kumwona mwananchi wake hakai katika nyumba iliyokuwa bora. Kwa hivyo, hilo limo katika mipango ya Serikali. *Is just a matter of time* basi na hilo nalo litafanikiwa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza hakujibu. Niliulizia Tume ya Udhhibiti wa Bei.

**SPIKA:** Tume ya Udhhibiti wa Bei hayo yamepitwa na wakati.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, namwomba radhi Mheshimiwa Sakaya kwa sababu ya mvuto wa suala lenyewe hili kidogo nilipitiwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Bei ilikuwepo kweli lakini sasa hivi kwa sababu Tanzania tunataka tuwe na uchumi ambao unakuwa *private sector lead*, tumeacha biashara iwe huria. Hata hivyo, Serikali haipendezewi kuona wafanyabiashara wanapata *super profit* kwenye biashara zao. Kwa hiyo, kwa sababu tupo katika mfumo wa uchumi huria, hatuoni sababu ya kurejesha Tume ya Bei kuweza kuingilia uchumi wenyewe. Hata hivyo, hatupendezewi kuona mwananchi hapati bidhaa kutokana na bei ilivyokuwa kubwa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bei za mijini na vijijini ni tofauti kubwa sana na kwa kuwa tuna sera ya kupunguza umaskini, hatuoni kwamba Serikali kwa kuachia bidhaa ziuzwe bei kubwa vijijini au Mikoa ya pembezoni, sera yetu ya kupunguza umaskini itakuwa ni ndoto? Kwa nini hatuigi mfano wa India ambapo bidhaa zote zinazozalishwa na zinazouzwa nchini bei za vijijini ni ndogo kuliko za mjini ili kuweza kupunguza umaskini?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa swali lake la kutoa mfano wa India kwamba India bei ya

bidhaa zilizo vijijini na mijini iko tofauti, ni kweli. Wengi ambao tumefika kule iko tofauti kwa sababu ya *structure* ya viwanda. Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri swali la msingi ambalo limeuliza kwamba hali tuliyonayo Tanzania ambapo kwa bahati mbaya tume-*centralize* viwanda Dar es Salaam, hii ndio sababu kubwa ambayo imesababisha kuwa na bei kubwa katika miji iliyo pembezoni kwa sababu ya *transportation cost*. Lakini suala la msingi kabisa ni sera zetu, sasa hivi tunapoelekea ni lazima tupanue *location* ya viwanda ili baadaye tunapoanza *distribution* ya bidhaa ziweze kuwafikia katika bei ambayo itakuwa ndogo hata wale wa vijijini.

Lakini kwa sasa hivi si suala la kiuchumi kwamba tupunguze bei kwa ajili ya watu ambao wapo pembezoni, ni lazima tuangalie namna gani tunaweza tukawa na sera ambazo zita-*address structure location* ya *industries*. Ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata la Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura atauliza swali hilo.

Na. 37

### **Uvuvi Mdogo kwa Matumizi ya Kawaida.**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA** aliuliza:-

Wananchi wengi waishio kandokando ya Maziwa na Bahari mara nyingi huvua samaki kama kitoweo tu cha familia bila bughudha ya vyombo vya Serikali. Je, kwa nini

wananchi wa vijiji vya Wenje, Nasomba Makande, Kazamoyo, Misechela na Meyamtwao vilivyo kandokando ya Mto Ruvuma wanasumbuliwa sana na Askari wa Maliasili kwa kupigwa na hata kunyang'anywa mali zao wanapovua samaki kwa kitoweo chao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Wenje, Nasomba na Lukala viko kwenye maeneo ya wazi na vinapakana na Mto Ruvuma. Lakini vijiji vya Makande, Kazamoyo, Misechela na Meyamtwaro vinapakana na Hifadhi ya Msitu wa Mwambesi ambayo pia ni Pori Tengefu lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1000. Kwa mujibu wa kifungu cha 19(1) cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori, Namba 5 ya mwaka 2009, Mapori Tengefu yana hadhi sawa na Mapori ya Akiba.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wananchi wengi kuharibu mazingira kwenye maeneo ya wazi, kumesababisha upatikanaji mdogo wa samaki na hivyo wanalazimika kuingia kwenye eneo la pori la Mwambesi ambalo limehifadhiwa na kuvua samaki kinyume cha sheria. Wanapokutwa na kikosi cha doria cha ushirikiano cha mwekezaji ajulikanaye kwa jina la *Tandala Hunting Safaris* na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, wahalifu hukamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi kama taratibu za

nchi zinavyoelekeza. Hata hivyo, yapo matukio mengi ya wananchi kuingia kusingizia kuvua samaki wakati wakifanya ujangili na kuuwa wanyamapori. Mathalani, tarehe 16/3/2011 alikamatwa ndugu Anafi Salumu Mkopoto wa kijiji cha Kazamoyo akiwa na bunduki aina ya *shortgun* na risasi tano ndani ya Hifadhi ya Mwambesi. Mtuhumiwa huyo alifikishwa Kituo cha Polisi na kufunguliwa Jalada namba TUN/IR/271/2012 na kutozwa faini ya shilingi 200,000/- kwa kosa la kupatikana na bunduki na risasi ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5/6/2012 kikosi cha doria ya ushirikiano kutoka Pori la Akiba Selous na Wahifadhi Wanyamapori toka Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru baada ya majibizano ya risasi na wavuvi, zilikamatwa silaha mbili na aina ya *Rifle 375* na *Shortgun* zilizokuwa zikitumiwa na wavuvi wa eneo la Milelani katika Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuliaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, eneo hilo la Tunduru Kusini unapovuka mto Ruvuma unaingia Hifadhi ya Taifa ya Niassa iliyoko nchini Msumbuji. Hivyo, ujangili huo unafanywa pande zote mbili za nchi ya Tanzania na Msumbiji kwa kusingizia kufanya shughuli za uvuvi wa samaki. Aidha, hakuna wananchi kwa taarifa tulizonazo Serikalini waliopigwa kwa kuvua samaki, bali walipelekwa kwenye vyombo vya Sheria na kufunguliwa mashtaka.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, kauli ya mwisho kabisa Mheshimiwa Waziri anasema hakuna

mwananchi yeyote aliyepigwa kwa kuvua samaki, naamini kabisa majibu haya Waziri ameyapata kutoka kwa viongozi wa Idara ya Maliasili Tunduru ambao swali la msingi linawatuhumu. Sasa kwa vile majibu haya Mheshimiwa Waziri ameyapata kutoka kwao, je, mimi mwakilishi wa wananchi wale nikimletea orodha ya wananchi walipigwa, kunyang'anywa samaki tena inaweza ikawa samaki wawili au watatu, hunyang'anywa mali zao ikiwepo baiskeli, je, Waziri analiambia nini Bunge hili, hatua gani atachukua dhidi ya hawa ambao wamempa majibu ambayo amekuja kuwasilisha hapa Bungeni wakati sio sahihi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika jibu la msingi ameeleza kwamba msitu wa Mwambesi una ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 1000 na Jimbo langu la Tunduru lina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 8000. Ni takribani asilimia 23 ya Msitu Tengefu ambao upo katika Jimbo la Tunduru. Je, Waziri atakuwa tayari kukutana na mimi ili tujadili mstakabali wa msitu huu ambao asili yake yake ni kumegwa baadhi ya maeneo ya vijiji kuandaa msitu huu ambapo Sheria iliyopitishwa ya Hifadhi ya Wanyamapori ya mwaka 2009 inatoa mwanya wa Serikali kurudisha maeneo haya kwa wananchi ili yaweze kutengewa matumizi mbadala wanayotaka wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza takwimu ambazo nimezitoa ni kama nilivyozungumza kwenye jibu la msingi kwamba ni kwa taarifa tulizonazo Serikalini na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kama kuna taarifa nyingine tofauti ambazo Mheshimiwa Mbunge au viongozi wengine wa

wananchi watakuwa nazo kuhusiana na tuhuma hizi, niko tayari kuzipokea, niko tayari kukaa naye, niko tayari kuzungumza naye ikiwa ni pamoja na kwenda katika hili eneo ili kuhakikisha kwamba amani kwa ujumla inarejea.

Mheshimiwa Spika, la pili ningependa kupitia Mheshimiwa Mtutura na kupitia Bunge lako Tukufu niwaarifu Watanzania kwamba hali ya ujangili ni kubwa nchini. Hali ya kuuawa kwa wanyama wetu ikiwa ni pamoja na Tembo kuuawa kwa watu kuingia katika maeneo ya hifadhi kinyume na Sheria wakisingizia sababu zozote zile zilizopo huku wamebeba silaha na wakati mwingine tumekamata watu walioingia katika maeneo yetu ya hifadhi wakiwa wamebeba silaha za kivita ikiwa ni pamoja na *Automatic Rifles*, ikiwa ni pamoja na *AK-47*; haya yameendelea na hali ya kuuawa kwa tembo hasa kutokana na kushamiri kwa biashara ya meno ya tembo ambayo hivi karibuni, kama miaka mitano, bei ya kilo ilikuwa ni dola za kimarekani 1000 lakini tunaambiwa ukienda kwenye masoko haya yasiyo rasmi huko duniani imefika sasa kwa kilo dola za kimarekani 1000 na wakati mwingine ni 1100. Kuuawa kwa wanyama hawa ni dharura kubwa ya kitaifa na mimi naomba nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ningepomba nitoe wito kwa wananchi wote, tushirikiane kwa kadri Wizara ya Maliasili na Utalii itakavyoendelea kukaza nyuzi na kuhakikisha kwamba tunadhibiti majangili, ninaomba tupate ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba takwimu za Pori Tengefu kama alivyozisema, eneo tu ambalo ni Pori Tengefu ni kilomita za mrabara 1000 lakini ukubwa wa eneo hili la pori



ni kubwa zaidi ya hapo. Mimi nipo tayari kukutana naye kama nilivyosema na niko tayari kwenda katika hili eneo ili tuweze kupata mwafaka ule ambao unakusudiwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yenyewe yamekwisha. Naomba niwatambue baadhi ya wageni tulionao.

Tanao wageni 34 wa Wabunge wote wa Mkoa wa Mtwara ambao ni Wajumbe wa Jumuiya ya Wazazi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wazazi wa Mkoa ndugu Kasugulu. Wako wapi? Nadhani bado wanaendelea na shughuli zao huko. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Asha Mohamed Omari ambao ni ndugu Fatma Shamte Chumu, ndugu Shaali Zahor Omar, ndugu Bishori Abdalla Tau, wasimame walipo kama wapo. Ahsanteni sana sijui ni ndugu zake au nani. *(Makofi)*

Tuna Mshauri wa *UNDP*, ndugu Anna Hovhannesian, yupo wapi? *She is there, okay*, ahsante sana karibu. *(Makofi)*

Tuna wageni 20 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni wanamichezo na watumishi kutoka Manispaa ya Iringa, wako wapi hawa? Ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanamitindo, pia wanafunzi 12 kutoka vyuo vya elimu ya juu Dodoma wamekuja kwa ajili ya kulitembelea Bunge. Ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Halafu Mchungaji Hosea Mwaijande amekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Mchungaji yuko wapi na yeye. Karibuni sana Mchungaji Mwaijande. (*Makofi*)

Shughuli za kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba watakuwa na kikao chao leo tarehe moja saa saba mchana katika ukumbi namba 231.

Halafu Waheshimiwa Wabunge napenda niwatangazie kuwa kazi ya kujadili maazimio yaliyokuwa yamepangwa kuingia Bungeni kesho bado haijakamilika katika ngazi ya Kamati.

Hivyo kesho siku ya Ijumaa tarehe 2 Novemba, kutakuwa na Semina kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, *Social Security Regulatory Authority* yaani *SSRA* kuanzia saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Semina hii ina lengo la kuwaongezea Waheshimiwa Wabunge uelewa juu ya mifuko ya jamii, uwezeshaji wake pamoja na mabadiliko yanayohitajika ya mfumo wa sekta ya hifadhi ya jamii nchini. Hivyo ni muhimu wote kuhudhuria. Kwa mfano swali alilouliza Mheshimiwa Dkt. Mbassa pale ndiyo mahali pake pa kuuliza na kutokana na uzoefu mbalimbali mlionao huko Majimboni kwenu basi pale patakuwa ni mahali pazuri pa kuuliza. Kwa hiyo, kesho saa tano ukumbi wa Msekwa kutakuwa na hiyo semina.

Halafu ninalo tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye ni Katibu wa Wabunge wa *CUF*, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote

wa *CUF* kuwa kutakuwa na Kikao cha chama leo kitakachofanyika ukumbi wa *basement* saa kumi na moja jioni.

Halafu Ofisi yangu, Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Wabunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa kutakuwa na maonyesho ya nishati mbadala upande wa umeme wa jua, mifumo ya *solar*, itakayofanyika leo tarehe 1 -2 Novemba kwenye viwanja vya Bunge karibu na jengo la ofisi za habari kuanzia saa nne asubuhi. Kwa hiyo, mtu unaweza kupita pale ukajifunza kidogo habari hizo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nimwite Mwenyekiti, Mheshimiwa Mabumba nikafanye kazi kidogo ofisini. Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu!

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester M. Mabumba)  
Aikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu tuendeleee!

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2012** *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3), Act, 2012]*

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa  
Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Naam!

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7). Naomba niisome:-

*“Halikadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba “Mwongozo wa Spika” kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papohapo au baadaye kadri anavyoona inafaa.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata mwongozo wako, Waziri wa Mambo ya Ndani anatamka kwamba Sheria zinazohusiana na Magereza hazielezwi Bungeni. (Makofi)

Kwa mujibu wa Katiba, suala lolote la nchi ni lazima lielezwe Bungeni kwa ile Ibara ya 63. Kwa hiyo, napenda

kupata mwongozo wako kutokana na majibu ya Waziri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Vicent Nyerere, naomba niichukue hoja hii, nitaitolea mwongozo baadaye. Naomba tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

### MAAZIMIO

**Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki *[The Protocol on the Establishment of the East African Kiswahili Commission]***

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali mapendekezo ya kuridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki *(The Protocol on the Establishment of the East African Kiswahili Commission)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kukushukuru wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kuipatia Wizara yangu fursa hii ya kuwasilisha mbele yenu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwani hatua hii muhimu imekuwa ikisubiriwa kwa shauku kubwa na wapenzi na wadau wa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Viti Maalum kwa maelekezo na michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili Azimio hili kwenye vikao vilivyofanyika baina ya Kamati na Wizara yangu tarehe 18 -22 Oktoba, 2012. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwamba michango yao tumeithamini na pia tumeifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sote tunavyojua, dhima ya Kiswahili katika kuwaunganisha wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imetambuliwa tangu zama za ukoloni.

Ndiyo maana kunako mwaka 1930 wakoloni wa Kiingereza waliokuwa wanatawala kanda yote ya Afrika Mashariki yaani nchi za Tanganyika, Zanzibar, Kenya na Uganda walianzisha Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ili kusimamia kwa umakini zaidi maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Kamati hiyo licha ya kubadilisha muundo wake na kuwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili - TUKI na hivi sasa kuwa Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili - TATAKI ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kazi zake za kimsingi zilibaki kuwa ni zilezile. Kwa hakika, lugha yenye uasili wa Afrika Mashariki iliyo na uwezo wa kuwaunganisha watu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanapoelekea kwenye shirikisho ni Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kuanzishwa upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mnamo mwaka 1999, ari ya

kuimarisha ushirikiano katika ukuzaji wa Kiswahili ndani ya Jumuiya iliongezeka na hatimaye imepelekea katika uanzishaji wa chombo mahsusi cha kufanyia kazi hiyo. Chombo hicho ni Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mweyekiti, Itifaki inayowasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuridhiwa ndiyo inayoelezea namna Kamisheni itakavyoanzishwa, majukumu yake, muundo wake na utendaji kazi wake. Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa chombo kitakachoongoza katika ukuzaji na maendeleo ya utumiaji wa Kiswahili, kwa ajili ya umoja wa kikanda pamoja na maendeleo endelevu kiuchumi na kijamii kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 3 ya Itifaki, Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki itatoa ushauri kwa nchi wanachama kuhusu masuala ya utafiti, ufundishaji, kujifunza na usanifishaji wa istilahi na maendeleo ya Kiswahili kama vile utayarishaji sera, kutoa elimu na kuhuisha mitaala. Lengo kuu ni kukuza Kiswahili ili kiwe lugha ya matumizi mapana katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamisheni itafanya kazi ndani ya muundo uliopo wa Baraza la Kisekta linaloshughulikia Kiswahili yaani Baraza la Kisekta la Elimu, Sayansi na Teknolojia na Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Mkutano wa 24 wa Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki uliofanyika Bujumbura Burundi

kati ya tarehe 21 – 26 Novemba, 2011 ulikubali ombi la Tanzania kuwa Makao Makuu ya Kamisheni. Barua rasmi ya taarifa kuhusu uamuzi huu ililetwa Wizarani tarehe 20 Machi, 2012. Tanzania kwa upande wake tayari imeshatoa kilichokuwa Kituo cha Utafiti cha Simulizi Asilia na Lugha za Taifa cha Afrika Mashariki (*Eastern African Centre for Research on Oral Tradition and African National Languages*) kilichopo Zanzibar kuwa Makao Makuu ya Kamisheni. Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeshataarifiwa rasmi kuhusu uamuzi huu wa Serikali ya Tanzania na imeshakikagua kituo hicho na kuridhishwa nacho. Ni muhimu Tanzania ikaridhia Itifaki hii kwani matokeo ya kujiunga kwake ni chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki zitakaposhirikiana katika jukumu hili la kukuza Kiswahili katika mapana yake kikanda, lugha hii itakuwa na kusambaa sehemu kubwa ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Pamoja na hayo, hadhi ya Kiswahili itapanda na kukua na pia kutoa fursa zaidi za ajira kwa wataalamu wake na kitaweza kutumika katika mikutano mingi zaidi ya Kimataifa kama ilivyo sasa katika Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamisheni itasimamia kwa umakinifu zaidi matumizi ya Kiswahili katika Jumuiya. Ni muhimu Kiswahili kikawa lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwani ndiyo lugha pekee ya mawasiliano mapana katika eneo hili, fursa ambazo Tanzania itazipata kwa kuwa Tanzania tayari ina vyombo anwai vya ukuzaji wa



kiswahili hususan BAKITA ambalo ni Baraza la Kiswahili, TATAKI ni Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili, BAKIZA ni Baraza la Kiswahili la Zanzibar na TAKILUKI, yaani Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania itaongoza katika matumizi ya Kiswahili, lakini faida nyingine ni kwamba Tanzania itaandika na kutafsiri vitabu vingi vya Kiswahili ambavyo vitauzwa kwenye soko la Jumuiya; la tatu, Tanzania itakuwa na nafasi kubwa zaidi ya kufundisha Kiswahili katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki; na nne, kuwepo na Makao Makuu ya Kamisheni nchini mwetu kutaongeza nafasi za ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo muhimu kwa Tanzania kutayarisha mkakati kufaidika na fursa zote zinazotokana na kuanzishwa kwa Kamisheni hii, naomba nihitimishe maelezo yangu kwa kusema ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa itifaki hii kwa Taifa letu na maendeleo ya lugha ya Kiswahili iwe lugha yetu ya Taifa na rasmi, ninayo heshima kuliomba Bunge lako Tukufu likubali Azimio la Kuridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ruhusa yako, naomba nilisome Azimio mahsusi la Kuridhia Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

**KWA KUWA** Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*The East Africa Community*);

**NA KWA KUWA** dhumuni mojawapo baada ya kuundwa upya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuwa na chombo kitakachosimamia kuongoza maendeleo ya Kiswahili Kikanda na Kimataifa;

**NA KWA KUWA** kati ya mwaka 1930 na 1964 kulikuwa na Kamati ya Lugha ya Afrika ya Mashariki ambayo ilikuwa na lengo la kusanifu na kuendeleza lugha ya Kiswahili katika Afrika ya Mashariki;

**NA KWA KUWA** Kamati hiyo ilipofika mwaka 1964 ilibadilishwa kuwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ambayo Mqkao yake Makuu yalikuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

**NA KWA KUWA** baada ya kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1977, Mabaraza ya Elimu ya lugha ya nchi zote ziliunda Taasisi, hivyo yaliendelea na ushirikiano usio rasmi baina ya nchi zao;

**NA KWA KUWA** nchi zote zilizokuwa mwanachama wa jumuiya ya Afrika ya Mashariki zinafaidika kielimu, kisayansi, kiteknolojia, kiutamaduni na kimaielewano katika lugha ya Kiswahili;

**NA KWA KUWA** katika Mkataba wa kuanzisha Afrika ya Mashariki vifungu vya 119 (2)(d) na 37 vinaeleza kuwa Kiswahili kitakuwa ni lugha muhimu ya mawasiliano mapana ya Jumuiya;

**NA KWA KUWA** kwa kutambua umuhimu wa msingi wa ushirikiano katika lugha ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambayo Makao Makuu yatakuwa Tanzania;

**HIVYO BASI**, Bunge hili katika Mkutano wake wa Tisa na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaazimia kuanzisha Itifaki ya kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa, sasa ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Ninakushukuru Mheshimiwa. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Azimio hili.

**MHESHIMIWA DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA (K.n.y. MHE. MARGARET S. SITTA - MWENYEKITI WA KAMATI ZA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasoma ushauri wa Kamati kwa niaba kwa ya Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, kama ilivyoainishwa na Kanuni 114 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kamati yangu imepata nafasi ya kutoa maoni ya Kamati kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tisa wa Bunge la Kumi, natumia nafasi hii kukutakia wewe Mheshimiwa Mwenyekitui, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wote, Katibu wa Bunge na Watumishi wote kila Kheri katika kutekeleza majukumu ya ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipata muda wa kutosha kutafakari na kujadili Hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Tarehe 18 Oktoba, 2012, Kamati ilikutana na Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - Mheshimiwa Amos Gabrieli Makalla ili kupata maelezo na ufanunuzi kuhusu uanzishwaji wa Kamisheni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kwamba ushirikiano miongoni mwa nchi waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Tanzania, Kenya na Uganda) wa kukuza na kustawisha lugha ya Kiswahili, ulianza tangu zama za Ukoloni mwaka 1930. Kutokana na kuanzishwa upya kwa

Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1999, ari ya kuimarisha ushirikiano huo katika kukuza na kustawisha lugha ya Kiswahili iliongezeka, na kubainishwa katika ibara ya 137 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; kwa kueleza kwamba Kiswahili kitakuwa lugha ya mawasiliano mapana ya Jumuiya. Ili kutekeleza azma hiyo, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 13 Septemba, 2008, nchi waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilisaini Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ambayo inahusisha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo ni Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda na Burundi pamoja na nchi nyingine zitakazojiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kuanzishwa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ni kuongoza ukuaji na maendeleo ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa ajili ya umoja wa kikanda, pamoja na maendeleo endelevu kiuchumi na kijamii, kikanda na kimataifa. Aidha, Kamisheni hii itatoa ushauri kwa nchi wanachama kuhusu masuala ya Utafiti, ufundishaji, kujifunza na ushauri wa istilahi. Ushauri kuhusu maendeleo ya Kiswahili yanayohusu utayarishaji wa sera, kutoa elimu na kuhuisha mitaala pia utatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo aliendelea kuieleza Kamati kwamba, Tanzania imeteuliwa kuwa Makao Makuu

ya Kamisheni hii. Aidha, Serikali imetoa kilichokuwa Kituo cha Utafiti wa Simulizi Asilia na lugha za Taifa cha Mashariki mwa Afrika kilichopo Zanzibar kuwa Makao Makuu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo Bunge litaridhia Azimio hili, nchi yetu itapata manufaa yafuatayo:-

- (i) Kuwa na nafasi kubwa zaidi ya kufundisha, kutafsiri na uandishi katika lugha ya Kiswahili ndani na nje ya mipaka ya nchi ikiwemo nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Afrika na duniani kote. Uzoefu unaonesha kwamba nchi nyingine zimekuwa mstari wa mbele kufundisha, kutafsiri na uandishi kwa lugha ya Kiswahili ingawa lugha hiyo siyo rasmi katika nchi hizo;
- (ii) Kueneza utamaduni wa Mtanzania kwa kutumia Ofisi za Balozi zake duniani. Lugha ya Kiswahili itaeneza mila na desturi za Tanzania ikiwemo mavazi, sanaa, tamthilia, chakula, na maliasili, ulimwenguni na hivyo kuvutia utalii na uwekezaji;
- (iii) Tanzania kuwa Makao Makuu ya Kamisheni kutaongeza nafasi za ajira kwa Watanzania. Heshima ya nchi kuwa mwenyeji wa Kamisheni inaambatana na kuajiri idadi kubwa ya wazawa, hivyo Tanzania itaifaidika na nafasi za ajira;

- (iv) Kuongezeka kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili katika nchi Wanachama wa Jumuiya, kutaongeza mauzo ya vitabu, majarida, filamu, tamthilia zinazotumia lugha ya Kiswahili, ambapo Tanzania huongoza; na
- (v) Kuwa katika nafasi nzuri ya kukuza na kuimarisha hadhi ya lugha ya Kiswahili kwani Kamisheni itasimamia utolewaji, uenezwaji na uhifadhi wa Kiswahili Sanifu kwa njia ya makubaliano na matumizi fasaha ya lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilikutana na wadau mbalimbali wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kujadili kuhusu Azimio hili la Bunge. Wadau hao ni pamoja na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TATAKI), Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), Chama cha Wanafunzi wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu Afrika Mashariki (CHAWAKAMA), watayarishaji wa vipindi vya redio na luringa kwa lugha ya Kiswahili na mhifadhi wa Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote waliofika mbele ya Kamati wakati wa kujadili itifaki hii. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Mohamed Seif Khatibu (Mb), kwa ushirikiano wake katika kujadili Kamisheni hii. Michango waliyoitoa Wadau itasaidia kuboresha utendaji wa Kamisheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Kamati ilitoa hoja zifuatazo

zilizohitaji ufafanuzi zaidi ikiwemo umuhimu wa urekebishwaji wa Vifungu vya itifaki vinavyohusu:-

- (i) Muundo wa Wajumbe wa Kamisheni kujumuisha makundi muhimu ya wadau wa lugha ya Kiswahili; ambao hawakushiriki katika Uandaaji wa itifaki;
- (ii) Utekelezaji wa Itifaki ya Kamisheni kwa kuzingatia suala la Muungano (Bara na Zanzibar);
- (iii) Ushiriki wa Wizara zinazosimamia utoaji wa elimu nchini (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Tanzania Bara na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali – Zanzibar);
- (iv) Upatikanaji wa fursa mbalimbali za kufundisha na kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili ndani na nje ya mipaka ya nchi kwa Watanzania; na
- (vi) Masuala ya kisera kuhusiana na somo la Kiswahili kufundishwa katika Shule za Serikali na binafsi nchini;

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 22 Oktoba, 2012, Kamati ilikutana Dar es Salaam na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo akisaidiwa na Wataalamu wa Serikali kupata mrejesho wa hoja za Wajumbe, ambapo pamoja na mambo mengine, Naibu Waziri alieleza kwamba itifaki ina nafasi ya kufanyiwa maboresho hata baada ya Bunge Kuridhia Uanzishwaji wa Kamisheni hii.



Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kufanya maandalizi ya awali ya Mkataba, na kwa kuzishirikisha kikamilifu Taasisi mbalimbali katika kujadili Mkataba husika. Ni matarajio ya Kamati kwamba utekelezaji wa Mkataba utakuwa na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kuridhika na ufafanuzi uliotolewa wa hoja zote muhimu kuhusu utekelezwaji wa Kamisheni, Kamati inakubaliana na hatua ya Serikali ya kuingia Mkataba wa Uanzishaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ambazo faida zake zimebainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki umechelewa, kwa ujumla ni mzuri, kwani una manufaa makubwa kwa Tanzania ambayo ni mwenyeji wa Kamisheni hiyo. Hivyo, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yake kama ifuatavyo:-

- (i) Serikali iandae mikakati mahsusi ya kuwezesha wananchi kuipenda, kuieneza, kuikuza na kuhifadhi lugha ya Kiswahili nchini ili kuwawezesha Watanzania kutumia Kiswahili fasaha;
- (ii) Fursa zilizopo za kufundisha na kutafsiri lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania zitangazwe ili kila mwenye sifa ya kufundisha lugha hiyo atumie fursa hizo;
- (iii) Serikali iandae Sera ya kuendeleza lugha ya Kiswahili ili kutoa mwongozo wa kukuza, kueneza, na kuhifadhi lugha ya Kiswahili nchini;

- (iv) Serikali iwezeshe kifedha na kiutaalamu Taasisi mbalimbali za lugha ya Kiswahili katika kutekeleza majukumu yao ikiwemo kuandika vitabu, machapisho, majarida mbalimbali, na kazi za sanaa kwa lugha ya Kiswahili ili kueneza utamaduni wetu.
- (v) Serikali iandae wataalamu wa kutosha kufanya tafiti mbalimbali zenye lengo la kueneza na kukuza lugha ya Kiswahili katika Mabara ya Afrika, Asia, Ulaya na Marekani.
- (vi) Lugha ya Kiswahili itumike katika makongamano, mikutano, warsha mbalimbali zinazofanyika nchini. Aidha, ikiwa italazimika kutumia lugha nyingine, huduma ya tafsiri ya Kiswahili itumike;
- (vii) Serikali ianzishe programu maalumu ya muda mfupi ya kutoa mafunzo ya ufundishaji na utafsiri wa lugha ya Kiswahili ili kuwezesha upatikanaji wa wataalamu wa kufundisha na kutafsiri katika lugha ya Kiswahili. Aidha, mafunzo hayo yaambatane na Cheti cha Uhitimu wa Mafunzo ili kuwezesha wahitimu kuuza utaalamu huo ndani na nje ya nchi. Hali kadhalika, lugha za kigeni ikiwemo Kifaransa, Kiarabu, Kijerumani zifundishwe kusaidia mhitimu wa Ualimu wa Lugha ya Kiswahili, kupata elimu ya msingi ya lugha za kigeni kufundisha watumiaji wa lugha hizo, Lugha ya Kiswahili;

- (viii) Katika kukuza na kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili, ni vyema Serikali ielekeze Taasisi zote za utoaji wa elimu nchini ikiwemo za binafsi kufundisha Somo la lugha ya Kiswahili kama sharti la Msingi, ili kuhifadhi matumizi ya lugha kwa umoja na mshikamono wa Watanzania;
- (ix) Serikali iwatambue na kuwashirikisha wadau wengine wa lugha ya Kiswahili katika utekelezaji wa Kamisheni ya Kiswahili;
- (x) Utekelezaji wa Mkataba wa Kamisheni hii ni mtambuka. Serikali ihakikishe kwamba Wizara zote zinazohusika na utekelezaji wa Mkataba huu (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Awali - Zanzibar, Wizara ya Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika Ofisi za Balozi, na nyinginezo) zihusike kikamilifu katika utendaji wa Kamisheni ya Kiswahili;
- (xi) Serikali ifikirie uwezekano wa kuwa na shule angalau moja ya mfano itakayotoa Elimu ya Awali mpaka Chuo Kikuu kwa lugha ya Kiswahili, sambamba na kufundisha lugha nyingine ikiwemo Kiingereza kama somo. Hatua hii ni muhimu, kwani wanafunzi wataweza kuelewa masomo wanayofundishwa, kutumia lugha ya Kiswahili fasaha sambamba na kutumia lugha za kigeni ikiwemo Kiingereza kwa ufasaha; na

- (xii) Bunge la Jamhuri ya Muungano liwe la mfano kwa kutekeleza shughuli zake zote kwa lugha ya Kiswahili ikiwemo kuwasilisha Miswaada na Mikataba iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nakushukuru kwa kuipa heshima Kamati yangu kujadili na hatimaye kuwasilisha maoni na ushauri kuhusu Uanzishaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki; hoja ambayo ni muhimu kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili nchini, Afrika Mashariki, Afrika na Ulimwenguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru kwa dhati Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara na Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Katibu Mkuu - Balozi Sethi Kamuhanda na wataalamu wote wa Wizara kwa ufafanuzi wa kina wa hoja za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa umakini mkubwa na ushirikiano waliutoa katika kufanikisha kazi hii. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta - Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile - Makamu Mwenyekiti, na Wajumbe ni Mheshimiwa Dkt. Maua A. Daftari, Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Pauline P.

Gekul, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Lameck O. Airo, Mheshimiwa Antony G. Mbassa, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mheshimiwa Ali J. Haji, Mheshimiwa Annamerystella J. Mallack, Mheshimiwa Martha J. Mlata, Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa Highness S. Kiwia, Mheshimiwa Mch. Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Clara D. Mwatuka, Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla, Mheshimiwa Nyambari C. Nyangwine, Mheshimiwa Rashidi A. Omari, Mheshimiwa Said Suleiman Said, Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mheshimiwa Saidi R. Bwanamdogo, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Shaffin A. Sumar na Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas D. Kashilillah, Katibu wa Kamati hii - Ndugu Stella Mlambo na Ndugu Happiness Ndalu kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kwa namna ya kipekee kabisa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Nzega kwa kuendelea kuniunga mkono katika jitihada mbalimbali ninazozifanya kuijenga Nzega mpya ikiwa ni pamoja na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Wananchi wa Jimbo letu la Nzega msiyumbe wala msibabaishwe, Mbunge wenu niko imara kusimamia kweli na kupambana na maharamia. Niwahakikishie jambo moja kuwa, siku zote kweli itaendelea kushinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii inaunga mkono Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, na kwa heshima na taadhima kubwa naomba kuwasilisha.  
*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Naomba sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mbilinyi tafadhali.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kutoa hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Azimio la Itifaki ya uanzishwaji wa Tume ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na afya njema anayoendelea kunijalia mimi pamoja na familia yangu hadi wakati huu. Aidha, namshukuru Mungu kwa kunilinda na kuniepusha na hatari za kiroho na kimwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu za pili zimwendee Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kuendelea kuniamini na hivyo kunipa dhamana ya kuendelea

kutumikia nafasi hii kama Waziri Kivuli wa Habari, Vijana Utamaduni na Michezo. Aidha, nampongeza yeye pamoja na Katibu Mkuu wa CHADEMA Mheshimiwa Dkt. Willbroad Slaa na timu nzima ya Makamanda wa CHADEMA kwa kazi nzuri na iliyotukuka wanayoendelea kuifanya nchi nzima ya kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu siasa za nchi yao kupitia operesheni za vuguvugu la mabadiliko za *Movement for Change* (M4C).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza Wabunge wenzangu wa CHADEMA kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kukijenga Chama Majimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini kwa umuhimu mkubwa, napenda kuishukuru familia yangu hasa mzazi mwenzangu Faiza na mwanangu Sasha-Desderia J. Mbilinyi kwa kunivumilia hasa ninapokosekana nyumbani kwa muda mrefu nikiwa katika shughuli mbalimbali za kuwatumikia wananchi ikiwemo ziara za (M4C).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili katika historia ya Tanzania ni lugha ya Ukombozi. Hii ni kwa sababu Kiswahili ndiyo lugha pekee iliyoweza kuyaunganisha makabila yote Tanzania na kujenga umoja katika kupambana na udhalimu wa Wakoloni na hatimaye kuweza kupata uhuru kama Taifa moja lenye umoja na uelewano miongoni mwa watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo jema kukumbuka na kuheshimu kwa dhati kabisa kwamba, misingi ya Taifa letu kwa kiasi kikubwa imetokana na Lugha ya Kiswahili. Uhuru na Umoja wetu ni tunu na hazina kubwa kwa Taifa

letu. Tunu hizi zimejengwa na lugha moja ya Kiswahili iliyotuunganisha sote pamoja tukiwa na lengo moja la kudai uhuru kwa wakati ule, na sasa katika harakati za kuleta maendeleo ya Taifa letu. Ndio maana nembo yetu ya Taifa inaendelea kuenzi misingi na tunu za Taifa hili za “Uhuru na Umoja”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lolote duniani, lina kitu mahsusi na cha pekee kinacholitambulisha Taifa hilo mbele ya Mataifa mengine. Kitu hicho huitwa utamaduni wa Taifa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya Kiswahili kama utambulisho wa Taifa la Tanzania licha ya kwamba Tanzania ina mambo kadha wa kadha yanayoweza kuitwa ni utamaduni, lakini utamaduni pekee wenye nguvu uliobaki katika Tanzania na ambao unaweza kuitofautisha Tanzania na mataifa mengine duniani ni lugha ya Kiswahili. Hivyo, wazo na azma ya kuanzisha Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ni heshima kubwa sana kwa Tanzania, kwani utamaduni wake wa lugha ya Kiswahili umeonekana na Mataifa mengine kuwa ni mzuri na wa kistaarabu na kwamba unafaa kuenezwa na kuenziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika Utengamano wa Afrika Mashariki, miongoni mwa sababu za kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ni pamoja na nchi wanachama kuwa na historia na tamaduni zinazoshabihiana. Hata hivyo, ni dhahiri pia kwamba miongoni mwa sababu hizo, lugha ya Kiswahili imekuwa ni chachu kubwa zaidi. Hii ni kwa sababu inazungumzwa na asilimia kubwa ya wananchi wa nchi



wanachama na hivyo kuwaunganisha watu haraka zaidi kuliko vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka, Kiswahili kikiwa lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Watanzania watakuwa na fursa kubwa ya kuendesha shughuli zao za kiuchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki bila kikwazo cha lugha. Kwa mantiki hiyo, fursa ya kukuza uchumi wetu itakuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fursa nzuri ambazo Watanzania wataweza kunufaika nazo kwa kuanzishwa kwa Tume hii ya Kiswahili, bado kuna changamoto ambazo Tanzania kama Taifa, ni lazima izifanyie kazi ili kupanua wigo wa kunufaika na Itifaki hii. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Tanzania kushindwa kutumia nafasi yake ya “Kinara” wa Lugha ya Kiswahili barani Afrika katika kusaka fursa mbalimbali katika soko la ajira. Uzoefu unaonesha kwamba asilimia kubwa ya Walimu na Wahadhiri wa Kiswahili katika Shule na Vyuo Vikuu vya nje wanatoka Kenya. Hivyo, Tanzania ina kazi kubwa sana ya kufanya juhudi katika kusaka fursa hizo ili kuonesha mfano ikizingatiwa kwamba Tanzania ndiyo kinara wa lugha ya Kiswahili duniani.

(ii) Kwa kuwa kuna ngazi nne za matumizi ya lugha ya Kiswahili, yaani ngazi ya kitaifa, ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ngazi ya Afrika na ngazi ya dunia; na kwa kuwa

kuna vituo vingi vya utangazaji duniani vinavyotumia idhaa ya Kiswahili; na kwa kuwa Kiswahili kinafundishwa katika Shule na Vyuo vingi duniani; na kwa kuwa idadi ya wazungumzaji wa Kiswahili ni kubwa na inazidi kuongezeka, basi Kamisheni hii itatakiwa kukabiliana na changamoto ya kuratibu matumizi ya Kiswahili katika ngazi zote nne ili kukipandisha hadhi na kuweza kuwa miongoni mwa lugha mashuhuri za Kimataifa.

(iii) Kiasi cha Shilingi milioni kumi kilichotengwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu Tume hii ya Kiswahili na kazi zake, ni kidogo sana ukizingatia umuhimu wa suala lenyewe. Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza kwa kina namna elimu kwa umma itakavyotolewa na majukumu ya nchi wanachama ni nini katika kutoa elimu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua umuhimu na mchango wa lugha ya Kiswahili katika kujenga udugu, umoja mshikamano wa Kitaifa na utangamano wa Afrika Mashariki na Afrika, na kwa kuwa kwa kuanzishwa kwa Tume hii ya Kiswahili ambayo Makao yake Makuu yatakuwa Tanzania, kutatoa fursa mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa Watanzania katika ukanda wa Afrika Mashariki; Kambi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono pendekezo la Itifaki ya Uanzishaji wa Tume ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kwa uwasilishaji wako mzuri. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye majadiliano na ninamwita Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale na Mheshimiwa Leticia Nyerere ajiandae na Mheshimiwa Ezekiel Wenje pia ajiandae. Mheshimiwa Mchungaji, tafadhali!

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kusema machache kuhusu Kamisheni ya Kiswahili au Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili. Kwa ujumla, uanzishwaji wa Kamisheni hii umechelewa sana kwasababu umesababisha fursa nyingi ambazo tungekuwanazo hapa Tanzania kuzikosa, lakini niwashukuru au nimshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu na Watumishi ambao kwa kweli walijitahidi kuweza kuleta hili Azimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili ni zuri na pamoja na kuwa limechelewa, lakini limefika pia kwa wakati muafaka ambapo sisi kama Wabunge ni vizuri tuweze kuridhia ili Kiswahili kiweze kuenea kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninawashukuru pia watu ambao wanasambaza Kiswahili pamoja na kwamba siyo katika ufasaha, lakini wanajitahidi sana kuhakikisha kuwa

Kiswahili kinazungumzwa karibu nchi nyingi na hasa wafanyabiashara ambao wamekuwa wakizunguka hapa na pale, maana ukienda Zambia, Malawi, Msumbiji, na hata nchi nyingi sana ambazo zinatuzunguka, unaona jinsi ambavyo Kiswahili kwa kweli kimekuwa muhimu sana. Kinazungumzwa na watu wengi sana, na hii ni kwa sababu ya mwingiliano wa kibiashara. Lakini nafikiri Serikali itaangalia ni namna gani inaweza kuwawezesha hao wafanyabiashara ambao wanazunguka hapa na pale kwa ajili ya kuwapatia semina ili lugha hii iweze kwenda kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kwamba tu iweze kuridhiwa na nchi hizi za Afrika Mashariki, lakini pia tufahamu kwamba nchi nyingi ambazo zinatuzunguka, wanapenda sana kuzungumza Kiswahili na itakuwa ni vizuri kama tutakuwa tunaweza tukafungua vituo vya kufundisha Kiswahili huku. Hiyo itakuwa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengine ambacho ningeweza kusema, wenzetu wa Kenya tumeona jinsi ambavyo wanajitahidi sana kueneza Kiswahili kwa kuwa na Walimu kila mahali na kila nchi, ukienda Ulaya unakuta Kenya wanafundisha Kiswahili, ukienda Marekani Wakenya wanafundisha Kiswahili. Nilikuwa pale Israel mpaka wakawa wameanzisha Ibada ya Kiswahili pale. Watu ambao wanaweza kuzungumza Kiswahili wakawa wanaalikwa kwenda pale kuhudhuria ibada. Hata Uingereza ni hivyo hivyo!

Hii ina maana kwamba kwa kweli Kiswahili sisi tumekuwa nyuma, tumeshindwa kutumia fursa vizuri,

tumewaachia wenzetu majirani zetu kwenda kutumia Kiswahili na kujipatia manufaa, sisi tunanyamaza kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kwamba Serikali katika kuridhia hili suala au katika kuanzisha hii Kamisheni, Serikali yetu iwe ya kwanza, iwe makini kuhakikisha kwamba kwa kweli inajitahidi kuomba nafasi mbalimbali ambazo vijana wetu tunaweza tukawatuma huko kwenda kufundisha. Tunaweza tukawapeleka Zambia, Malawi, Msumbiji, Congo na kila mahali ambako kinazungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wanazungumza Kiswahili, lakini siyo kwa upana mkubwa, Uganda bado walikuwa na matatizo kidogo ya kuzungumza Kiswahili, labda kwa kuridhia itifaki hii sasa itawasaidia kuhakikisha kwamba Kiswahili kinakwenda vizuri, lakini mwanzoni walikuwa wanafikiri Kiswahili, kulikuwa na mambo fulani ambayo yalijitokeza katika vita vya Uganda, kwa hiyo, wakafikiri kwamba hawa waliokuwa wanazungumza Kiswahili ndiyo walikuwa wanawaua na hawakufanya mambo mazuri kwao. Kwa hiyo, Uganda kidogo Kiswahili kilikuwa kinasuasua, lakini kwa Azimio hili na Itifaki hii ya kuanzisha Kamishna hii, bila shaka itakifanya Kiswahili kikue kwa haraka zaidi katika nchi zetu za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itumie fursa hii vizuri, tuna vijana wetu wengi ambao wamesoma, wangeweza kupata nafasi hizo, siyo hapa tu, lakini wangeweza kwenda hata Ulaya kama tutakuwa tayari kufungua vituo ambavyo vitakuwa vinafundisha Kiswahili. Nilikutana na kijana mmoja kutoka Japan Mbeya pale

anasema yeye kazi yake kubwa kule ni kufundisha Kiswahili na anajipatia hela. Wajapani wengi wanapenda kujifunza Kiswahili. Kwa hiyo, fursa kama hizo zingeweza kutumika katika nchi nyingine, Mabalazi wetu waliopo huko basi watusaidie kuhakikisha kwamba vituo kama hivi vinapatikana ili vijana wetu waliosoma waweze kupelekwa huko na kuweza kujipatia ajira kwa namna yake.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake, mimi naunga mkono kabisa itifaki hii ya kuanzishwa Kamisheni hii kwa sababu ni muhimu hasa kama Taifa kwa sababu lugha hii sisi tuna-*own* ni lugha yetu. Hili suala liwe ni *urgent* na liwe ni *important*, lisiwe ni suala ambalo tunamalizia kwenye makaratasi, lakini baada ya hapo tunalala tena. Nilikuwa naomba tuhakikishe kwamba Kiswahili kinakuzwa kwa haraka zaidi, na sisi tunachukua fursa hii ya kwanza kabisa, kwa sababu Kiswahili ndiyo lugha ambayo sisi Watanzania tumeitumia enzi na enzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi wake na kwa ujumla wake, nasimama tu kuunga mkono hoja hii kwamba naomba Wabunge wote turidhie, tukubali hili Azimio liweze kutekelezwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale. Sasa namwita Mheshimiwa Leticia Nyerere na Mheshimiwa Ezekiel Wenje ajiandae na Mheshimiwa Gorge Mkuchika ajiandaye.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika suala la Itifaki ya Uanzishwaji wa Tume ya Kiswahili Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kujivunia hasa kwetu sisi Watanzania ukizingatia kwamba tutapata faida nyingi sana kutokana na Tume itakayotokana na Itifaki hii. Faida ya kwanza itakuwa ni kuweza kutumia lugha ya Kiswahili kuendeleza elimu yetu na vile vile kutumia lugha ya Kiswahili katika kufanya utaifi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine ambayo tutaipata kama Watanzania ni kuweza kujiendeleza zaidi kibiashara, ukizingatia kuna baadhi ya watu wanakwama kufanya biashara kwa ufanisi kwa sababu ya vikwazo vya lugha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumepata fursa, lakini kupata fursa ni jambo moja na kuitumia fursa ni jambo lingine. Watanzania tumejiandaa vipi kunufaika na hii fursa ambayo tunayo sasa ukizingatia na Makao Makuu ya Tume yatakuwa Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme wazi kwamba Watanzania tuna changamoto nyingi sana. Tatizo siyo kukosa Maprofesa wanaojua Kiswahili, tatizo ni kushindwa kutumia vizuri uwezo wetu wa kielimu kwa kushindwa kuonisha elimu na nidhamu husika katika utendaji wa kazi yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuzingatie uwajibikaji, pamoja na kwamba tumepata fursa kama Watanzania, ukizingatia kwamba wengi wetu wanaelewa na kukijua Kiswahili vizuri, lakini uwajibikaji ukoje? Ni lazima tulifanyie kazi hilo. Vinginevyo hii fursa haiwezi kutunufaisha Watanzania na badala yake itawanufaisha wenzetu wa Kenya na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima pia tujifunze kujali kazi. Watanzania walio wengi wanapopata kazi hawazithamini, wanafikiri kupata kazi ni jambo la mzaha. Ni lazima tuwaandae Watanzania kwamba anapoipata kazi iwe ya kufundisha Kiswahili, iwe ya kutangaza kwenye idhaa ya Kiswahili. Ni lazima aiheshimu ile kazi, ni lazima atambue kwamba maisha yake yanaitegemea hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wa Tanzania au Serikali kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu hili, kwani tumekuwa tukizingatia ujuzi ambao ni wa kielimu na tunakwepa ku-*address* suala ambalo ni gumu sana kwa Watanzania walio wengi nidhamu kwenye kazi. Bila ya kuwa na nidhamu ya kazi, haijalishi uwe umesoma shahada ngapi; hata ukienda kwenye ushindani wa kimataifa kikazi, huwezi ukachukuliwa.

Vile vile mbali ya nidhamu, kuna ule mwonekano unapokwenda kutafuta kazi iwe ya kufundisha, iwe ya kutangaza kwa Kiswahili, kama wewe mwonekano wako upo upo tu, hakika huwezi kupata kazi! Hapo sasa tunaanza kushangaa, mimi nina Ph.D kwenye Kiswahili, lakini kwanini wameniacha wakamchukua Mkenya? Mimi sijui,



nimebobebea kufundisha Tanzania zaidi ya miaka 20, kwanini wameniacha wakamchukua Mganda?

Mwonekano ni jambo la kuzingatia! Hakuna mtu anaajiri mtu ambaye ana uwezo tu wa kufanya kazi lakini mwonekano wake hauna mvuto. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacheka lakini hili ni jambo muhimu sana, ni jambo la msingi kuzingatia. Tumekuwa tukikwepa hapa kwa muda mrefu, lakini naiomba Serikali tusaidiane wote kwa pamoja kuwabadilisha Watanzania wawe na mwonekano wa kuajiriwa. Jambo la kulalamika sasa tuliache pembeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tumekuwa na mazoea ya kulalamika tunapoachwa kwenye kazi. Tunakwenda kwenye *interview*, unasema nimeachwa wakati nina-*qualify*, nimeachwa wakati sijui nina *masters degree* kwenye Kiswahili, lakini umejiangalia asubuhi kwenye kioo kabla hujatoka nyumbani kwako, mwonekano wako ukoje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la kuzingatia, tutanufaika na Tume hii kwa kiwango kikubwa kabisa endapo tutakubali kujisahihisha kama Watanzania ili tuweze kutumia elimu zetu katika hizi nyanja za lugha ya Kiswahili pamoja na mahitaji mengine yanayotakiwa kwenye kazi ikiwemo mwonekano wa mfanyakazi mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nitoe rai kwa Serikali na Wizara husika, tunahitaji kuwaelimisha Watanzania kuwapa elimu dunia, kuacha ile ya darasani ambayo inaitwa *academic knowledge*,

haitoshi. Vinginevyo, tutapata fursa kama hii ya kuletewa Tume nchini kwetu, lakini sisi wenyewe Watanzania hatuwezi kunufaika na hii fursa.

Kwa hiyo, katika utaratibu wa maandalizi, ningeomba sana Serikali ishiriki kikamilifu kuwaelimisha Watanzania katika hili ukizingatia kwamba ni moja ya mahitaji katika upatikanaji wa ajira hasa zile za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nisipoteze muda, naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia kwenye hili Azimio la Kupitisha Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema kwamba kwenye hii taarifa aliyowasilisha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa pili, Waziri amesema kwamba Baraza la Mawaziri walipokutana Burundi, lilipitisha kwamba Makao Makuu ya Tume yatakuwa Tanzania. Sasa ukisoma hiki kitabu walicholeta ukurasa wa 11 Ibara ya 14 sehemu ya pili inasema hivi kwa Kiingereza: „*The Headquarters of the Commission shall be determined by the Council.*„ Tafsiri yake ni kwamba Makao Makuu ya Tume hii yataamuliwa na Tume hiyo baada ya kwamba sasa imetengenezwa ndiyo wataamua kwamba Makao Makuu hasa ya Tume hiyo yanakwenda kuwekwa nchi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Mheshimiwa Waziri anasema wao wameshapitisha wakati leo ameleta Azimio kwamba sisi tupitisha ili Tume hii itengenezwe, na Sheria hii

waliyoitengeneza inasema kwamba Makao Makuu ya Tume yataamuliwa na hiyo Tume baada ya kuwa-*composed*; sasa wao hayo mamlaka wametoa wapi? Kama wameanza kuvuruga hata haijaanza kutekelezwa, sasa itakuwaje? Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ukiangalia bajeti ambayo Wizara imeandaa *East African Community* kama Jumuiya, Tanzania ndiyo nchi ya mwisho kwa wananchi wake kujuzwa au kujulishwa kwenye uelewa wa elimu ya jinsi gani Jumuiya inavyokwenda. Sasa leo kama Wizara wanasema wao wameandaa Shilingi milioni kumi tu ya kwenda kuelimisha Watanzania kuhusu hii Tume, hii Shilingi milioni kumi wanakwenda kuifanyia nini? Au ndiyo wanakwenda kwenye yale mambo tuliyoletewa hapa ya Afrika Mashariki kwamba wanalipia magari ya matangazo? Huwezi ukatangaza vitu *serious* kama hivi kwa kutumia magari ya matangazo, kumbe unatangaza Disko. Sasa kama kwa hii Shilingi milioni kumi, hii pesa haitoshi, na Wizara iangalie ni mfumo upi utakwenda kutumika wenye tija wa kueleweshwa Watanzania wengi kuhusu kazi na kwanini hii Tume leo tunapitisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, nilikuwa nahitaji tujiulize kwamba mpaka sasa kwa muda mrefu Tanzania ndiyo inaonekana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba ndiyo nchi ambayo Kiswahili kinatumika sana. Lakini tumefanikiwa kiasi gani? Kwa sababu leo ukienda hata Rwanda utakuta walimu wengi wanaofundisha Kiswahili, asilimia kubwa wengine wametoka Kenya. Sasa leo tunaunda hii Tume, lakini hatujui kama nchi tumefanikiwa kiasi gani. Kwa hiyo, sisi ndiyo tunaonekana

kwamba ndiyo nchi mama wenye Kiswahili. Lakini tumefanikiwa kiasi gani? Kwa maana kama ni watu wetu kupata ajira katika hizi nchi nyingine, Kiswahili hakitumiki sana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo hii natoa tu kama changamoto kwamba tuchukue tathmini kwamba mafanikio yetu ambayo tunapata mpaka leo, huko nyuma tumefanikiwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho napenda nisisitize ni kwamba sisi kama Taifa tathmini yangu ninayotoa ni kwamba sisi wenyewe tumeshindwa kuendeleza Kiswahili. Nasema hivi kwa sababu ukiangalia nchi hii, sheria inasema kwamba lugha ya kufundishia kwenye Shule za Kiswahili, kwa mfano, kwenye Shule za *Primary* itakuwa ni lugha ya Kiswahili. Lakini leo sisi ndiyo tumejaza *English Medium* hizi zinazofundisha kwa lugha ya *kiingereza* nchi hii.

Watoto wa viongozi wote nilisema hata katika Bunge kipindi kile mpaka na wa kwangu wote wanasoma kwenye hizo *English Medium*. Sasa hiki Kiswahili tunaki-*promote* vipi? Yaani tunakiendelezaje hiki Kiswahili? Hapa Bungeni tunapiga kelele kweli Kiswahili lugha yetu, lugha yenu mbona watoto wenu hawasomi kwenye hizo shule za Kiswahili? Ninyi mnataka kutumia tu watoto wa watu maskini ku-*promote* Kiswahili, haiwezekani! Hii siyo haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kweli Wizara na kama kweli Serikali mpo *serious* kwamba mnataka ku-*promote* Kiswahili, turudi kwenye sheria, kwamba sheria kwa mfano lugha ya kufundishia kutoka kwenye shule zetu za

*primary*, kwa sababu unapompa mtoto msingi wa lugha, hapo ndiyo tutakuwa tunakuza Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kwamba, nimesoma *objectives* za Tume kwenye *article seven* katika hiki kijitabu walicholeta. Moja, hii *Commission* wamesema kwa kiingereza kwamba *is going to develop Kiswahili as a region language, expressing and conveying positive African values with the respect to issues of gender, equity, human rights and democracy.*

Sasa ukiangalia kwa kazi kama hii ambayo Tume inaweza kufanya ya ku-*develop Kiswahili as a regional language*, haiwezekani leo uka-*develop Kiswahili as a regional language* kwa mantiki hii wakati Kenya wanafundisha kutokea chekechea mpaka Chuo Kikuu kwa kutumia Kiingereza. Ukienda Rwanda wanafundisha kwa kutumia Kifaransa, ukienda nchi nyingine kama Uganda wanatumia Kiingereza. Mimi napendekeza kwamba katika hiyo *article seven* ukienda (g) inasema hii Tume itakuwa inafanya kitu kingine kinaitwa *quality assurance*.

Sasa *quality assurance and curriculum standardization*, natoa changamoto kwamba kama inawezekana, kama kweli tunataka kupeleka Kiswahili kama *regional language*, basi hii Tume kutoka kwetu Tanzania tusukume ikiwezekana shule zote *East Africa* katika ngazi ya msingi, basi wafundishe kwa kutumia Kiswahili. *This is the only way* tunayoweza kutumia kupeleka Kiswahili iwe katika hiyo *level* ya msingi na ienee katika kila nchi kama kweli hiyo ndiyo dhamira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Azimio hili zuri sana. Lakini kwa sababu mwaka huu mwaka wa Uchaguzi kwa chama changu cha Mapinduzi, nianze kuwapongeza wanachama wenzangu hasa Wabunge mlioshinda kwa kishindo katika maeneo yenu. Nawashukuru wapigakura wangu kule Newala kwa kunipa tena *NEC* kwa kishindo, lakini pia kwa wale vijana wangu wa Jangwani wa Yanga kuwapongeza mambo yanavyokwenda vizuri, walileta Kombe la *Challenge* humu ndani. Maagizo ya mimi mdhamini wao wa klabu ni kwamba safari ijayo walete klabu bingwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimesimama hapa kuunga mkono hoja, kuridhia suala la muda mrefu sana ambalo Serikali hii ya awamu ya Nne tangu tumeanza, alianza Mheshimiwa Waziri Mohamed Seif Khatib, nilifuata mimi akafuata Mheshimiwa Nchimbi na sasa amefanikisha Mheshimiwa Dkt. Fenella. Niwaambieni ndugu zangu kwamba kupata hii kwamba iwe Makao Makuu haikuwa kazi rahisi. Wenzetu walitaka sana hasa Kenya, lakini tulikuwa *aggressive*. Mimi nilipeleka mpaka Zanzibar nikawaonesha ilipokuwa Kituo cha Simulizi ya Lugha na nini, tukawaambia na majengo yapo ndiyo maana hatimaye tumefanikiwa. Kwa hiyo, nataka kuipongeza sana Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo kwa kufanikisha jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wanaofuatilia Kiswahili, ni kama tumerudi katika historia. Huko zamani tulikuwa na *East African Swahili Committee*, tumeambiwa tangu mwaka 1930 wakazi wa akina Hellen White, Wazungu waliona umuhimu wa kuwa na *East African Swahili Committee* kwa maana ya kuwaunganisha watu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania tunaishi kwa umoja na mshikamano moja ya sababu ni kwa sababu tunazungumza lugha moja. Hakuna Rais, Waziri Mkuu au Mbunge au anayekwenda kuhutubia watu wake kwa lugha nyingine akatafuta mkalimani kama inavyokuwa nchi nyingine. Makabila yote Tanzania tunaongea Kiswahili. Jambo hili Mungu ametusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii tunayofikia sasa itazidi kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara anayoongoza Kaka yangu Mheshimiwa Samuel Sitta, tukifanikiwa kuimarisha Kiswahili, nina uhakika hata ule mtengamano wa Afrika Mashariki utakuwa rahisi kwa sababu tutakuwa tunaongea lugha moja na mimi nataka kutoa ushauri hapa kwamba tayari katika Bunge la Afrika, katika *African Union* tunaongea Kiswahili. Hivi ninyi Afrika Mashariki hapa Bunge lenu ni lazima tuendeleo na Kiingereza mpaka leo? Kwanini tuiseme anayetaka kusema Kiingereza haya, anayetaka kusema Kiswahili haya, hatuwezi tukazungumza tunaanzisha *Commission* ya

Kiswahili Afrika Mashariki, lakini Mkutano wenyewe pale katika Bunge tunaongea Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ushauri huo, tulenge sana Kiswahili kutumika Bunge la Afrika Mashariki kama vile ambavyo kinatumika katika Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa Watanzania wenzangu kuhusu Azimio hili, nina ujumbe. Kwanza, naona wenzangu wamesemea ni lazima tujiandae kusambaza Walimu katika Afrika Mashariki. Wizara ya Habari miaka miwili mitatu nyuma kulikuwa na walimu 300 wamejiorodhesha, wako tayari kwenda kufundisha Kiswahili nchi nyingine, lakini wanahitaji kuwezesha wale, *contact* hawana, utaratibu na namna ya kujua: Je, Rwanda wanataka wangapi? Msumbiji wanataka wangapi? Wizara tuwasaidie watu hawa kuwafanyia *marketing*, kuwafanyia utafiti, kujua wapi walimu wanahitajika na tuwaeleze kwamba sisi tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza habari ya Kenya kwamba ina Walimu wengi, pale wamekuwa *aggressive*; wale ni kwamba wanapita kusema sisi ni walimu. Lakini na mimi nataka kusema jambo lingine kuhusu Kenya. Ndugu zangu, tofauti ya Kenya na sisi ni kwamba Mkenya anayejifunza Kiswahili anajifunza *Swahili grammer*, na wanapokwenda kufundisha Kiswahili unafundisha Kiswahili kile kilichozingatia *Swahili grammer*, siyo uzoefu wa kusema Kiswahili. Hata ukienda Uingereza wanasema Kiingereza sanifu ni kile kinachozungumzwa *London Square*. Sasa na sisi Kiswahili sanifu unaweza ukawa unasema Kiswahili kila siku, lakini husemi Kiswahili sanifu, huna hati ya



kwamba wewe unajua *Swahili grammer*. Kwa hiyo, huwezi ukapata ajira katika nchi. Wale wanauliza vyeti.

Kama kuna jambo Wakenya wako mbele, leo wanajifunza *Swahili grammer* ndiyo maana wale wanaojua Kiswahili wanajua sana na wale wasiojua hawajui kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nataka kutilia mkazo hili sana, tuwe makini, tujifunze Kiswahili sanifu. Wenzetu Kenya wanazingatia sana suala la *grammer* ya Kiswahili na wana wanafunzi wengi sana wanaojifunza Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini imezungumzwa habari ya ajira hapa, kwamba moja ya faida ni kwamba watu wetu wanapata ajira sawa. Lakini mwelewe sasa hivi katika vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki tunavyoitwa Arusha pale na Mheshimiwa Samuel Sitta tunazungumza mambo ya utangamano wa Afrika Mashariki, tunazungumza habari ya kazi ikitangazwa iwe ruhusa kuombwa kwa watu wa nchi zote. Katika Kiswahili watakapotangaza kazi watazingatia nani ana cheti cha Kiswahili, mitihani ya Kiswahili na siyo nani kasema vizuri Kiswahili. Ooh, mimi nimezaliwa wapi, najua Kiswahili tangu mgongoni, hapana! Wanataka taaluma ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kutilia mkazo sana kwamba tuwe makini katika kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba na Wabunge wenzangu, sisi hapa ni shule, kila tunalolifanya hapa watu wanatuona na wanatufuatilia. Sisi tujitahidi kusema Kiswahili sanifu humu ndani. Siku moja nilisimama nikapiga kelele

hapa kwamba jamani eeh, katika maneno ya Kiswahili yanayoazimwa kutoka nje, hayana wingi.

Neno baiskeli haina wingi, baiskeli moja, baiskeli mia mbili; neno skauti halina wingi, skauti mmoja, skauti mia mbili; hakuna chama cha maskauti wala hakuna chama cha maskauti wa kike, ni Chama cha Skauti wa Kike, Chama cha Skauti wa Kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini moja tunaliharibu sana na nitalisemea baadaye kwa vyombo vya habari. Neno hili ni masaa. Saa ni moja. Mwendo wetu kutoka Dar es Salaam kwenda Addis Ababa itachukua mwendo wa saa nne, siyo masaa manne. Humu ndani kila siku tunapiga masaa. Tuanze na sisi humu ndani. Watoto wetu wanatusikiliza, tujitahidi kuzungumza Kiswahili sanifu tena ukishasema masaa sasa wanakwenda mbali zaidi, wanasema nimemsubiri lisaa limoja, hakuna lisaa limoja wala hakuna masaa, nimesubiri muda wa saa moja, wananchi wanatusikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho, ndugu zangu Wizara ya Habari tuna kazi ya kufanya. Naomba Wizara ya Habari mtusaidie vyombo vya habari kutumia lugha sanifu katika vyombo vyao. Wanaoandika wengi wanaharibu Kiswahili, hiyo masaa wanatumia, lakini hasa wale watangazaji wa redio, katika Kiingereza, kuna neno wanasema *code switching*. *Code switching* maana yake unahama lugha hii kwenda lugha hii. Huwezi ukamsikiliza Mtangazaji hasa redio hizi ukisikiliza vijana hawezi kuongea mwanzo mpaka mwisho wa sentensi mbili tatu hajapachika maneno ya Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasafiri kwenda Dodoma, unaona! *On my way, I met* Mussa pale tukajadiliana, tukazungumza! Kiingereza wanasema, *code switching*, kwanini kuchanganya? Ukiamua kusema Kiswahili sema Kiswahili; ukiamua kusema Kiingereza una hamu nacho, sema Kiingereza. Nina hakika na hapa ndani na sisi tujitahidi, maana kuna watu hapa wanaongea Kiswahili, akiona anahitaji aeleweke vizuri, lakini apige *code switching*, atie na Kiingereza. Jamani lugha rasmi humu ndani ni Kiswahili. Hivi huwezi kujieleza mwanzo mpaka mwisho? Kama umekwama wapo wataalamu, waulize akina Dkt. Mohammed Seif, ni wataalam wa Kiswahili, akina Mzee Mkuchika *literature*, eeh njooni hapa. Maana kuna wengine mnawaza Kiingereza halafu mnakuja kusema kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri niseme hayo, vyombo vya habari naomba sana, mtoto nyumbani anaambiwa saa mbili kwenda Addis Ababa, lakini angalieni matangazo ya *Vodacom, Tigo*, na kadhalika, wanasema masaa 24. Nami naomba hasa ile redio ya Serikali watu wa *TBC* wakati wa Mzee Karume baada ya kusilikiza taarifa ya habari akaona wakati ule *RTD* inazungumza Kiswahili siyo kizuri, mimi nilikuwa nafanya *temporary* pale *News Room RTD* alituletea Mzee mmoja Marehemu Mohamed juma Jongo. Yule alikuwa ndiye mtalaam wa Kiswahili.

Mkishatafsiri mnampa yeye anasahihisha Kiswahili kile ndiyo inakwenda kwenye taarifa ya habari. *TBC* mtu akija kuripoti pale analeta matangazo ya masaa, hebu

mfanyieni masahihisho kwa sababu kadri mnavyotangaza ninyi watu wa *TBC* masaa 24 watu wa mabenki kwenye *ATM* waliandika huduma masaa 24.

Mimi nikiwa Waziri wa Habari niliwaandikia nikawaambia futeni. Benki zote sasa wameandika saa 24, huduma saa 24, na siyo masaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, iko haja sheria ya Kiswahili iliyoanzisha Baraza la Kiswahili la Taifa BAKITA, ni lazima tutizame BAKITA upya. BAKITA haina meno, BAKITA imekuwa ni ya kutoa ushauri, kazi yao ni kutoa vitabu, maana Waingereza walitoa kitabu kinaitwa *Common Mistakes in English* na wao wametoa kitabu kinaitwa Makosa yanayojirudiarudia katika Kiswahili. Lakini hayafuatwi, wala hayazingatiwi! Kwa hiyo, nasema huko siku zijazo najua baadaye utakuja Muswada, nafikiri wa vyombo vya habari, muangalie na hili Baraza la Kiswahili la Taifa lazima lipewe meno. Leo mtu kama anaharibu lugha, hata kama kila siku anasikika kwenye redio, hakuna mahali BAKITA anaweza akawaita akasema bwana wewe unatuharibia lugha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, BAKITA lazima tuwape meno. Nami nasema ndugu zangu, hii ni fursa nzuri kwa Watanzania, ni kweli tunasema Kiswahili kila siku, lakini Kiswahili tunachokisema siyo Kiswahili sanifu. Wenzetu wa nchi jirani wanajitahidi kusema Kiswahili sanifu na kujifunza Kiswahili sanifu. Kwa hiyo, mimi nataka kusema kwamba nadhani kengele ya kwanza hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni ya pili.

**MHE. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba nimesimama hapa kuunga mkono hoja. Naunga mkono Azimio hili lipite, Watanzania tuwe mstari wa mbele kuenzi lugha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## **TAARIFA**

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Nilitaka kumpa taarifa mzungumzaji aliyepita aliposema kwamba lugha rasmi ya Bunge ni Kiswahili. Nilitaka tu kumjulisha kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya 144(1) ya Kanuni zetu, shughuli za Bunge zitaendeshwa katika lugha ya Kiswahili au Kingereza. Alichokisema siyo sahihi.

**MWENYEKITI:** Naamini taarifa imepokelewa. Sasa tuendelee. Nadhani alichokuwa anaongea msemaji, unajua akina Mzee Mlokozi wako wengi humu ndani. Ninaposema Mlokozi, mnanielewa. Kuna pahali usipoongea neno moja Kiingereza hawakujui kama wewe umefika Chuo Kikuu. Kwa hiyo, naomba tuendelee.

Sasa namwita Mheshimiwa Machali atafuatiwa na Mheshimiwa Mkosamali na baadaye Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae. Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia juu ya kuanzishwa kwa Kamisheni ya Kiswahili hapa katika ukanda wa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kabisa niunge mkono wazo au hoja iliyoletwa na Serikali ya kuanzishwa kwa Tume hii ya Kiswahili ndani ya ukanda huu wa Afrika ya Mashariki. Ni wazo zuri, binafsi na mimi kama Mtanzania Mswahili, lakini naomba nianze kwa kueleza mambo machache kidogo, kwamba Serikali imekuwa ni muhalifu wa kwanza wa kutokutaka kuona Kiswahili kikisonga mbele au kikipiga hatua. Nasema ni mhalifu wa kwanza; kwanza, kwa kutumia ithibati au ushahidi wa taarifa yenyewe ambayo imewasilishwa na Serikali, imeandikwa kwa Kingereza. (*Makofi*)

Kwa hiyo, inawezekana leo tunaletewa kwamba, pengine tunataka ianzishwe hii Tume au Kamisheni ya Kiswahili, halafu Serikali yenyewe imeleta taarifa yake kwa lugha ya Kingereza. Kwa hiyo, nimeona kwamba sisi tumekuwa ni watu wa kusema tu, lakini vitendo tunaweka pembeni. Hili ni tatizo la kwanza.

Kwa hiyo, Serikali inawajibika kupiga hatua kwa kujifanyia tathmini wenyewe kwanza, kama kweli inataka kukienzi Kiswahili na kuhakikisha kwamba Kiswahili kinakuwa ni lugha rasmi, lakini pia ni lugha katika maeneo mbalimbali ya kikazi, basi ikenzi Kiswahili kwa vitendo na siyo kukienzi kwa maneno matamu matamu kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri alivyokuwa akiwasilisha hotuba yake hapa Bungeni.

Vile vile Serikali ni mhalifu wa kwanza kwa kuwa imeruhusu kuanzishwa kwa shule nyingi za Kingereza ambazo zimepewa jina la *English Medium Schools* kwa maana ya shule za chekechea kwa maana ya

*kindergarten* lakini pia Shule za Msingi. Sasa yote hii siyo kuki-*promote* Kiswahili ila ni kukiangamiza. Kwa hiyo, Serikali inawajibika kuangalia upya Sera zake za kuruhusu kuwepo kwa utitiri wa shule nyingi ambazo zimekuwa zinatoa elimu kwa kutumia lugha ya Kiingereza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, ku-*promote* pia siyo Kiswahili. Tuendeleo. (*Kicheko*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ndiyo masuala haya ambayo alikuwa anazungumza Mheshimiwa Mkuchika, masuala ya *code switching* na *code mixing*. Kwa hiyo, hatuwezi tukakikuzi Kiswahili kwa kuendelea kuwa na mtazamo au njia hii ya kuhakikisha kwamba Kiingereza kinapenya katika maeneo mengi kama ilivyo katika maeneo mbalimbali hasa ya utoaji wa elimu kama kwenye Shule za Msingi ambazo zinazidi kumea kama uyoga katika maeneo mbalimbali.

Kwa hiyo, Serikali inawajibika sasa kuangalia upya kama kweli tunataka kuona Kiswahili kinapiga hatua, tupunguze uwepo wa shule nyingi ambazo zinafundisha au zinatoa taaluma kwa kutumia lugha ya Kingereza na lugha nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka hapo, Watanzania sasa tumejikuta kwamba tumekuwa ni kama watumwa wa lugha za kigeni, tumekuwa ni watumwa wa lugha za kigeni kana kwamba mtu imefika mahali bila kuzungumza Kiingereza unaji-*feel* au unajiona kwamba wewe kama vile sio msomi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawajibika sasa Serikali kuhakikisha kwamba itungwe sheria ambayo itakomesha na kuweza kupiga marufuku matumizi makubwa yaliyokithiri ya lugha za kigeni.

Tunapokuwa tuko kwenye vyombo vya kufanya maamuzi kama hapa Bungeni, tunapokuwa kwenye warsha mbalimbali, tupige marufuku matumizi makubwa ya lugha za kigeni kama vile Kiingereza na lugha nyingine, itakuwa ni njia au mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili inazidi kukamata hatamu katika maeneo mbalimbali. Vinginevyo, tunazidi kukiangamiza Kiswahili. Kwa hiyo, tumejikuta kwamba tuna-*create* au tunatengeneza utumwa miongoni mwetu sisi wenyewe. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa na wewe ni mhalifu namba mbili. Tuendeleo. (*Kicheko*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hii yote ndiyo ile kitu ambayo tunasema kwamba ni athari za Kikoloni zote hizi na hii yote, ni nani kasababisha? Ni Serikali iliyoko madarakani ndio ambayo imetufanya tuwe hivi, sio sisi! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni Serikali iliyoko madarakani ndiyo imetufanya tuwe hivi, unaenda mahali, unajieleza unatafuta huduma, unaambiwa zungumza Kiingereza na wakati Watanzania wenyewe nikizungumza Kiswahili wananielewa. Ndiyo maana tunakuwa hivi. Kwa hiyo, chanzo ni Serikali yenyewe. Mheshimiwa Waziri



naomba kwa kweli ku-*check* na watu wa Serikali ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukawa sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, ukienda kuangalia moja ya lengo au dhumuni la kuanzishwa kwa Tume hii, pale lengo la 2(b), naomba ninukuu halafu nitaendelea. Wanasema kwamba, *"Specifically, the Commission shall develop Kiswahili as a regional language expressing and conveying positive African values with respect to issues of gender equity, human rights and democracy."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia hapa masuala ya haki za binaadamu pamoja na demokrasia, bado niseme tu kwamba Serikali haijaweza kulienzi na kuliheshimu wazo hili. Huwezi ukasema kwamba lugha ya Kiswahili itatumika katika kuhakikisha kwamba masuala ya haki za binaadamu na demokrasia yanapatikana, wakati tukifanya tathmini hapa, ni Watanzania wangapi ambao wana uwezo wa kuzungumza lugha ya Kiswahili pamoja na lugha za kigeni? Wengi utakuta ni Waswahili, lakini twende kwenye vyombo mbalimbali vya kufanya maamuzi kama vile Mahakama. Nitaomba nizungumzie hapa kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nakumbuka nilimwuliza swali Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwamba, ni sababu gani ambazo zinapelekea Mahakama zetu kuandika hukumu kwa lugha ya Kiingereza? Sababu iliyotolewa na

Serikali ni kwamba inaonekana kwamba taaluma ya Sheria inahitaji matumizi maalum ya istilahi ambazo kwa kweli zinaweza zikafikisha ujumbe kwa urahisi, jambo ambalo mimi binafsi napingana nalo kwa nguvu zote. Leo tuna taaluma kama za *ICT, Information and Communication Technology*.

Ni taaluma ambazo ni ngeni sana katika nchi yetu, lakini ukienda kwenye maduka ambayo yanauza vitabu, utakuta kuna Kamusi. Wataalamu wetu wameweza kutengeneza Kamusi ambazo zinahusiana na masuala ya *ICT*, lakini Serikali leo inasema kwamba hakuna istilahi ambazo ni maalum ambazo zingeweza kutumika katika Sekta ya Sheria.

Wazo hili naomba Serikali kwa kweli muweze kuangalia vizuri. Nenda kuna Kamusi ziko chungu nzima wametengeneza wataalamu wetu wa Kiswahili waliobobea kama akina Prof. Kahigi. Prof. Kahigi namtambua sana kama ni mtaalamu aliyebobea katika *field* ya Kiswahili, amenifundisha Kiswahili kwenye *level* ya Chuo Kikuu. Kwa hiyo, ninapozungumzia lugha ya Kiswahili kwamba ile dhana ya Watanzania ambao wamekua wakizungumza, kwamba Kiswahili hakina msamiati wa kutosha, hakina istilahi za kutosha, naomba, hebu tuache kuendelea kuwapotosha na kuwadanganya Watanzania, kwa sababu msamiati upo na ndiyo maana jana nikasema Mheshimiwa Waziri anaweza akatupatia taarifa za tafiti ambazo amefanya?

Nakushukuru Mheshimiwa Waziri alikuwa mkweli, alisema kwamba hawajafanya utafiti ambao ni *official*. Ningemtaka atuletee utafiti huo ambao unaonyesha

kwamba Kiswahili kimepungukiwa msamiati. Ziko Kamusi nyingi na ndiyo maana hata Kamuzi za Kiswahili kwa Kiingereza zimeandikwa.

Hiyo ni ishara kwamba tumepiga hatua katika kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili inaimarika, na matokeo yake sasa suala la kuendelea kuandika hukumu kwa lugha ya Kingereza, tunawanyima haki Watanzania wengi ambao hawajui lugha ya Kingereza. Kuanza kutafuta watu ambao watafanya tafsiri ya hukumu au maamuzi ambayo yamefikiwa na Mahakama zetu, naomba nishauri Serikali, kuna haja ya kuhakikisha kwamba sheria zote ambazo zinatungwa kuanzia sasa hivi Miswada iletwe kwa lugha ya Kiswahili ndani ya Bunge.

Turejee uliokuwa Muswada wa mabadiliko ya Katiba, mwanzoni ulikuwa umeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, baadaye tumepiga kelele hapa ndani, Serikali mlikwenda mkatafuta watu wakaweza kutafsisri na mkaleta kwa lugha ya Kiswahili. Mnataka kutuambia kwamba ile lugha mliitoa wapi kama Kiswahili hakina msamiati wa kutosha?

Mheshimiwa Spika, leo kuendelea kutuambia kwamba sheria nyingine haziwezi zikatafsiriwa, mnapata wapi ujasiri huo Serikali? Serikali nitaomba mtupatie majibu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ambayo inasimamia masuala haya, tunaomba mtueleze ujasiri wa Serikali kuendelea kuzungumza kila siku kwamba Kiswahili hakina msamiati wa kutosha. Huo ujasiri mnaupata wapi kama siyo utumwa wa Kikoloni? Utumwa wa Mataifa ya kibeberu

ambayo yamekuwa yanatupa masharti magumu kwamba ili kusudi tuwapatie misaada ni lazima mtumie lugha yetu. Tumeshuhudia Rais Kagame aliwapinga Wafaransa na akasimama kidete baada ya kusema kwamba yeye sasa anatangaza kwamba wataanzia kutumia pia Kiingereza katika nchi ya Rwanda. Sasa sisi urahisi unatoka wapi?

Naomba turejee Muswada ulioletwa Bungeni wa mabadiliko ya Katiba; ulioletwa kwa lugha ya Kiingereza na baadaye baada ya kupiga kelele, mlikwenda kufanya tafsiri na mmeleta na leo tumepata Sheria ya Mabadiliko ya Katiba iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Sasa tukienzi Kiswahili kwa vitendo, tusikienzi Kiswahili kwa kuleta maazimio mbalimbali na hotuba nzuri nzuri ambazo mmekuwa mnatuletea, halafu mkienda kwa pembeni, mnafunika kombe. Bungeni ni suala tu kwamba la *formalities*, ni kautaratibu ka kawaida, tutasema sana pale, halafu imetoka, hatujengi Kiswahili chetu, ila tunazidi kukidumaza Kiswahili chetu na hasa huko Mahakamani. Wako watu wengi wanadhulumywa haki zao kwa sababu hawajui kusoma Kiingereza na kuweza kukitafsiri. Sasa nini kifanyike? Hasa kwenye hili kwa upande wa Mahakama, ninashauri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kengelee ya kwanza hiyo.

**MWENYEKITI:** Ni ya pili. Nakushukuru. Tutaanza na wewe!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

**MWENYEKITI:** Nakushukuru kwa mchango wako japo umechanganya Kiswahili, Kiingereza, ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Kigola, Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Tundu Lissu wajandae.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii. Hili na mimi niweze kuchangia mambo machache kuhusu Azimio letu la kuunda Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili ni zuri sana, nami nafurahi napata faraja kwamba tunaendelea kui-*promote*, kuiendeleza lugha ya Kiswahili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya Kiswahili hasa Sera yetu ya lugha ya Kiswahili, Sera ya Lugha, bado haijaleweka vizuri na haijasimamiwa vizuri, lugha rasmi ya Serikali ni ipi? Mimi kwa mfano nimekuwa nikihudhuria baadhi ya vikao vya Madiwani kule Vijijini, nyaraka za Serikali zimeandikwa kwa Kiingereza na hawa Madiwani wengine hata Kiingereza hicho hawakifahamu. Sasa nataka mniambie, Sera yenu ni ipi? Kwa sababu mnasema Sera, Kiingereza kwenye mambo ya Kimataifa na kadhalika. Sasa Sera ni nini? Sera yenu ya lugha ni ipi Vijijini, Serikali za

Mitaa na Serikali Kuu? Sera yenu ya lugha ni ipi? Kwa sababu lazima ieleweke na tuisimamie na huu mkanganyiko ndiyo umekuja sana mpaka kwenye Sekta ya Elimu. Sera haieleweki, Shule za Misingi, leo Tanzania tumeungana kwa sababu ya Kiswahili, lakini tunakokwenda, watoto hao wanaoishi *boarding* miaka saba, wanaongea Kiingereza kila siku, inawezekana bado tuko kwenye kipindi cha mpito.

Baadaye inawezekana hawa wasije wakajua Kiswahili vizuri, tusipowawekea mkakati unaoeleweka wa Sera ya Lugha. Kwa hiyo, Taifa linaweza kuja kugawanyika kuwa na watu wa aina mbili; wanaojua Kingereza na wanaojua Kiswahili. Kwa hiyo, Sera yetu ya elimu ikoje? Kumekuwa na mitazamo miwili kuhusu elimu. Kuna watu wanaeleza kwamba kuna sababu zinazofanya tuendelee kufundisha kwa Kiingereza katika elimu ya Sekondari na kuna wale wanaoeleza kwamba tuanze kutumia Kiswahili.

Watu wametoa mitazamo miwili; hawa wanaosema kwamba tuendelee na Kiingereza elimu ya Sekondari, wanatoa sababu mbalimbali, mojawapo ikiwa gharama, lakini hatujawahi kujua au kusikia kwamba mlifanya utafiti mkagundua kwamba ni gharama kiasi gani inahitajika ili kubadilisha Mitaala yetu. Watu wasome Kiswahili mpaka sekondari na Vyuho Vikuu. Mimi ninavyoamini na nimesoma Kiswahili mpaka *Form Six* nikapata 'B' nzuri tu. (*Makofi*)

Wale watu wanaoeleza, wanasema watu wa saikolojia kwamba unapomfundisha mtu kwa lugha nyingine, haelewi kama angejifunza kwa lugha ya kwanza, na ndiyo kitu kinachoendelea kwenye nchi hii. Watu wanasoma *Form One, Form Two, Form Four* mtu ukimuuliza Fizikia ni nini?

Atakuelezea vizuri tu, amekariri. Lakini mwulize hicho kitu ni nini? Maana yake ni nini? Hawezi kukwambia. Sasa tunakwenda wapi? Tuendeleo na elimu hii ya kutukaririsha watu kwa lugha nyingine. Tunao China na nchi nyingine wanajisifia kwa lugha zao. Sisi mtu kuongea lugha ya kigeni anajiona kama ndiyo mtu wa tofauti, kumbe ni utumwa tu, wala Kiingereza siyo lugha *special*, yaani ya tofauti sana. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo lugha ambayo inazidi Kiswahili, yaani hakuna kipimo, hakuna mzani wa kupima kwamba lugha hii ni bora kuliko lugha nyingine. Labda kama tumekubali kwamba sisi Tanzania na Afrika tuathiriwe na utandawazi ili tusiathiri utandawazi, kama tutakubaliana na hivyo kwamba utandawazi ni siyo kuwa Kijiji, kama sisi hatutaathiri Vijiji vingine, ila Vijiji vingine vituathiri, basi tuendeleo na mifumo yetu hii ya elimu na mifumo yetu hii ya Sera za lugha.

Mimi niombe jambo moja kubwa sana kwamba, hii Tume ambayo tunaiunda leo ifanye kazi kubwa ya nje ya nchi. BAKITA, TUKI na nani wabaki na shughuli za ndani kufanya tafiti zetu za ndani, Mitaala kushauriana na Wizara na vitu vingine vinavyohusu Kiswahili ndani. Hii Tume kazi yake kubwa ihakikishe na tunapofika pale, ikiundwa, tujue Kenya wanataka walimu wangapi wa Kiswahili, Uganda wanataka walimu wangapi, ndiyo iwe kazi yake kubwa, itusaidie katika mambo ya nje kuliko hata mambo ya ndani ya kueneza lugha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia la mwisho, ningependa kupata majibu ya Serikali. Sisi utamaduni wetu

ni Kiswahili. Sasa utamaduni huu tunauenzi namna gani? Kwa sababu bado yaani kinadharia ni kama tunasema kwamba tunapenda Kiswahili, lakini kivitendo haipo. Mchangiaji aliyepita ameeleza vizuri hata Maazimio, Mikataba hii ambayo bado mnaingia Afrika Mashariki, mnaandika kwa Kiingereza. Sasa eleza ni namna gani wakati hata Mikataba yenyewe hii bado mnatuletea Bungeni kwa lugha ya Kiingereza. Kwa hiyo, kama tumeamua jambo fulani, tulisimamie, tuwe na uhakika nalo. Kama tunaona kwamba Kiingereza ni bora, tukisimamie kuliko kwenda na mikanganyiko ya namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ninaunga mkono Azimio hili. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mkosamali kwa mchango wako. Namwita sasa Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Tundu Lissu wajandae. Mheshimiwa Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hii mada ya leo ambayo ni muhimu sana kwa Watanzania pamoja na Afrika Mashariki. Ni kwamba mimi hapa nilikuwa nashangaa kidogo kwamba imeonyesha kwamba toka mwaka 1930 Afrika Mashariki walishaona hilo na wenzetu Wakoloni waliona kwamba Kiswahili katika Afrika ni cha msingi sana, wananchi waongee Kiswahili. Sasa kama mwaka 1930 waliliona hilo suala, sisi tumekuja kuliona leo kwamba Tume ianzishwe kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Kiswahili? Lakini mimi ninachotaka niseme kwamba nashukuru Serikali kwa kuleta



mjadala huu tuweze kuujadili na kuliweka sawa na tuone kwamba katika Afrika Mashariki Kiswahili kinapewa kipaumbele.

Sisi tumeona hata katika hao wawekezaji wanakuja kuwekeza kwenye nchi yetu, utakuta Mikataba mingi sana inaandikwa kwa Kiingereza. Sasa kama Mikataba mingi inaandikwa kwa Kiingereza na wale watu unaoingia nao Mikataba wanajua kuongea Kiswahili, kuna masuala mengine yanawekwa pale, vifungu vingine watu hawaelewi. Cha ajabu unakuja kuona kuna siku watu wanapelekana Mahakamani, sheria inaweza ikaona inamkandamiza yule mtu ambaye alikuwa anaingia Mkataba naye, ameingia Mkataba bila kujua. Sasa napenda niseme kwamba ikija kubainika Kamisheni hii ikimaliza kazi na Kiswahili kikapitishwa na ikionekana ile Mikataba ya Kiingereza iliandikwa, kuna mambo fulani tulikuwa hatujayaelewa.

Sasa baada ya kutafsiri kwa Kiswahili tukajua kwamba kuna makosa yalifanyika na sisi tukaingia tofauti, nadhani sheria nyingine tena ilibidi ziangaliwe zichukuliwe hatua. Kwa mfano, unaweza ukaona kuna Mikataba ya Wafanyakazi. Mikataba ya Wafanyakazi inaandikwa Kiingereza, sasa na yule mfanyakazi Kiingereza hajui, sasa inakuja tatizo wakati wa kuja kupata mafao yake. Anakuja kupiga hesabu baada ya kupata kiasi kikubwa mtu

amefanya kazi miaka 20, miaka 10 utakuta anapata Shilingi milioni mbili, anakuja kusomewa hesabu anasema Mkataba ndivyo unavyosema. Kumbe yeye hakuelewa vizuri. Sasa ikija kubainika kwenye Mashirika yale ambayo wameandika Mikataba kwa Kiingereza kwa wafanyakazi wetu, nadhani sheria itabidi iangalie upya kwa udanganyifu wa kuingia Mikataba kwa Kiingereza kwa mtu ambaye hajui Kiingereza.

Suala lingine la msingi ambalo naliona, katika Afrika Mashariki sisi tunashirikiana katika biashara. Sasa kama tunashiriki katika Afrika Mashariki kwa biashara na Afrika Mashariki ukienda Kenya wanaongea Kiingereza, Watanzania Kiingereza walio wengi hawajui. Sasa tunasema Afrika Mashariki tunashirikiana biashara. Kivipi wakati mawasiliano ni magumu? Kwa sababu mawasiliano ndiyo yanaunganisha biashara mtu afanye biashara vizuri, sasa Kiswahili kitachukuliwa kipaumbele kwa Afrika Mashariki, tutakuwa tumeokoa Watanzania wengi sana. Watanzania wengi sana wanapenda kufanya biashara, lakini wanashindwa kuunganisha kufanya biashara vizuri kwa sababu lugha ya Kiingereza hawaijui. Kwa hiyo, mimi huu Muswada nakubali kabisa kwamba kuanzia leo, tena nadhani inacheleweshwa, ingekuwa tunapitisha kesho ili uanze kutumika, ningefurahi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo naliona, hata matangazo ya biashara ya kawaida ambayo tunayo, tunatangaza kwa Kiingereza, ndiyo maana hata Mlima Kilimanjaro kipindi wananchi walishindwa hata kuupigia kura kwa sababu matangazo mengi sana ni ya Kiingereza. Sasa utainuaje biashara kwa Kiingereza wakati Watanzania

wengi hawajui Kiingereza? Tukapata maksi chache kwenye Mlima wa Kilimajaro. Lakini tungekuwa tunatangaza kwa Kiswahili, maana yake Watanzania wengi wangeweza kupeleka maoni yao, sasa wanapeleka maoni wachache tu wale waliosomea Kiingereza.

Kwa hiyo, sisi itatusaidia kwa asilimia kubwa sana. Halafu suala lingine nimeliona kwa wawekezaji. Wawekezaji wengi sana wananunua maeneo, sasa wakinunua maeneo wanaingia Mikataba na Wanavijiji, sasa ole Mikataba kama imeandikwa Kiingereza, Wanakijiji wetu wanajua Kiingereza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba yoyote ambayo imeingiwa na Vijiji vyetu vya Tanzania, Vijiji vyovyote ambavyo viko Tanzania, kama Mikataba ile mwekezaji ameingia na Kijiji, halafu imeandikwa Kiingereza, ile Mikataba lazima irudiwe upya kwa sababu huwezi ukaingia Mkataba kwa lugha ya Kiingereza na Wanavijiji na unajua kabisa Wananchi wetu wa Vijijini hawajui Kiingereza, halafu tunasema maeneo ya mwekezaji.

Huu Mkataba umeandikwaje? Tunasema Wanakijiji walikaa waka-sign; sijui waka-sign minutes, waka-sign muhtasari, walivyo-sign sasa walikubaliana; walikubaliana muhtasari gani huo? Unakwenda kwenye muhtasari tofauti, unakwenda kwenye Mkataba unaelezwa kwa Kiingereza, mambo yanakwenda tofauti. Kwa hiyo, wawekezaji wanachukua maeneo makubwa na wameingia Mkataba

na Wanavijiji kwa Kiingereza na ikibainika kwamba Mkataba umeandikwa kwa Kiingereza, huo ni batili, siyo Mkataba tena. Sisi tunataka Mikataba yote wanayoingia kununua ardhi yetu iandikwe Kiswahili, wananchi waweze kuielewa vizuri. Hiyo itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba yoyote kwenye Makampuni yoyote kama mfanyakazi Mkataba wake umeandikwa kwa Kiingereza na mfanyakazi hajui Kiingereza, hiyo Mikataba ibadilishwe iandikwe Kiswahili. Bahati nzuri sana mimi kwenye Wilaya yangu ya Mufindi Kusini nilishatoa kauli.

Nilisema wawekezaji wote waongee Kiswahili na wafanyakazi, kwa sababu wafanyakazi wale wote wanajua Kiswahili. Bahati nzuri na wale wawekezaji wameshajifunza Kiswahili na sasa hivi wanaongea Kiswahili. Sasa bila kuweka msisitizo ule wasingeeongea. Lakini sasa wanaongea Kiswahili na wananchi wanaelewa na wananchi sasa hivi wanaangalia haki zao. Kwa hiyo, wanaangalia hata mishahara mingine utakuta mtu anaandika *bonus*, mtu hajui *bonus* ni nini. Mtu unaandika *overtime*, *overtime* hajui sasa huyo mtu wa kawaida anaona karatasi kwenye Mkataba wake imeandikwa *overtime*, lakini halipwi.

Kumbe ilikuwa ni halali yake apewe na anafanya kazi zaidi ya ule muda aliopewa. Sasa kwa sababu, hajui hawezi kulalamika kwamba, ni haki yake. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba, kwa Serikali, Mikataba yoyote ambayo imeingiwa na wafanyakazi wa kawaida, imeandikwa kwa Kiingereza, tukiridhia hii, ianze kubadilishwa iandikwe kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa shule zetu ni kwamba, lugha ya Kiingereza, haiwezi kufutwa moja kwa moja kwa sababu, ukienda Kimataifa, hata ukifanya biashara za Kimataifa ni lazima uongee Kiingereza, kuna Mataifa mengine mnaongea Kiingereza, lakini litumike kama somo la kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, somo la Kiingereza linakuwepo kama somo. Watu wanaosoma masomo, kwa mfano wana masomo saba likiwepo somo la Kiingereza, hakuna tatizo. Sasa watu wengine wanatafsiri tofauti, wanafikiri kwamba, Kiingereza kinafutwa kabisa; sio kufutwa kabisa, ni kwamba, tuhakikishe kipaumbele tunaweka katika Kiswahili, katika Afrika Mashariki tunaweka Kiswahili, lakini somo la Kiingereza linakuwepo. Kwa sababu, kama unafanya *International Trade*, maana yake ni biashara za Kimataifa, hujui Kiingereza, maana yake utapata shida na hutoweza kufanya biashara za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe somo la Kiingereza linakuwepo vile vile na wale watu ambao wanaweza kuongea Kiingereza wanaweza wakaongea. Lakini tunasema kwa Tanzania, tuhakikishe Kiswahili kinapewa kipaumbele kwa mambo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, napongeza sana Baraza la Kiswahili, *BAKITA*. Wamejitahidi sana kuelimisha hata kwenye vyombo vya habari kwamba, Kiswahili kipewe kipaumbele. Wameeleza sana, wametuada

na sisi Wabunge kwamba, tukiwa Bungeni, tuwaelimishe wananchi wetu kwamba, Kiswahili kipewe kipaumbele. Kwa hiyo, natoa pongezi kubwa sana kwa Baraza la Kiswahili la Taifa, wamejitahidi na wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wengine wanaanza kukwepa, yaani badala ya kutangaza Kiswahili vizuri, utakuta wanaponda kama alivyoongea Mjumbe mmoja hapa, wanajua kwamba, mtu akiongea Kiingereza ndio msomi zaidi; kuongea Kiingereza sio usomi.

Wengine wanajua kwamba, ukiongea Kiingereza ndio utaalam, sio utaalam, hiyo ni lugha ya kawaida kama lugha nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hata watu labda wanakwenda kufanya usaili wa kazi. Utakuta mtu anaulizwa kwa Kiingereza, wanapima Kiingereza wanasema akishindwa hapewi nafasi ya kazi. Watoto wetu wengi sana wamemaliza hata vyuo vikuu wamekosa kazi. Hata kazi za Afrika Mashariki, ukienda pale utakuta Wakenya ni wengi sana, sasa wamekosa kazi pale eti wanasema ni kwa sababu yeye ameshindwa kuongea Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hata Watanzania, hata Mameneja maofisini; wakiwa wanatoa *interview* kwa wafanyakazi wetu yaani Meneja amekaa pale na yeye Kiingereza anababaisha-babaisha tu, lakini anamuuliza yule mwanafunzi ambaye ametoka Chuo Kikuu, akishindwa Kiingereza anamnyima kazi wakati ni Mtaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasisitiza kwamba, *interview* zote ambazo zinatolewa Tanzania hapa ziwe ni

kwa Kiswahili, halafu tuone watoto wetu kama hawatapata kazi. Watoto wetu wengi sana wameshindwa kupata kazi hata kwenye Mashirika ya Kimataifa; utakuta wameweka mtu ametoka nchi nyingine, kwani sisi hatuna wataalam wanaoweza kufanya kazi za Kimataifa hapa Tanzania? Wapo wengi, lakini wanaangalia Kiingereza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wengi sana wameshindwa kupata kazi mpaka sasa hivi wanahangaika kwa sababu ya *interviews* zinatolewa kwa Kiingereza. Sasa hilo linakuwa ni tatizo kubwa sana. Lakini kama tutapitisha lugha ya Kiswahili, maana yake ni *interview* zote ambazo zinatolewa kwenye maofisi yetu, kwenye ajira zetu, zitumie Kiswahili ili watoto waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta wanasema mtoto labda aandike *page* 12 aandike kwa Kiingereza, akikwama wanasema wanamnyima kazi. Wewe mpime mtoto kwa vitendo usimpime kazi kwa kuongea Kiingereza; kwa nini hujampima kwa Kiswahili? Kama wewe ni Mtanzania ni kwa nini usimpime kwa lugha mbili? Aongee Kiswahili, aongee na Kingereza au umwambie hebu chagua ni lugha gani unataka tukuulize maswali?

Mtoto mwenyewe achague ni lugha gani atumie ambayo anaweza kufaulu *interview* yake, lakini wewe unaanza kumkomalia Kiingereza ili ashindwe umnyime nafasi, kumbe wewe una ndugu yako unamsomesha Ulaya, umemleta hapa, unajua kwamba, atapata nafasi kwa vile

huyu ameshindwa Kiingereza, kumbe yule sio Mtaalam huyu anayekijua Kiswahili ndio Mtaalam zaidi. Yule amekuja tu kutoka nje wewe umemsomeshasomesha nje huko, sisi mtoto amesoma shule za Kata hapa anakwenda kufanya mtihani, unamwacha kumbe ndio Mtaalam, anajua na mazingira na ndiye angeweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapa kwenye haya masuala ya barabara, utakuta wanaofanya kazi pale anasema anajua Kiingereza, wanaojua Kiswahili na ni Wataalam wa barabara, wanajua barabara vizuri hawajapewa kazi eti kwa sababu, yule anajua Kiingereza; wakati kuna hao Wachina wanakuja wengine hapa Kiswahili hawajui, hata Kiingereza hawajui, wanapewa nafasi. Ni kwa nini tuiseme wanaojua Kichina tuwafukuze wote tusiwaone hapa? Lakini mtu hajui Kiswahili humpi kazi, anayejua Kichina unampa kazi, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haiwezekani, hatuwezi kuendelea namna hiyo. Ni lazima tusimame tujivunie Kiswahili na ajira zote tunatoa kwa watoto wetu wanaojua Kiswahili. Sio unampa mtu anajua Kichina, halafu ndio unampa barabara kwa sababu ya Kichina, sisi Kichina hatujui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunakagua barabara moja kule, watu wanaongea Kichina; sisi Kichina hatujui, bahati nzuri kuna Mswahili mmoja kasoma-soma Kichina pale na yeye akapewa nafasi ya kutafsiri, anaweza



akatafsiri tofauti kwa sababu, anatafsiri kwa sisi ambao Kichina hatukijui. (*Makofi/Kicheko*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Lakini pia, neno *interview* sio Kiswahili, ni usaili. Nakushukuru. (*Kicheko*)

Naomba nimwite Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Tundu Lissu, ajiandae.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza naomba niungane na wenzangu kuunga mkono Azimio hili, limekuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila tu naomba niseme kwamba, Tanzania itaongoza katika matumizi ya Kiswahili; nafikiri *Commission* hii haiwezi kuwa sababu ya Tanzania kuongoza katika matumizi ya Kiswahili; sisi tunaongoza katika matumizi ya Kiswahili tayari. Ni wengi zaidi, tunazungumza Kiswahili kuliko mtu yeyote hapa duniani na

ndio tunazungumza Kiswahili fasaha kuliko mtu yeyote hapa duniani, sisi tunaongoza tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, si kweli kama tukiunda *Commission* hii ndio Tanzania itaongoza kwa kuzungumza Kiswahili, hata kidogo. Hii itakuwa ni msaada tu wa kuendeleza Kiswahili. Kwa hiyo, nafikiri hili neno uliloliweka hapo Mheshimiwa Waziri, sio sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ni nchi yetu ilifaidika sana na tukaimarika sana na tukawa na umoja na amani kwa sababu ya mawasiliano ya lugha yetu ya Kiswahili. Hapa katikati tumeanza kuikoroga kidogo, tunachanganyachanganya Kiswahili na Kingereza, lakini kwa kweli, ni lugha ambayo imetusaidia sana kujenga umoja wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri hilo ni moja ambalo limefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana. Lakini la pili, lugha inasaidia sana katika kujenga uchumi wa nchi. Mataifa kama China, ambapo leo kuna uchumi mkubwa, watu wanajifunza Kichina kwa nguvu. Kwa sababu, ili ufanye biashara na Wachina na kwa sababu, ni wachache wanaojua lugha nyingine zaidi ya lugha yao, imebidi watu wajifunze Kichina, ili kufanya biashara na Wachina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, na sisi Tanzania kwa sababu, tuna rasilimali nyingi na watu wanazitaka rasilimali zetu, wenzetu kama Waganda, sasa hivi wanafundisha Kiswahili kuanzia darasa la kwanza mpaka mwisho kwa sababu ya faida za kiuchumi zilizopo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Kenya, wanajifundisha Kiswahili kwa maana ya soko lililoko Tanzania. Lakini vilevile kwa kuangalia masoko ya nje ya kutumia lugha kwa ajili ya kujijenga kiuchumi; sisi hilo hatujalionna. Kwa hiyo, lugha kuitumia kama lugha, kama sehemu ya kujijenga kiuchumi, bado haijafanyika hapa Tanzania na tumelala usingizi, watu watatumia rasilimali hii ya lugha kuweza kuuchukua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sio *Commission* itakayotusaidia, ni Taasisi za Kiswahili ambazo zipo, ni Serikali yenyewe ambayo ipo, tuanze kukitumia Kiswahili maana hatujakitumia; tuanze kutumia Kiswahili kwa maana ya faida ya kiuchumi sasa. Tumekitumia Kiswahili kwa maana ya kujenga Utaifa wetu, tukitumie Kiswahili sasa katika kujenga uchumi wa Taifa letu kwamba, tutafaidikaje katika kutumia lugha hii kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda nje, leo tunakwenda katika Bunge la Afrika, tunazungumza Kiswahili, Bunge la *SADC*, ambapo kuna Msumbiji wanazungumza Kireno, Wakongo wanazungumza Kifaransa, nchi nyingine zote zilizobaki 10 zinazungumza Kiingereza; ni kwa nini sisi tusizungumze Kiswahili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo *SADC Forum* nenda. *PAN AFRICA* tunazungumza Kiswahili, juzi tumekwenda *IPU* kule tunakuta wenzetu wote wanakuja na lugha zao, sisi

watu tumekaa pale tunazungumza Kiingereza, kwa nini?  
Aibu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UNESCO* wameanza kutumia Kiswahili, siku nyingi tu. Wametangaza kwa kutumia Kiswahili, sisi wenyewe hatuna uchachu wa kuendeleza Kiswahili, hata pale tunapopata fursa hatuzitumii fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuja Rais Kikwete, katika Bunge hili. Akasema tumepata nafasi 500, wakati huo Libya za kwenda kufundisha Kiswahili; hebu tuiulize Serikali, ni watu wangapi katika 500 walipelekwa kufundisha Kiswahili Libya? Miaka mingapi ile? Hata nafasi za kiuchumi kwa kuendeleza watu wetu tumeshindwa kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema zipo fursa za kiuchumi kwa kutumia lugha. Ni lazima tuangalie sasa sisi wenyewe ndani, sio *Commission, Commission* zinafanya mambo yake ya jumla kwa jumla ya Afrika Mashariki, lakini sisi wenyewe ambao ndio hasa wenye lugha ya Kiswahili, kwa kiasi gani tutafaidika kiuchumi kwa kutumia lugha yetu? Niombe sana hilo tulizingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni asubuhi leo hapa Mheshimiwa Mnyaa, aliuliza swali akazungumzia suala la *Capital Punishment*. Sasa, tukasema ukishachanganya Kiswahili na Kiingereza kwa watu wa huko nje hawatafahamu umekusudia nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sheria zetu hapa Tanzania, ukiibiwa ng'ombe na Kijiji fulani, iko Sheria inasema uzifuate hizo nyayo mpaka Kijiji zinakomalizikia halafu utoe adhabu kwa wao huko ng'ombe

walikomalizikia. Kama waliibiwa 100, basi wao wote huko watoe ng'ombe 100, wao watajuana ni nani kaiba hao ng'ombe; iko Sheria hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kule Zanzibar, siku hizi vile vile watu wanapita nyumba kwa nyumba wanapiga bakora, utoe kaseti, yamini kadhalika, ndio *Capital Punishment*. Sasa alizungumza Kiingereza kikaingiliana maneno ikawa haikuweza kueleweka vizuri, alichanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hili ndio tatizo ambalo linapatikana wakati mwingine. Kwamba, hata yule unayemuuliza swali anaweza asielewe ulikusudia nini, kumbe alikusudia bakora zinazocharazwa Zanzibar kwa kila mtu sasa hivi.

Kwamba, huna kaseti, huna hiki, unacharazwa bakora. Unagongewa nyumbani, kuna *Capital Punishment* inafanyika pale, ndio alichokuwa anakusudia hicho, hiyo ndio *Capital Punishment* aliyoikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angeisema kwa Kiswahili tu kwamba, kuna adhabu ya jumla inafanyika, Waziri Mkuu, angefahamu vizuri hilo swali. Sasa nasema ni vizuri tu vile vile tunapojenga hoja zetu hapa ndani ya Bunge, tukawa tunaziwasilisha katika lugha ambayo inaeleweka kwa wananchi vile vile. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni lugha hii kutumika katika Taasisi. Tunapata aibu, tunapata kigugumizi; anakuja Rais kutoka Uchina, akifika hapa atazungumza lugha yake ya Kichina, lakini Rais wetu atazungumza Kiingereza, hapo ni kusema hapa hapa Tanzania hatuna basi, watu

wanaoweza kutafsiri lugha ya Kiswahili kwa Kichina, ili yule mwingine anayetakiwa kuambiwa asikie?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana Rais anapozungumza kama Rais, analizungumzia Taifa, Taifa ambalo linazungumza Kiswahili. Kwa hiyo, tungetegemea mgeni amekuja anazungumza Kichina, wala hatutafsirii kwa Kiswahili, tunatafsiriwa kwa Kiingereza; sisi wenyewe tunazungumza Kingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Kitaasisi ya Kiswahili vile vile nayo bado hayajafanyika, hata sisi Wabunge tunakwenda kwenye Semina unakuta mtu karatasi ile, nyaraka zimetengenezwa kwa Kiingereza.

Kwa sababu, mfadhili anasema hawezi kulipa pesa mpaka ionekane kwa lugha ya Kiingereza, tumekuwa watumwa bila ya sababu. Nashauri kwamba, matumizi ya lugha Kitaasisi, sasa ni lazima yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja imezungumzwa kuhusu Mahakama, pale Zanzibar wamejenga uwezo mkubwa sana wa kutafsiri lugha ya Kiingereza kwa Kiswahili. Kama mnataka kutengeneza Miswada ya Kiswahili, ukienda Zanzibar wako Wataalam, Waandishi wa Sheria wazuri, mmoja ni Mheshimiwa Abubakar Khamis. Ni Mwanasheria mzuri tu wa kuandika kwa lugha ya Kiswahili, Miswada ya Kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Hazina ipo, lakini kwa sababu, Kitaasisi hatutaki kuzitambua, ndio maana hazifanyi kazi zinakufa. Pale ambapo tuna shida kubwa,

ndio tunawaita, kama ilivyokuwa Muswada ule wa Katiba, ndio tuliwatafuta tukakaa nao, tukaandika; kwa hivyo, uwezekano huu upo, tutumie nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu na la mwisho, naomba sasa basi, kwa sababu, tunaunda *Commission*, suala la kuwa na uwiano wa matumizi yake katika Afrika ya Mashariki ni la muhimu sana. Moja ni Taasisi yetu hii ya Bunge. Tunapofanya chaguzi zetu hapa unaambiwa ujieleze kwa Kingereza; kwa sababu, sasa tunafanya na *Commission* ya Kiswahili, tuanzie hapo, Mheshimiwa Sitta, tuanzie hapo. Yale mambo yote tunayoyafanya sasa Afrika Mashariki, tuyafanye kwa Kiswahili kwa dhamira kabisa kwa sababu, kama hatukudhamiria kubadilika, hatuwezi kubadilika. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kubadilika kama hatuitumii hii lugha katika taasisi zetu. Taasisi moja kubwa muhimu ni Bunge, Bunge la Tanzania, Bunge la Afrika Mashariki, Bunge la *SADC*, Bunge la *AU*, Bunge la *APU* na kadhalika. Tukiitumia lugha humo, ndio tunaweza kuisambaza lugha vizuri na kila mmoja akaona kwamba, hii lugha kumbe ni rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hausa maneno yao kwa 45% ni Kiswahili, lugha ya Kihausa ya ki-Nigeria, 45% ni Kiswahili. Kwa hiyo, tuna nafasi kubwa tu ya kukipanua Kiswahili kwa sababu, wako wenzetu wanakitumia Kiswahili kwa wingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kongo pale wanakitumia Kiswahili, *DRC*, Mozambique wanazungumza Kiswahili kizuri

sana tu, Zambia wanazungumza Kiswahili kizuri sana. Kwa hiyo, hakuna tatizo kwenye *SADC Forum* nako tukatumia vile vile Kiswahili. Kwa hiyo, naomba suala la kutumia Kiswahili kitaasisi ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, namwomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie tu; hapa mmezungumzia kwamba, kuna suala la kuvunjwa hii *Commission* kwenye *Article* ya 25. Lakini hamkuandika ni utaratibu gani mpaka itafika rai ivunjike, mmeandika tu kuvunja; ni utaratibu gani utafikia mpaka ivunjwe, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natahadharisha hivi kwa sababu, tuna *experience* ya kuvunjika kwa *East African Community*. Sasa kama tunaweka tu kuvunja, hakuna utaratibu wa namna ya kuvunja katika Azimio lenyewe, nafikiri kuna mashaka kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono Azimio. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakushukuru pia kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Tundu Lissu na kwa vile muda utakuwa hauruhusu, atakuwa ni Msemaji wa mwisho. Baadaye nitatoa Mwongozo kama alivyohitaji Mheshimiwa Nyerere.

Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia huu mjadala muhimu. Kuna msemu wa Kiswahili unaosema



kwamba: “*Nguo ya kuazima haifichi uchi*”, aah, “*haisitiri matako*”. (Makofi/Kicheko)

**MWENYEKITI:** Tukumbuke lugha ya heshima. Ahsante sana, tuendeleo.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni msemo wa Kiswahili wala sio matusi, “*nguo ya kuazima haisitiri uchi; haisitiri matako*”. Samahani, nashukuru sana; nguo ya kuazima haisitiri matako. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uchi wetu katika lugha uko wazi na unatia aibu sana;. Kama kuna mtu anasikiliza Bunge hili Tukufu halafu akasikia aliyoyasema Mheshimiwa Hamad kwamba, *Capital Punishment* ni adhabu ya viboko; anayefahamu maana ya *Capital Punishment*, atajiuliza hilo Bunge la Tanzania lina Wabunge wa aina gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Capital Punishment* ni adhabu ya kifo sio adhabu ya viboko. Kwa hiyo, ninaposema uchi wetu ki-lugha unatia aibu, maana yake ni kama hiyo. Watu hawajui Kiingereza humu na sio humu tu, watu hawajui Kiingereza nje ya Bunge hili Tukufu. Watu hawajui Kiingereza Mahakamani, Majaji hawafahamu Kiingereza, ni aibu tupu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni aibu ya kujitakia. Sisi ni nchi ya awali ya Kiswahili. Sisi ni Taifa la awali la Kiswahili, lakini kama kawaida ya watumwa, tunaona aibu ya kile kilicho chetu, tunaona aibu juu ya sisi wenyewe tulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema nchi yetu ni nyumba ya awali ya Kiswahili. Tumekuwa tukizungumza tangu miaka ya uhuru kwamba, Kiswahili ni lugha ya Taifa. Tunapiga makelele kwenye majukwaa kwamba, Kiswahili ni lugha ya Taifa imetuunganisha, haya ni maneno ya bure tu. Inapofika kwenye masuala ya msingi tunagundua kwamba, sisi ni watumwa na Kiswahili, si jambo la kuonea fahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, tukiachia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 hii tuliyonayo sasa, Katiba zetu zote za miaka yote, zimekuwa ni za Kingereza. Pili, hata hii Katiba tuliyonayo sasa ambayo ni ya Kiswahili na ambayo hiyo ya Kiswahili Sheria inasema, hiyo ndio lugha rasmi ya hii Katiba, hata Katiba yenyewe ya sasa haitambui Kiswahili kama lugha ya Taifa. Nionesheni mahali ambapo Katiba yetu inasema lugha ya Tanzania itakuwa Kiswahili, kwenye Katiba yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria zetu zote zinazotungwa na Bunge hili na zilizowahi kutungwa na Bunge hili, ukiachia Katiba na ukiachia Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Sheria zetu zote zinatungwa kwa Kiingereza. Hata zile ambazo zina tafsiri ya Kiswahili, Sheria zetu zinasema ile iliyoandikwa Kiingereza ndio nakala rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Taifa la watumwa na watumwa huwa wanaona aibu ya wao ni akina nani. Watatafuta vitu vya kurefusha nywele, watajitahidi kujionesha wao ni wazungu kwa kujipaka vitu vya ajabu ajabu, watatumia lugha za kukopa hata ambazo hawazifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama zetu zinafunga watu, zinahukumu watu kunyongwa, kunyanng'anywa mali, zinaathiri haki za watu. Sheria zetu zinasema lugha ya Mahakama itakuwa Kiingereza au Kiswahili, lakini kama kawaida ya Watumwa Sheria inasema lugha ya rekodi ya Mahakama itakuwa Kingereza, hicho ambacho hawakijui. Mtu akisoma hukumu ya Jaji wa Tanzania leo, anajiuliza hawa watu ni wa wapi? Ni Taifa la watumwa na mambo ya kitumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kawaida ya watumwa, tunasema Kiswahili ni lugha ya Taifa, lakini tunapopeleka watoto wetu kusoma shule ya msingi mpaka darasa la saba, wakimaliza wanapoondoka shule ya msingi tunasema ahaa, Kiswahili hakifai tena tutaonekana wa ajabu tukizungumza Kiswahili. Kwa hiyo, lugha ya kisomo kuanzia kidato cha kwanza mpaka mwisho, ni lugha ya bwana mkubwa, ni lugha ya bwana. Sisi ya watwana ni Kiswahili, tunakiacha shule ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mikutano ya Kimataifa, nasikia watu wanasema AU, Umoja wa Afrika, unatambua Kiswahili kama moja ya lugha za Afrika, ahsante sana. Ningeomba tuletewe, kama inawezekana, Hotuba hata moja ya Rais wetu au Mawaziri wake katika hiyo Mikutano ya Kimataifa ya Umoja wa Afrika, ambako wamezungumza Kiswahili, hata moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumwa hawapendi kilicho chao, hawajipendi. Tunakwenda kwenye Mikutano ya Kimataifa Umoja wa Mataifa, lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kimataifa kwa sababu, inazungumzwa na nchi zaidi ya

moja ni ya Kimataifa, lakini tunakopa nguo ambayo haisitiri utupu wetu, tunachekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuchagua lugha, ni suala la kiuchumi. Ukiamua kwamba, Kiswahili ni lugha ya watwana, ukakopa Kingereza, unakwenda kwenye Mikataba na makampuni ya kigeni ukawaambia aah, sisi tutatumia lugha ya Kiingereza, hii ambayo hamuijui; matokeo yake ni kwamba, tunaingizwa kwenye Mikataba ya ajabu kwa sababu, tunasaini mambo ambayo hatuyajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza mabilioni na mabilioni na mabilioni ya fedha. Kwa hiyo, ni suala la kiuchumi, sio suala tu la lugha ya kunywa pombe kwenye baa. Ni suala la kiuchumi, ni suala la haki, ukiandika Mkataba wa wafanyakazi Kiingereza wasichokijua watasaini vitu wasivyovijua, wataumizwa haki zao kwa hiyo, sio suala dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho. Wazanzibari kama kawaida yao, wametufundisha sana. Walikuwa wa kwanza kutufundisha umuhimu wa kuwa na haki za binadamu kwenye Katiba. Wametufundisha kuwa na kura ya maoni kwenye mambo muhimu ya Kitaifa. Sasa wametufundisha juu ya kuwa na fahari na lugha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar, inatangaza kwa ufahari mkubwa kwamba, Sheria zote zitakazotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, zitakuwa ni za Kiswahili. Sisi tuliopo humu ndani kama kawaida ya watumwa, tunaendeleza mambo ya ajabu

ajabu, hatujui Kingereza, ukizungumza ni aibu tupu kama nilivyosema. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa vile tuko kwenye mchakato wa Katiba Mpya, kama sisi sio watumwa, kama mnataka kunikanusha haya niliyosema, Katiba yetu Mpya itangaze kwamba hii nchi ni ya Kiswahili, Lugha yake ni ya Kiswahili, Sheria zake ni za Kiswahili na ndio itakayokuwa Lugha ya Matumizi katika maeneo yote ya maisha ya nchi hii. Vinginevyo, tutaendelea kuwa watumwa, tutaendelea kuvaa nguo za kuazima tukifikiri tumefunika matako yetu kumbe yako wazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru kwa maelezo yako. Nadhani kama Taifa, tunaelekea sehemu nzuri kwamba, Kiswahili tukitangaze kwa nguvu zote kwa lengo la kupata kwanza umoja wetu, ajira kwa Watanzania na mambo mengine kama hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kusitisha shughuli za Bunge, nina matangazo yafuatayo:-

Tutakaporejea Saa 11.00, wafuatao naomba wajiandae watachangia. Tutaanza na Mheshimiwa Albert Obama, atafuatiwa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, atafuatia Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na wengine wataendelea kutajwa na atakayekuwepo Mezani.

Lakini, naomba pia nitoe Mwongozo kuhusu ombi la Mheshimiwa Vincent Nyerere, kwa kutumia Kanuni ya 68(7), kama Bunge hili haliwezi kujua habari ya Magereza.

Mwongozo ni kwamba, masuala ya Magereza yameanzishwa kwa Sheria ya Bunge na kwa maana hiyo, Bunge lina Mamlaka ya kuhoji mambo yote yanayoendelea katika Magereza. Kiti, kimemwagiza Waziri wa Mambo ya Ndani, kuja kuisoma *Prison Act* hapa, ili tujiridhishe na yale maelezo ya wafungwa wanakula milo mingapi.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli hizi mpaka Saa kumi na moja jioni. Ahsanteni.

*(Saa 6.55 mchana, Bunge lilifungwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea tunaanza na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Margret Sitta na Mheshimiwa James Mbatia wajiandae, Mheshimiwa Obama!

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kujadili hii

*protocol* ya Kiswahili. Kwanza kabisa naomba niseme mimi ni mmoja katika watu walioko kwenye Kamati iliyoletewa *protocol* hii na nimeshiriki, haya mengine ni mawazo yangu binafsi, lakini yale maoni ya Kamati yetu yaendeleo kuheshimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nafikiria kwa kuwa hii *protocol* ya Kamisheni ya Kiswahili ilisainiwa kwanza tarehe 3 Septemba, 2008, ni Kamisheni tu ambayo imechelewa kuletwa Bungeni. Kwa kuwa imechelewa kuletwa Bungeni kuanzia 2008 mpaka sasa tunairidhia Bungeni 2012, kwanza naona wameichelewesha sana. Kwa hiyo, naomba tu niunge mkono moja kwa moja kwamba, ni kitu kizuri, Kiswahili kiweze kukuzwa siyo Tanzania tu, lakini kiwe Afrika Mashariki na nchi ambazo zitajiunga huko baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kuona faida tutakazokuja kuzipata, lakini wasiwasi wangu ni kwamba, hata kama kitakuwa kinatoa ajira kufundisha katika nchi mbalimbali, lakini sijaona kama Tanzania tumeshakuwa na mfumo ambao sasa wale watakaokwenda kufundisha hata kama wakihitajika watakuwa na vyeti ambavyo vinastahili kufundisha mfano. Je, watu wangapi wanaofundisha Kiswahili Tanzania walio-*qualify* kufundisha madarasa ya awali na kweli akikuletea hicho cheti utaona ame-*qualify* kufundisha shule zetu za awali, Sekondari na Vyuho Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiria kwamba, umuhimu sasa wa Baraza letu la Mitihani kutoa vyeti kwa watu ambao watakwenda kwenye *career* za Kiswahili vyeti hivi vitolewe kwa madaraja mbalimbali. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini najaribu kujiuliza tena Wakenya sasa hivi ni *aggressive* sana kwenye kufundisha Kiswahili na kama tulivyoambiwa na mchangiaji mmoja kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tumia Kiswahili, *career* sijui ndio nini, tumia Kiswahili. Ahsante.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa sasa hivi Tanzania tukitafuta wale ambao wana vyeti vya kufundisha Kiswahili bado ni wachache. Kwa hiyo, nafikiria vile vile na *list* nzima za Walimu ambao wanajua Kiswahili.

**WABUNGE FULANI:** Orodha.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Orodha, nafikiri humu Bungeni tuna lugha mbili; hiyo ni kazi ya Kamisheni itakayofanya huko, mimi sifanyi kazi ya kamisheni natoa mchango. Kwa hiyo, hilo nalo nafikiria kwamba, ile orodha ya Walimu watakaofundisha Kiswahili kwa Tanzania waweze kujulikana kama wako Baraza la Mitihani, kama wako Wizara ya Elimu, kama wako Wizara ya Habari na Utamaduni ni vizuri nao hiyo taarifa wawe nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine sasa hivi Kiswahili ni bidhaa, ni bidhaa ambayo sasa itauzwa. Kwa hiyo, wauzaji sasa lazima watayarishwe na ndiyo maana nikasema kwamba lazima watu wafundishwe, wawe wameiva kwa kwenda kufundisha hiki Kiswahili kwa sababu sasa ni bidhaa ambayo itauzwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile wenzetu kama walivyosema, Kiswahili hiki wanakitaka si tu kukijua, wanataka wakifanyie biashara nchini kwetu Tanzania. Mfano, wako Wachina pale Dar es Salaam wanajua Kiswahili sana, wamejifunza wanauza maua Kariakoo. Sasa wamejifunza Kiswahili ili wachukue na biashara zetu, kwa hiyo tusijikute tunafundisha Kiswahili na vilevile tunatolewa kwenye masoko. Wachina pale wanauza maua, ukifika unaongea Mchina anaongea Kiswahili kumbe na biashara wametunyang'anya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri na sisi kama Watanzania tuweze kuliona hilo, wako Warundi, wako Rwanda, wanakazania kweli kweli mpaka wajue Kiswahili ili waweze kuingia Tanzania waweze kupata kazi za kilimo, waweze kufanya biashara na waweze kupewa maeneo ya kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri tujue hiki Kiswahili tunachotaka kiendelezwe na Kamisheni hii, Tanzania tumejiandaa vipi kwa sababu ukiangalia kwa umbali, licha ya kufanya Kiswahili kijulikane, sisi hatutakitumia sana kwa nchi nyingine kwa sababu Watanzania tulikuwa tunabaki nyuma kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nafikiria kwamba hii Kamisheni itakapokuwa imeanzishwa ya Afrika Mashariki, Kiswahili tumeshakijua, ni mikakati gani sasa ya kuuza Kiswahili cha Afrika Mashariki katika Mabara mengine, Kiswahili tutakachokuwa tunakijua Watanzania wote na Afrika Mashariki kitatusaidiaje kivita, kiuchumi kwa

kupambana na nchi nyingine. Nalo hilo ni muhimu sana ili tuweze kuliona ili tuweze kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaanza sasa hii Kamisheni itakuwepo, mitihani ya Kiswahili ile ambayo huwa inafanywa katika madarasa mbalimbali, je, hii mitihani itakuwa ni ya Afrika Mashariki au itakuwa kila nchi inajitungia mitihani? Ni vizuri tujue kama Baraza la Mitihani watachukua hilo kama ni sehemu ya kutunga mitihani ya Afrika Mashariki au ni suala tu la usahihi wa lugha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kazi za BAKITA na BAKIZA, zitakuwa zipi kama Kamisheni hii itakuwa inafanya kazi kwa ufasaha. Kwa hiyo, ni vizuri hizi taasisi zetu za Kiswahili za BAKITA na ile ya Zanzibar waangalie, usije ukakuta na wao wakamezwa wakajikuta sasa wanakuwa tu kama wanapeleka *document* kwenye Kamisheni huku na wao hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii ambayo imechelewa. Pia naomba na yale maoni yetu ya Kamati yaweze kuzingatiwa. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Tujitahidi, maneno ku-*qualify* hayatakiwa na ndiyo maana hata katika Bunge la Afrika Kiswahili kitafutwa sasa, kwa sababu Watanzania hamwongei Kiswahili.

Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Nyalandu na Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Mbatia wajiandae.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi kwanza kusema kwamba, naiunga hoja hii mkono asilimia mia kwa mia. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii na Naibu Waziri kwa mawasilisho mazuri ya Azimio hili. Ni Azimio ambalo kama walivyosema wenzangu wengine lingeweza kuja miaka kadhaa iliyopita na tungeweza kuliunga mkono kwa sababu ni Azimio nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujikita katika mambo machache, jambo la kwanza ambalo ningependa kujikita kwalo ni kwamba, katika nia yetu na azma yetu ya kutaka kukiimarisha Kiswahili ningependa kusiwe na hofu, ningependa kusiwe na mashaka juu ya nia ya dhati ya Serikali ya Tanzania pamoja na Serikali za Afrika Mashariki kutaka kuimarisha Kiswahili na labda watu wakawa na mashaka kwamba kuimarika kwa Kiswahili kunaweza kukazuiwa na kuwepo kwa lugha nyingine na ndiyo jambo ambalo nimelisikia sikia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niwatoe watu mashaka, mimi nilitoka Viwanda na Biashara tulikuwa tunafanya biashara, niko Wizara ya Maliasili na Utalii tunahitaji lugha nyingi kweli kweli. Tunahitaji vijana wetu wajue lugha nyingi kweli kweli na wakati ule ule tunahitaji Kiswahili kiendeleo kushamiri na inawezekana tukaimarisha Kiswahili, tukakipa Kiswahili kipaumbele na wakati ule ule tusije tukaondoka katika mfumo mzima wa dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 60 na miaka 70 wale waliozaliwa wakati ule walijulikana na natumia hili

neni siyo kwa sababu nachanganya Kiingereza ni kwa sababu hakuna tafsiri yake ya Kiswahili walijulikana kama jamii waliita *generation x*, ni kizazi cha wakati ule kilikuwa na tabia fulani fulani. Wale waliozaliwa kufikia Vita Kuu ya Pili ya Dunia walijulikana kama *baby boomers generation*, kilikuwa ni kizazi kilichokuwa na aina fulani ya tabia, mwelekeo, jinsia na mvuto wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizazi kilichozaliwa miaka ya 80 na kuendelea kikaja kujulikana kama *generation Y*, na kizazi hiki wamekifanyia uchunguzi, watu wengi wakakuta kizazi hiki kwanza kinahitaji kama vitabu vilivyoandikwa, kinahitaji ishara na miujiza, ni kizazi ambacho kina udadisi mkubwa, ni kizazi jasiri sana, ni kizazi ambacho hakina mipaka katika mawazo, katika fikira, katika wanachofikiria kukifanya katika ubunifu, ni kizazi ambacho mipaka haiwahusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni kizazi ambacho kilijulikana kama kizazi cha mtandao na kimeambukiza na vizazi vingine kwa sababu wanatembea na simu za viganjani, wanawasiliana kwa njia ya ujumbe mfupi mfupi unaojulikana kama *SMS*, wanawasiliana kwa njia ya simu, kwa njia ya barua pepe na simu za viganjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizazi hiki kimebadilisha maisha na mfumo tuliokuwa tunaufahamu na yameleta maneno mengi ambayo yameingia katika sehemu ya maneno au msamiati wa Kiswahili. Kizazi hiki katika maisha yanavyoendelea hakisubiri tena taarifa ya habari ya *TBC* ya saa mbili, hakisubiri taarifa ya habari ya *ITV* ya saa nne, hakisubiri magazeti ya kesho kwa sababu habari zote

zinapatikana kwa kadri zinapotokea kupitia *facebook*, wapo kwenye *twitter*, wanatembea na simu ambazo zinamwonesha uko wapi, uwongo umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizazi hiki ni kizazi tofauti, ni kizazi chenye haraka, ni kizazi ambacho kama nilivyosema kinahitaji ishara na miujiza na kizazi kinachotaka kujua watokapo, kinataka kujua walipo na kinataka kujua waendapo. Kiswahili kitaendelea kuwa lugha ya heshima, lugha ambayo lazima tuitilie mkazo, lugha ambayo ni lazima ikue na ni lazima iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kizazi kama nilivyosema dadisi, wanasema *miracles of science*, miujiza ya sayansi inaendelea kuongezeka na tathmini au *researches* hizi zinafanyika kwa lugha nyingi duniani, zinaunganishwa unapata kitu kimoja, dunia ya sasa ni kama Kijiji na Tanzania ni sehemu tu ya hicho kijiji, kizazi ambacho sasa dunia kwake ni kama kijiji hata suala zima la ajira limekuwa kama kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna ajira zinazojulikana, Kiswahili chake utanisaidia, lakini zinaitwa *outsourcing*, ni kazi ambazo vijana wetu wa University of Dar es Salaam au *Saint Augustine University* au hapa *UDOM* au *Saint John* na kadhalika watafanya kazi kwa niaba ya shirika la *ATNT* la Marekani wakihudumia wateja waliokaa Chicago na wao wako hapa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizazi hiki ni kizazi cha wakati wote, ni kizazi ambacho lazima tuwapanulie mawazo, tuwaambie inawezekana kulinda lugha yako mwenyewe kuifanya iwe na heshima na mvuto, watu wakaja kujifunza, lakini haijakuzuia wewe kujifunza lugha zingine kwa bidii kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Microsoft Corporation* kubwa duniani wamepiga hodi Nairobi, kwa sababu gani? Walipoangalia Nairobi, waliangalia uwezo wa vijana waliokuwa wanajua Kiingereza walikuwa ni wengi kuliko wa kwetu, waliokuwa wanajua lugha zingine zaidi ya Kiingereza walikuwa ni wengi kuliko wa kwetu. Waliokuwa wanaweza wakaunganisha *interacting language system*, Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, walikuwa ni wengi kuliko Dar es Salaam, wakaweka *headquarters* kwa eneo letu la Afrika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Google* imekuja kujulikana kama zamani walipojenga mnara wa Babeli, mnara mkubwa, watu waliunganisha lugha, wametafsiri lugha zote duniani, wameziweka katika simu yako ya mkononi, unaweza ukazifahamu na sasa wamezipenyeza katika maisha ya kila siku ya wanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ulipo ukishika simu yako wanakujua uko wapi, wanakujua unaongea na nani, una kula nini, dunia imekuwa kama kijiji na sasa imekuwa ni kama mnara wa Babeli. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na mfumo tu wa mawazo, tuseme inawezekana ukakiunganisha Kiswahili kikawa kikubwa, lakini

tukawabeba vijana wetu kwa mikono tuhakikishe kwamba wanasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nangaalia lugha zinazoongoza duniani ni zipi. Lugha ambayo inazungumzwa na watu wengi kuliko zote duniani ni *Chinese* Mandarin na hii asili yake ni *Saino Taibethan* sijui Kiswahili chake, lakini inazungumzwa katika Jamhuri ya Watu wa China, Taiwan, Singapore na baadhi ya maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi za Afrika wanasisitiza sasa watoto wao wajue Mandarin kwa sababu biashara kubwa zinafanyika, kufikia mwaka 2013 Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Utalii Duniani, *UNWTO* limesema China itaizidi Amerika kwa kuwa na watalii wengi duniani itakapofika mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, Afrika ilipata wageni milioni 50, ni wangapi kati ya milioni 50 waliokuja Afrika walikuwa wanaweza wakakiongea Kiswahili. Ndiyo maana katika kufanya hizi kazi ni lazima tufahamu tunaihitaji dunia, tunazihitaji lugha zingine zote kama zenyewe zinavyotuhitaji sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha inayofuata ni lugha ya Hindi au Hindu, inazungumzwa India na Pakistan na watu wengi. Inafuata lugha ya Kispania au Spanish inazungumzwa Spain na nchi zote za *Latin America* na *Southern Western USA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Amerika walipanga kwamba, wanafunzi wasifundishwe lugha nyingine zaidi ya Kiingereza, lakini kufikia mwaka jana wamesema Spanish ni lazima iendelee kufundishwa kama lugha ya pili katika *continental United States*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya nne ni hiki tunachokiita Kiingereza kwa idadi ya watu na hii ni katika Makoloni yote ya Uingereza, Amerika yenyewe ikiwepo, Seychelles, Newzealand, Afrika ya Kusini, Philipines na Makoloni mengine yote yaliyobaki Afrika yanaongea Kiingereza. Kiingereza ndiyo lugha iliyochaguliwa na Jumuiya ya Ulaya kuwa lugha ya sayansi na teknolojia katika karne ya 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokienzi Kiswahili tukibeba Kiswahili na nahau za Kiswahili, methali za Kiswahili tuhakikishe kwamba tunasukuma vijana wetu kama mvua waweze kujifunza hizi lugha zingine zote. Nchi jirani wameweza kujifunza lugha ya Kiarabu na kama tunavyofahamu nchi zote za Mashariki ya Kati na nchi zote za Kusini mwa Afrika zinazungumza hii lugha muhimu sana ya Kiarabu, ni lugha ambayo inatumika kwa biashara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kama mwakilishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuwasihi vijana wa Kitanzania waanze kujifunza pamoja na lugha zingine kama Kiarabu, lugha nyingine ni Bengali, hii ni ya Bangladeshi, lugha nyingine ni ya Kireno, Kirusi, Kijapani na Kijerumani.



Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimalizie kama nilivyoanza, Itifaki hii itasaidia kukiimarisha Kiswahili, itasaidia kuifanya Tanzania iwe kiongozi katika suala zima la kuongeza hamasa na hamu na shauku na mvuto wa lugha yetu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo nawaasa vijana wote kuanzia Tunduma mpaka Singida, kuanzia Kilimanjaro mpaka Mtwara, wahakikishe kwamba hakuna kijana anayemaliza kidato cha nne, kidato cha sita au Chuo Kikuu bila kujua lugha nyingine katika Jumuiya ya Ulaya, wanahakikisha vijana wanajua lugha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza wajasiriamali wote ambao wameweza kuthubutu wakaanzisha zile *English Medium*, wakaanzisha zile shule ambazo zinafundisha Kiingereza. Walimu Watanzania tunawapongeza, tunaomba mjitahidi, tunaomba tujifunze na lugha zingine, ni sera ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba Kiswahili ni cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sera ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba vijana hawa wanajua lugha zaidi ya moja kwa sababu biashara ya Kimataifa itategemea sana na uwezo wetu, itategemea sana na kujiandaa kwetu kama nchi, itategemea sana na sisi kuandaa vijana hawa kushindana na nadhani

tusizungumzie habari za ujio wa lugha zingine za kikoloni kama za makabaila, mabeberu, kuna vitu duniani, alisema mtu mmoja hutakaa uweze kuvibadilisha penda usipende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi lugha zimekuja, zitakuwepo na pamoja na nia njema ya kunyanyua lugha yetu, napenda nitoe onyo kwamba, haitawezekana katika dunia hii kufanya lugha zingine zisiwepo au zisiwe na maana au ziwe ndogo kuliko watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Namwita sasa Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa James Mbatia ajiandae na Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Kombo Hamis Kombo wajandae. Mheshimiwa Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyoko mezani ya kuridhia itifaki ya kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii pamoja na wanafamilia wote wanaoongozwa na Mzee Sitta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeweza kusimama hapa kutokana na ushirikiano mkubwa ninaopata kutoka kwa wanawake wa Mkoa wa Tabora kupitia UWT ambao wameendelea kunipa ushirikiano ndiyo maana napata nguvu ya kusimama hapa, nawashukuru sana akinamama.

Hali kadhalika niwashukuru sana Wana-CCM wa Urambo kwa kunipa u-NEC, ahsanteni Wanaurambo, tupo pamoja ahsante sana, hali kadhalika nawashukuru Wana-CCM wa Mkoa wa Tabora ambao wamenipa ujumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa. Nawashukuru sana na tutashirikiana vizuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii na nimeshiriki vizuri katika majadiliano. Kwa hiyo, naunga mkono yote yaliyowasilishwa na Kamati ya Huduma za Jamii na namshukuru sana Dkt. Kigwangala kwa kuwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki imewasilishwa leo rasmi, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuiridhie kwa sababu ina faida ambazo tayari wenzangu wamekwishazungumza. La kwanza, ambalo ningependa ni ufafanuzi kutoka kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kweli kwa kuleta itifaki, lakini yako mambo ambayo yanahitaji kuangaliwa kwa makini zaidi, la kwanza, tungependa kujua mpaka sasa hivi tumeshapata maombi mangapi ya Walimu kutoka nchi jirani au wanachama wa Afrika Mashariki, je, kuna maombi yoyote ambayo tumeshapata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna maombi yoyote tumeshapata, tumeweza kutimiza kwa kiasi gani inaweza kutusaidia kujua tulipoanzia na kujipima kwa baadaye tutakapokuwa tunaendelea kutoa wataalam wa Kiswahili kutoka nchi mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kufahamu kutoka Serikalini kwamba iwapo ziko fursa ambazo zilipatikana, wakapatikana Walimu kutoka Tanzania kwenda nchi jirani Kenya, Uganda na kadhalika hizo fursa zilipatikanaje. Swali langu hapa ni kuhusu uwazi je, vijana wa Tanzania wasomi, wataalam wa Tanzania wanazifahamu hizi fursa? Zinakuja kwa utaratibu gani kwa sababu nafikiri wako watu ambao wana utalaam tayari, wanaweza kufanya kazi hizo, lakini je, hizi fursa zinakuja kwa njia ya uwazi wa kuwezesha kijana wa Tanzania kuzifahamu na kuzifuatilia ili nao waweze kutumia ujuzi wao katika kuendeleza Kiswahili katika nchi jirani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, napenda Serikali inifafanulie, nilikuwa naangalia takwimu ya Wizara ya Elimu na kwa sababu suala hili mimi naamini halitafanikiwa kama hakutakuwepo na ushirikiano kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Michezo na Vijana pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, lazima wafanye kazi kwa pamoja kwa sababu wao kwa njia moja au nyingine wanahusika kwa upande wa utamaduni na utoaji wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi ambavyo hali itakavyojitokeza kwamba Kamisheni ikianza kufanya kazi kwa vyovyote idadi ya wataalam na Walimu watahitajika zaidi, lakini kwa takwimu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi nilizonazo zinasema kwamba, Walimu tu ambao tunawahitaji sisi wenyewe hapa Tanzania hasa Walimu wa Sekondari tayari kuna upunguf wa Walimu 2338 na hawa tunawahitaji katika shule zetu za Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo siamini kwamba, tunaweza kutegemea hawa Walimu wanaongojewa katika shule za Kata na nyinginezo ndiyo hao hao waende kufundisha nchi jirani Kiswahili. Maana yake ni nini, naamini Serikali itakuja pengine na mkakati wa kuongeza Walimu wa kufundisha somo la Kiswahili pia na wataalam wa kuendeleza Kiswahili nchi jirani. Je, Serikali inalifahamu hili na kama inalifahamu inaweka mkakati gani wa kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya Walimu na wataalam ambao watakwenda kuendeleza katika nchi jirani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiria niwaombe Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Habari, Utamaduni, Michezo na Vijana wakae pamoja na kuandaa mkakati. Badaaye watuletee, tuuone mkakati huo, kwa sababu sisi tunaamini Kamisheni ikianza kufanya kazi, ongezeko litakuwa kubwa, haitakuwa rahisi kutimiza idadi ya watu wataalam watakaohitajika kama tutaendelea na utaratibu huu huu wa walimu wanaopatikana kidogo kidogo ambao mpaka leo hii bado tuna upungufu mkubwa hata wa Walimu wa somo la Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu ni Wizara hizi mbili kwanza kushirikiana pamoja kuweka mkakati wa pamoja ambao kama nilivyosema hapo awali tungeomba tuupate na hasa sisi Kamati ya Huduma za Jamii. Nadhani tutawafuatilia kwa karibu ili tujue mkakati gani ambao watauweka ambao utasaidia kupata wataalam ili kukabiliana na hili soko ambalo litakuwa kubwa zaidi la ajira kutokana na mahitaji yatakayopatikana kutoka nchi jirani katika kuendeleza Kiswahili katika nchi

zao. Wakati huo tunaamini kwamba Kiswahili kikiendelea zaidi ushirikiano katika nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi zitakua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yangu ni hayo matatu ambayo ningeomba tu kumalizia kusema kwamba, kwanza nawapongeza sana Serikali kwa kuleta itifaki hii na nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuiridhie ili ianze kufanya kazi. Naamini yako maeneo ya Itifaki yenyewe ambayo itafanyiwa marekebisho hasa maeneo ya muundo wa Kamisheni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kimsingi tufahamu maombi ambayo tumeshapata, ni kiasi gani tumeweza kukidhi mahitaji yaliyotoka katika nchi jirani, lakini pia tujue Serikali watautumia utaratibu gani kuweka hizi fursa wazi ili vijana watakaopenda kufanya kazi hiyo Walimu na wataalam watakaopenda kufanya kazi hizo waweze kupata taarifa za fursa hizo kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mkakati utakaoandaliwa wa kupata wataalam hawa bila kutegemea hawa Walimu wanaondaliwa kwa utaratibu wa kawaida. Kwa sababu tatizo mojawapo ambalo limewWwalimu wa Tanzania ni kuwatambua kwa vyeti maalum. Hicho kimekuwa ni kikwazo kwamba, wengi wanapenda kupata Walimu ambao wana vyeti maalum vinavyowatambua kwamba wao ni wataalam katika lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo nashukuru na naipongeza sana Kamati yangu kwa ushirikiano. Pia

naishukuru Serikali kwa kuwakilisha Itifaki hii na naomba tuiridhie. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kutoa mchango kidogo kwenye itifaki au Azimio lililopo mbele yetu la Kamisheni ya Kiswahili ya ukanda wetu huu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukazungumza sana, tukaweka mikakati mingi sana, lakini yale tunayazungumza kwa dhamira njema, hatuyafanyii tathmini inatupa shida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili ni lugha ya Kimataifa, Kiswahili kiko nje ya mipaka ya Tanzania, lakini wenye mtoto wao Kiswahili tunaonea aibu lugha yetu sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mmoja au miwili, halafu nitaendelea, kwa kuwa, napenda kusema hoja kwa kielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwa Waholanzi mwaka 2007 mpaka 2009, kati ya masharti niliyopewa ili wakanitunuku *degree* niliyokuwa nasomea ya masuala ya Uhandisi yaani Shahada ya Uhandisi ni pamoja na kujifunza lugha yao.

Kati ya alama 180 nilizotakiwa nizipate ili niweze kutunukiwa hiyo shahada inabidi alama 40 ni kujifunza

Kiholanzi au ki- *Dutch* na ufanye andishi na uliwakilishe kwa ki- *Dutch*. Ni sharti la kwanza kabisa na wanajivunia lugha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwetu sisi hapa tunaona kuzungumza Kiswahili ni kana kwamba hujaelimika hivi. Kwetu sisi hapa tuna Wabunge wanaotoka kwenye Bunge hili wanakwenda kwenye Bunge la Afrika wanaogopa kutetea Kiswahili chao, mpaka watendaji wa Tanzania wanaokwenda kwenye Bunge kama wakarimani wanakuwa hawana kazi sasa na wanataka kufuta Kiswahili katika Bunge la Afrika kwa sababu hakina wasemaji. Sasa ninaona labda tuna tatizo, tujitafakari upya, kweli tuna tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutazungumza mengi kwa sababu nisingependa na hili ni jambo la Kitaifa, tusirushiane kwamba hili ni la Chama cha Mapinduzi. Sasa mkisema ni la Chama cha Mapinduzi labda mimi nikitoa vitabu ambavyo vimesimamiwa na Serikali vya Kiswahili, tutasikitika sana hapa, kwa sababu kwa mfano, hiki kitabu ni muhtasari kwa shule zetu za msingi, nitatoa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kwamba, makadirio ya kipindi kwa darasa la kwanza, urefu wa kipindi ni dakika 30. Hivi ni muda wa kipindi au ni urefu wa kipindi? Ni urefu! Hiki ni kitabu na ndiyo miongozo na hii ni *syllabus* au ni muhtasari ambao ndiyo unatumika shuleni leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kuangalia labda hata tuchukue muhtasari mwingine huu hapa, huu muhtasari



kwenye ukurasa wa juu umeandikwa *Ministry of Education and Vocational Training*. Ukurasa wa kwanza umeandikwa, siyo mimi lakini nasoma iliyopo hapa imeandikwa, *Ministry of Education and Culture*, kitabu hiki ndicho kipo kwenye shule zetu leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natafakari kwa upana kwa kweli na kwa chanya tu na wala siyo masuala ya kuumbuana, hapana! Lakini kama muhtasari wa shule zetu, *BAKITA* sijui wako wapi? Tatizo tulilonalo ni kwamba, tuna tatizo kubwa kwa hawa watendaji ambao uzalishaji wa hii mihtasari inayosimamiwa na Wizara zenye dhamana kwa ajili ya watoto wetu, ni vitabu vingi tu ninavyo, nilifanya utafiti zaidi ya miaka 17, nina vitabu vingi kweli vinavyofundishwa kwenye shule zetu, vyote hivi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie ndugu yangu aliyesema tujitahidi kupata lugha nyingi na nakubaliana naye kabisa kwa sababu sisi siyo kisiwa, tuseme tutajifunza Kiswahili tu, hapana! Nakubali tujue na Kiingereza vizuri na Kifaransa na Kijerumani vizuri na kadhalika. Hebu tuangalie sera yetu ya elimu ya Taifa, ili ambayo ndiyo tunayoitumia leo, sera ya elimu ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na uniruhusu tu nisome lugha ya pili tunayoisema tunaijua Watanzania, lengo la elimu ya nchi hii, kwa ruhusa yako. Inasema:

*“To develop and promote self confidence and an inquiring mind and understanding and respect for human*

*dignity and human right and readiness to work hard for personal self advancement and National improvement ..."* Hapa kuna neno 'and' saba, *National Education Policy* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Inasikitisha sana kwa kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inabidi, ni ushauri tu na ni kwa nia njema kabisa kabisa. Kwa kuwa, Bunge limepewa dhamana ya kuisimamia Serikali, yale yote tunayoyazungumza na tunayokubaliana tuangalie upya utaratibu wa uendeshaji Bunge ili kipindi fulani tujitathmini na tuikamate Serikali kwamba yale tuliyoagiza wamefanya nini badala ya kuendelea tu na mchezo huu tunaoendelea nao kila siku hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli inasikitisha sana, kwa sababu tutazungumza na tutakuwa kama tunafanya ngonjera tu, muda wa Watanzania tunautumia na fedha za walipa kodi tunazitumia hatujui tumeji-*organise* namna gani, inakuwa ni shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nakumbuka mwaka 2002 tarehe 14, Oktoba ilikuwa ni siku ya Jumatatu na ilikuwa ni siku ya kumbukumbu ya kifo cha Mwalimu Nyerere, tukaomba kuonana na Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Mheshimiwa Alhaji Ally Hassan Mwinyi. Tuliambiwa Mzee wetu huyu, tukajitafakari kwamba anakijua Kiswahili vizuri na ni Mwalimu mzuri wa Kiswahili. Sasa atufanyie nini Taifa namna ya kumuenzi vizuri Mwalimu Nyerere?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 15/10/2002, siku ya Jumanne tukaonana na Mzee Mwinyi na kweli siku ile

nilionana na Mzee Mwinyi, tukamwomba tuanzishe Taasisi ya Mwinyi ya Lugha ya Kiswahili ili tuweze kukipa nguvu Kiswahili katika Taifa letu, miaka kumi iliyopita, Mzee Mwinyi akakubali! Tukaiandikia Wizara mpaka kesho hawakujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namna tu ya kumwezesha Mzee Mwinyi aweze kusimamia vizuri ili tuweze kupata busara zake, asimamie Kiswahili kama zao la Taifa letu la Tanzania. Sasa ndiyo maana nasema tuna tatizo ambalo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hiyo nakumbuka tulipokutana na Mzee Mwinyi tulikaa na Ndugu Polisya Mwaiseje, akatufundisha, akatuambia hakuna kitu kinachoitwa kukariri, akasema badala ya kusema kukariri unasema kuhifadhi. Akatuambia hakuna kitu kinachosema onyesha bali unaonesha, ona. Kwa hiyo, Mzee huyu ni hazina, lakini tumemtumiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwamba, hili suala la ufisadi lipo kwenye utendaji wa Taasisi za Elimu za Taifa la Tanzania, *seriously!* Tusipoziangalia vizuri ikiwepo *BAKINA*, Taasisi ya Elimu, *EMAC* na zikiwemo na taasisi nyingine nyingi tu zinazosimamia mfumo wa elimu ya Taifa letu, tusipozichunguza vizuri haya yote tunayozungumza na ukitaka kuangamiza Taifa lolote na ukitaka kuua Taifa lolote anza kuua mifumo yake ya elimu inayolinda utu wa mwanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maangamizi tunayoyaona leo hii hapa Tanzania kuporomoka kwenye kila sekta ni kwenye

kuingiza ufisadi katika sekta ya elimu katika nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa kabisa na kwa dhamira iliyo safi kabisa naunga mkono Azimio hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa tisa mwaka 2012 tarehe 13, 14 na 15 siku ya Jumatano, Alhamisi, Ijumaa na Jumamosi nilikuwa Kenya. Wakenya ukitembea kwenye ndege zao wanatangaza kwa Kiswahili, wanaimba kwa Kiswahili kwamba karibu Kenya na Kiswahili ni lugha ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye Kamati yako, tulipokuwa Mkoani Kagera nikaja Mwanza, tukapanda ATC na Ndugu Rage kuja Dar es Salaam, ATC ndege ile moja lugha yao ya kwanza ni Kiingereza. Hata kutamka uwanja wetu wa Mwalimu Nyerere ni shida kwa wale watendaji kule ndani. Kwa hiyo, hatuna usimamizi na tunaogopa kufanya maamuzi magumu kwa maslahi ya Taifa letu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nihitimishe kwa kusema kwamba, uzalendo, hata elimu hii tunayosema tunaitoa, tunatoa elimu nzuri, wanasema kwa walionacho na elimu ya mlalahoi kwenye shule za Kata. Lakini hata hiyo elimu inaonekana ni bora kwa wale walionacho haina uzalendo, watoto hawa ndiyo miaka 50 au 100 ijayo watauza nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Bunge hili kwani lina mamlaka na utukufu wa Bunge hili ukiwa ni

utukufu kwelikweli, ikiondokana na mambo ya rushwa na vishawishi vingine vyote tukaisimamia Serikali vizuri na tukajitathmini sisi wenyewe vizuri, basi Taifa hili litapata mwelekeo mpya, tutapata Kiswahili ambacho tutakitumia vizuri na Kiswahili kimejaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 1977 nilisoma Kanuni ya Tatu ya Isaac Newton inayosema: "Katika kila Kani mkabala kuna kani iliyo mrejeo sawa na kinyume." kwa Kiingereza wanasema: *"To every action there is an equal and opposite reaction"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Kiswahili kina misamiati ya kutosha, katika kila kani mkabala kuna kani iliyo mrejeo sawa na kinyume. Mwaka 1977 nilikuwa darasa la tano, ni zaidi ya miaka 35 iliyopita bado tunaimba wimbo ule ule na tunazidi kurudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna mahali tumekwenda kando kidogo, tumekosa maono yaliyo dhahiri kwa kuweka Utaifa wetu mbele, kwa kuweka Utanzania wetu mbele na kwa kuacha na haya mambo mengine mengine yote, tuhakikishe kwamba Mama yetu Tanzania tunayemlilia, sisi sote tutamuenzi Tanzania, Tanzania patakuwa ni mahali pazuri, Kiswahili kitatumika vizuri katika Bunge la Afrika, Bunge la Jamhuri ya Muungano na Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Baba yangu Samuel Sitta, Afrika Mashariki kwenye Bunge tutumie

Kiswahili ndiyo maana ya hii *protocol*. Tusiruhusu wengine wakachukua cha kwetu, halafu tukabaki tulalamika tu, tunalalamika tu, hapana, tufanye matendo leo na siyo kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia muda huu.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbatia kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo ajiandae na Mheshimiwa Eugene Mwaiposa pia ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia kidogo kwenye itifaki ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwenda moja kwa moja na kwanza nimshukuru Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuleta itifaki hii hapa Bungeni japokuwa imekuja ikiwa imechelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi, kwenye *article number 28* inaonekana kwamba, hii itifaki imesainiwa tarehe 13 Septemba, 2008, kwa hiyo, mpaka leo ni miaka mitano. Kwanza walioweka saini hapa ni nchi tatu tu yaani Tanzania, Kenya na Uganda wakati huo nadhani Rwanda na Burundi walikuwa hawajaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kujua, Wizara na Serikali ituambie leo kwamba sasa hivi inakwenda

kutekelezwa kwenye nchi tatu au inakwenda kutekelezwa kwenye nchi zote ambazo zipo kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki? Kama inakwenda kutekelezwa kwenye nchi zote ni kwa nini basi wenyewe hatujawaona hapa wameweka saini kukubaliana na itifaki hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo hapo kwenye hiyo hiyo *Article number 28*, imechukua miaka mitano hii itifaki ikiwa ndani ya Serikali, sisi tumeiona leo kama Wabunge, lakini ndani ya Serikali ina miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua ndani ya hiyo miaka mitano kama Taifa na kama Tanzania tumejiandaa vipi kwenda kunufaika na fursa ambazo zipo ndani ya itifaki hii? Kwa sababu tumeambiwa zipo faida kadhaa nyingi ambazo tumeambiwa kwenye itifaki nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa miaka yote hiyo sasa, wamefanya uchunguzi wa kutosha na udadisi wa kutosha ili kujua fursa zilizopo. Kama Taifa miaka yote mitano tumejiandaa vipi sasa au tunasubiri tuingie kwenye itifaki wenzetu waje watupiku waweze kuchangamkia fursa ndiyo sisi tuanze kuona kwamba tumeachwa nyuma? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kujua kwamba kama Taifa tumeandaa vipi shule zetu kuanzia *Primary School, Secondary School*, vyuo vyetu kuanzia *Certificate, Diploma Level* mpaka vyuo vikuu, tumejiandaa vipi kutoa wataalam wa kutosha, lakini pia wenye uwezo mkubwa wa kuweza kuingia kwenye soko la ushindani wa ajira? Kama

Taifa tumewaandaa vipi mpaka hapa tunapozungumza sasa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna mifano mingi ya jinsi gani ambavyo Watanzania tunajulikana kama tunaongea Kiswahili ambayo ni lugha ya Taifa letu. Lakini kutokana na kwamba tumebaki nyuma, wenzetu wametupiku kwenye mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwa mfano, kwenye suala la utalii, hoteli nyingi za Tanzania zinachukuliwa na Wakenya yaani zinaongozwa na Wakenya na wenzetu Wakenya na Uganda wanabebana sana. Akipata Meneja ukakuta wahudumu karibu wote wa hoteli wanakwenda kuwachukua kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kujua kwamba, tunapoingia kwenye hii itifaki tumejiandaa vipi? Kwa sababu nina wasiwasi kwamba, sisi ni wazungumzaji wazuri wa Kiswahili na tumeona kwa jinsi gani ambavyo wanaopata fursa za kufundisha hata kwenye shule za *academy au English Medium au shule za International School* za Tanzania wengi ni wa kutoka nje japokuwa tuna Walimu wengi ambao wanazungumza Kiswahili kizuri lakini hawatumiki na hatuchangamkii hizo fursa kwa sababu ya udhaifu wetu kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tupate ufafanuzi kwamba, tumejiandaa vipi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaweza kunufaika na manufaa yaliyopo kwenye hii itifaki nzima.



Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kujua kwenye *article number 28* ambayo inasema kwamba, *Executive Secretary* atakaa kwa muda wa miaka mitano na kuna uwezekano wa ku-*renew*, ina maana ni miaka mitano tena mingine. Sasa najiuliza mtu tuko watano, kama tupo watano au watatu halafu nchi moja ipate fursa labda ya kuongoza miaka kumi yaani kuongoza ile Kamisheni miaka kumi, ina maana nchi nyingine ambazo zitakuwa wasindikizaji labda miaka 50 hawajawahi kuongoza ile Kamisheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza ni kwa nini tusifanye miaka mitatu au kama ni miaka mitano kusiwepo na uwezekano wa ku-*renew* ili kila nchi ipate fursa ya kuweza kuongoza ile Kamisheni. Hilo ni pendekezo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la mwisho ni kwamba tumekuwa tunaona ndani ya nchi yetu pamoja na kuwa hata sisi wakubwa tunaboronga kwenye Kiswahili, lakini lipo tatizo kubwa kuanzia misingi ya watoto wetu, kuanzia huku chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunashuhudia watoto wetu wanakuwa na lafudhi za Kiingereza kwenye Kiswahili wanachokizungumza, kuanzia watoto wa miaka minne au mitano. Unakuta mtoto anazungumza lafudhi ambayo *the way* anavyoizungumza hiyo lafudhi anaweka Kiingereza ndani yake.....

**MWENYEKITI:** Tumia Kiswahili Mheshimiwa Mbunge.  
(*Kicheko*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba, watoto wetu kuanzia ngazi za chini kidogo hata miaka minne au mitano wanazungumza Kiswahili ambacho kina lafudhi ya Kingereza ndani yake lakini wazazi tunaona na tunaacha, walezi tunaona na tunaacha na hata Walimu wanaona na wanaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unakuta mtoto anasema, '*Daddy unajua, you know*', ni mtoto mdogo, anakuwa katika ile hali, anazungumza Kiswahili, lakini anachanganya ndani yake na Kiingereza hata ile unajua, wajua eeh, wajua! Huyo ni mtoto mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kama Taifa tuanze kulikemea kuanzia chini, kwa nini tumuache mtoto huyu mdogo wa miaka mitano au sita anakuwa na ile *spirit* au lafudhi mpaka anakua. Kwa hiyo, matokeo yake anakuja kuwa mkubwa kama tulivyo sisi watu wazima tunaboronga Kiingereza na Kiswahili ambacho ni lugha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni kwamba, kama Taifa nina wasiwasi kama fursa zilizopo ndani ya itifaki hii tutanufaika nazo. Nina wasiwasi! Ninachoomba kwa kweli Serikali ijipange ije na mikakati na elimu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie, tangu mwaka juzi au mwaka jana ndiyo angalau Watanzania wengi tumeanza kufahamu nini Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni kwa sababu gani? Elimu sasa hivi imeanza kwenda mpaka vijijini na imesogea sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nilivyoingia Bungeni hapa sikujua kabisa nini maana ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu ilikuwa haitangazwi na elimu haitolewi vijijini na hata mijini elimu ilikuwa haitolewi au ilikuwa inatolewa kwa kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wachache waliokuwa wanajua, lakini sasa hivi kutokana na kwamba elimu imetolewa mara kwa mara kwenye vyombo mbalimbali na matangazo mengi yametolewa, tumeweza kuelewa kwa upana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda pia na hii Kamisheni, elimu itolewe vya kutosha na kuwepo na mikakati ya kufika hadi ngazi ya chini kabisa ili kila Mtanzania ajue kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha yake na kwamba kuna Kamisheni ambayo inashughulikia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, angalau kama Taifa tutaweza kunufaika na fursa hizo na kuhakikisha kwamba sisi kama Watanzania na lugha yetu ni Kiswahili inaweza kufahamika na kuweza kuwanufaisha Watanzania badala ya kuwa wasindikaji kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ahsante kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa ajiandae na pia Mheshimiwa Maryam Msabaha ajiandae, Mheshimiwa Janeth Mbene na mwisho Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa John Shibuda wajiandae.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia na mimi lile azimio lililoletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna tofauti baina ya kusema na kutenda. Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili Tanzania ni jambo ambalo limesemewa zamani katika vyombo vya kutunga Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niseme kwamba, watungaji wa Kamusi za Kiswahili itawabidi waende chini zaidi katika kutafuta lahaja za kuweza kutafsiri lugha ya Kiswahili. Nasema hivyo kwa nini? Watungaji wa Kamusi za Kiswahili walipotumia neno simika kama ni sehemu ya kusimamisha, nasema kwamba walikosea na si tafsiri sahihi ya lugha ya Kiswahili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kuna kichongeo cha penseli, hapa wamezidisha lugha ambayo kuisema, maana yake wamekiita Kifirio, kweli hii ni lugha ya Kiswahili? Ni kitu cha kukipa chombo ambacho kinatumika katika jamii? Hatuwezi tukasema kama hiki ni kichongea penseli tu? (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kifulio!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Hatuwezi tukasema kama hiki ni kifulio cha penseli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kwamba, tunacheka lakini lugha ya Kiswahili tunaitafsiri katika lugha ambayo siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niafiki uanzishaji wa Kamisheni hii, niafiki uanzishaji wa Kamisheni hii na niseme kwamba tuna wajibu wa kuisoma, kuifahamu na kuisomesha kinyume na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa Tanzania tumeifanya lugha ya Kiswahili kwamba si elimu ambayo inaweza ikampa mtu ajira. Lakini tuangalie vijana wetu wana sanaa imewaajiri kwa kiasi kikubwa, kwa nini Serikali haijaipa kipaumbele miaka yote mpaka inatoa kipaumbele leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niseme kwamba, kuanzishwa kwa Kamisheni hii kutasaidia Tanzania kuondoa mianya ambayo walikuwa wakiitumia nchi za wenzetu katika kutukosesha ajira kwenye taasisi zinazomilikiwa na Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini vile vile, hatupaswi kamwe kujidharau, kuna wale ambao wanaamini katika masikio yao na mawazo yao kwamba eti Kiswahili ni

Kikongo, hebu tujiulize Kongo ina watu asilimia ngapi waliotumia Kiswahili?

**MJUMBE FULANI:** Wengine wanasema Kiarabu!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Wengine wanasema Kiswahili ni lugha ya Kiarabu, sasa mimi niseme kwamba Kiswahili kwa kweli ni mchanganyiko wa lugha ambao umeweza kuzaa lugha ambayo ni nzuri na ina ladha hata katika kuitamka kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, niseme kwamba, kupewa umuhimu wa kuwekewa Makao Makuu ya Kamisheni hii kuwa Tanzania ni suala la kujipongeza. Kwanza ni kuona kwamba, hizo nchi ambazo wao wanatoa wataalam wa kwenda kusomesha kwingine, lakini wanajua kwamba Walimu wa lugha ya Kiswahili basi ni Watanzania. Lakini kwa sababu ya kuidharau kwetu, kwa sababu ya kutoitilia maanani na kwa sababu ya kutojiendeleza...

**MJUMBE FULANI:** Kuithamini!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Na kwa sababu ya kutoithamini, wenzetu wanachukua nafasi ya kwenda kusomesha nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunawapongeza Wakenya na Waganda kwa kuchukua nafasi ya kwenda kusomesha lugha ya Kiswahili katika Mataifa mengine, ni kwa sababu wamejiendeleza na nina uhakika waliowaendeleza ni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu hapa wamekaa Tanzania wamesoma, wamesomeshwa, wameifahamu lugha na wamekwenda nchi nyingine kuchukua nafasi za urais. Wapo ninawajua kwani wamelelewa hapahapa Tanzania lakini sisi wenyewe tumeipuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Kamisheni hii itumie muda wake mkubwa katika kupopotoa lahaja na istilahi za Kiswahili. Wapopotoe maneno ya lahaja na istilahi za Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya sehemu za Visiwani Zanzibar ukisema tembo ni matusi, watu waelewe kwamba mnapokwenda sehemu fulani ukitamka neno fulani ni tusi na vile vile kwa Zanzibar ukisema amesimika basi ni matusi, tena Zanzibar yote.

**MJUMBE FULANI:** Kwa hakika!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Na neno la kifiria ni Tanzania nzima ni matusi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kama wengine ni wachafuzi wa lugha, ni wachafuzi wa lugha ya Kiswahili na siku hizi kumeingia lugha za Wamalenga wanaitwa Wamalenga wa Mamboleo. Mimi nasema wale ni wachafuzi wa lugha.

Kuna mshairi mmoja alisema washairi wa kileo si washairi kathani, washairi wa kileo si washairi kathani, mashairi ya kileo si mashairi kathani, wayaita mamboleo lakini mtihani, hayana vibwagizo wala hayana mizani, haya si mashairi. Sasa ni kukivuruga Kiswahili! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokiomba ni kwamba, Kamisheni hii isimamie lugha ya Kiswahili ili lugha itamkwe ilivyo sahihi. Mimi napendekeza kwamba kifirio kiitwe kifilio. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo kwa utalaam wako wa lugha. Naomba sasa kumwita Mheshimwa Eugen E. Mwaiposa na Mheshimiwa Maryam S. Msabaha pia ajiandae.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nashukuru kwa kupata nafasi na mimi niweze kuchangia. Nitachangia kwa ufupi sana kwa sababu mengi yamekwishachangiwa na wasemaji wengi ambao wametangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali, kwa kuleta kwa wakati Itifaki ya Tume ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki. Kama ambavyo wamesema wengine ni kweli tumechelewa, lakini pamoja na kuchelewa kwetu nilitaka tu kuongea mambo matatu ya msingi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuhusu fursa ambazo zitatokana na Tume hii. Fursa ya ajira inaonekana kama ndiyo ya kwanza ambayo Watanzania wataifaidi, lakini lipo jambo la msingi la Watanzania kuweza kujua fursa hizi zitapatikana kwa njia ipi.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi naweza kusema hawana utamaduni wa kutafuta fursa na kuzikimbilia. Kama tutaendelea na mfumo au tabia hii ni wazi tutakuta ajira zimechukuliwa na hizi nchi nyingine ambazo tuko pamoja nazo katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Nawaomba sana Watanzania, kwa kutumia Bunge hili, wajifunze kutafuta fursa na kuzikimbilia ili ziweze kuwa mkombozi wa ajira katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mwaka jana nilikwenda katika Mkutano wa Umoja wa Afrika (AU), uliofanyika Addis Ababa. Nilipata fursa pia ya kuongea na Wafanyakazi wengi Watanzania ambao wako Ethiopia. Wengi wao wapo katika Mashirika mbalimbali ya Kimataifa, lakini la msingi walilokuwa wanasikitika ni uwezo wa Watanzania kuomba kazi katika mashirika mbalimbali ya nje. Walikuwa wanasema kwamba, hakuna Mtanzania anayejitokeza kuomba kazi katika mashirika mbalimbali kwa sababu ya kutokujiamini kwao. Pia wanasema zilitokea nafasi mbalimbali, kulikuwepo na nafasi moja tu ambayo ilikuwa ni lazima ijazwe na Mtanzania, nafasi ile ilitangazwa kama mara tatu ndipo alipoweza kupatikana Mtanzania wa kuijaza. Kwa hiyo, hii inaonesha kabisa kwamba, Watanzania hatuna utamaduni wa kuzikimbilia zile fursa ambazo zinatolewa katika mashirika mbalimbali ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nilifikiria kwamba tatizo kubwa ni la lugha. Tunatangaza kwamba Tanzania tunatumia Lugha ya Kiswahili na Lugha ya Kiingereza, lakini katika uhalisia Watanzania walio wengi *either* hawajui kabisa hata hicho Kiswahili, lakini pia hawajui Kiingereza.

Tuko hapa katikati, ukimwambia aongee kwa Kiingereza hawezi kuzungumza moja kwa moja Kiingereza kizuri, lakini pia ukimwambia zungumza kwa Kiswahili kama unavyotuona wengi hata hapa Bungeni ni kwamba, hatuwezi hata tukazungumza hicho Kiswahili kwa ufasaha na kwa muda mrefu bila kuchanganya changanya maneno mengine ya Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni tatizo. Tunahitaji kuhakikisha kwamba tunajifunza lugha yetu vizuri kama wenzetu Wakenya ambavyo wameweza kujifunza Kiswahili fasaha. Hii itapatikana tu kama kweli nchi pamoja na Watanzania, wana nia ya dhati ya kukikuza Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe tu kwamba, kama kweli Serikali ina nia ya dhati ya kukikuza Kiswahili kutoka Tanzania, basi tuanze sasa kuzungumza kwa Kiswahili katika majukwaa ya nchi za nje na hii ianze kwa Viongozi wetu wanapokwenda nje wazungumze kwa Kiswahili. Hata Watanzania wengine ambao wapo katika nafasi mbalimbali za Kiserikali, wasikie fahari kuzungumza Kiswahili kwa sababu wapo watu wenye taaluma ya kutafsiri Kiswahili kwa hao wengine ambao hawakijui vizuri.

Kwa kufanya hivyo, sisi wenyewe tutakuwa tumeandaa utaratibu wa kuziwezesha ajira za Kiswahili kuwepo duniani, lakini kama hatutakizungumza katika mikutano na majukwaa mbalimbali nje ya nchi, basi maana yake ni kwamba, hata ajira za kutafsiri Kiswahili, tunakuwa tunazitokomeza au kuziondoa bila ya sisi wenyewe kufahamu. Kwa hiyo, naomba tuanze sasa kuzungumza kwa Kiswahili katika majukwaa na tuanze na Viongozi wetu wanapokwenda katika semina au mikutano mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe sana hasa Tanzania, pamoja na nchi nyingine, tuanze pia utaratibu wa kutumia Balozi zetu kwa ajili ya kufundisha Kiswahili sehemu wanazozifanyia kazi. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa na watu wengi sana wanaozungumza Kiswahili katika dunia hii ambayo sasa pia itakuwa njia mojawapo ya kukikuza Kiswahili katika ulimwengu wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo machache sana ambayo nilikuwa nataka niyazungumze na nashukuru pia kwa kupata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, kwa mchango wako. Namwita Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Suzan Lyimo na Mheshimiwa Ali Juma wajiandae.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kupata fursa ya kuchangia Muswada huu ambao uko mbele yetu.

**MBUNGE FULANI:** Azimio.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Azimio la Afrika Mashariki kuhusu masuala ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina sikitiko langu kubwa sana; tunaposema Soko la Afrika Mashariki ni pamoja na sisi Watanzania kupata ajira za walimu wetu kwenda

kufundisha Lugha ya Kiswahili, lakini unakuta nafasi hizi zinaporwa na wenzetu wa Kenya, Uganda na nchi nyingine ambazo ni za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda Marekani unakuta Wakenya wametuzidi hata katika kufundisha Kiswahili pale Marekani. Kuna ushahidi tosha, kuna mtoto wa Mheshimiwa ambaye alikuwa Waziri wetu wa Fedha, Mheshimiwa Mustapha Mkulo, kulikuwa na Wakenya ambao walikuwa wanafundisha Kiswahili lakini yule mtoto akawa anafundisha Kiswahili pia, wakawa wanasema hiki siyo Kiswahili, Kiswahili fasaha ni kile cha Kenya. Mpaka Mheshimiwa Asha-Rose Migiro akaingilia kati akasema Kiswahili cha Tanzania ndiyo Kiswahili fasaha, lakini Kiswahili cha Kenya siyo Kiswahili fasaha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo hii unakuta sisi Watanzania tunashindwa hata kuchangamkia zile fursa za Kiswahili ambazo ni nafasi za Watanzania, tunaacha zinaporwa na wenzetu wa Afrika Mashariki. Hili tuliangalie kwa umakini kabisa. Ukienda kwenye hoteli za kitalii leo unakuta Wakenya ni wengi, Watanzania walio wengi wanaishia kufanya kazi za kutandika vitanda, kufagia na kudeki. Sasa zile nafasi zetu wanachukua Wakenya na wanawatafutia sababu makusudi kabisa hata kama kuna Watanzania pale wanaojua vizuri kabisa, lakini wanafanya mizengwe fulani fulani unakuta Wakenya wanatuzidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mzee wangu, Mheshimiwa Sitta, aliangalie suala hili kwa umakini hasa katika hizi Sekta za Ajira katika Afrika Mashariki. Tuangalie kwa umakini na tujiulize tunaingia kwenye masuala haya lakini Watanzania tumejipanga vipi? Unakuta leo hii hapa tuna nafasi zinatokea za Walimu kwenda kufundisha Rwanda, Uganda, lakini zile nafasi hawazipati. Kwa nini unakuta nafasi zile hawazipati?

Ni kwa sababu zinachukuliwa na Wakenya, sisi Watanzania tunakuwa tuko wapi? Tunajikuta kwenye Kiswahili hatupo, kwenye Kiingereza hatupo, tunaelea katikati kama mchangiaji aliyetangulia alivyosema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tujiangalie tumejipanga vipi; hawa Walimu tunao wa kutosha katika shule zetu? Tuangalie watoto wengi leo wanaanza chekechea lakini hawafundishwi Kiswahili. Anaanza kufundishwa Kiingereza kuanzia akiwa mdogo mpaka anakuwa mtu mzima, kwa hiyo, unakuta yule mtoto anakuwa mtumwa katika nchi yake, hajui Kiswahili, hajui Kiingereza vizuri. Sasa tunakwenda wapi? Kama sheria inapitishwa basi ipitishwe na ianzie shuleni tunakofundishwa lugha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, BAKITA wamejitihadi sana katika kipindi chao cha Jumamosi, wamekuwa wakirusha vipindi vya kwa ajili ya kufafanua mambo ya Kiswahili. Watanzania walivyo wasikivu, wengi sana wamekuwa wakipiga simu Radio One wanaulizia hili suala liko vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanze sisi hapa hata Miswada mingi ije kwa Kiswahili na tuitafakari kwa Kiswahili basi tutapata jibu, lakini leo hii utakuta wengine tunapiga

makofi tu hatujui hata kilichopitishwa mle ndani ni kitu gani, baadaye kinakuja kutuletea matatizo sisi wenyewe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia kwenye Halmashauri nyingi, Madiwani wengi hawajui Kiingereza, unakuta Miswada ile inapitishwa kwenye halmashauri na inaisababishia Serikali hasara kubwa. Hili tuliangalie kwa umakini na lugha yetu tuipende, hakuna nchi ambayo inaendelea kwa lugha ya kuiga. Leo mkiangalia Korea wameendelea kwa lugha yao. Ukienda Ujerumani wameendelea kwa kuipenda lugha yao. Ukienda Japani wanaendelea kwa kuipenda lugha yao. Kwa nini sisi Watanzania hatuipendi Lugha yetu ya Kiswahili tunaiga lugha za watu mpaka mavazi tunajikuta tunaiga na kupenda ya nje kuliko ya hapa nyumbani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni machache tu, lakini naomba Kiswahili hasa katika Soko la Afrika Mashariki na Miswada ambayo inajadiliwa katika Bunge la Afrika Mashariki pia ipitishwe kwa Kiswahili, kwani sisi tukiwa na paa katika Kiswahili tutakuwa tumesonga mbele na tutakuwa tumeitangaza lugha yetu na watoto wetu watakuwa wamejitambua wako wapi na hata nafasi zetu tutakuwa tunajitambua tuko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unakuta hata wanawake wengi wanadhulumiwa katika mirathi kwa sababu

Miswaada na Sheria zinakuwa zinapitishwa kwa Kiingereza. Sasa unakuta mtu pale ana haki lakini anashindwa kabisa kuuliza haki yangu iko wapi. Unakuta mtu anafungwa pasipokuwa na sababu kwa kutokujua kile ambacho kimeandikwa mle ndani.

Kama kingekuwa kimeandikwa kwa Kiswahili labda angeweza kujitetea mwenyewe akajua hii ni haki yangu ambayo ninaidai; lakini unakuta mtu yule anahukumwa kwa jambo ambalo halijui kwa sababu hukumu ile imetolewa kwa Kiingereza na Watanzania wengi na hasa walio pembezoni hawajasoma Kiingereza, wamesoma hii hii Lugha ya Taifa.

Nitoe mfano tu; mabango mengi pale Dar es Salaam utakuta yameandikwa kwa Lugha ya Kiingereza. Sasa mtu anatoka pembezoni mwa nchi anakuja Dar es Salaam anatafuta chuo, anakipita mara tatu, mara nne, hajui kile chuo kiko wapi kwa sababu bango limeandikwa kwa Lugha ya Kiingereza. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa nini tusiwe wazalendo tukaipenda lugha yetu ya Kiswahili, matangazo yetu ya vyuo tukaandika kwa Kiswahili, matangazo ya biashara tukaandika kwa Kiswahili, kama wenzetu wa Korea wanavyofanya? Kwa sababu Korea ukienda dukani kama hujui Kikorea huwezi kuuziwa kitu mpaka uwe na mkalimani. Leo hii ukienda Ujerumani kama hujui Kijerumani huwezi kupata ajira mpaka ujue Kijerumani. Kwa nini sasa tusipende angalau tukabaki kwenye Kiswahili? Tubaki kwenye Kiswahili na tuseme wakati Mawaziri

mnasafiri kwenda huko nje, Rais anasafiri kwenda kwenye mikutano, waweke kipaumbele kwenye Kiswahili, waseme na sisi tunataka tuzungumze kwa Kiswahili katika mikutano hii na Watanzania watatuelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie na mikataba ambayo tunaingia na wawekezaji ipo katika Lugha ya Kiingereza. Sasa wengi hawajui, hata hao ambao wapo migodini, ambao ndiyo wamiliki wa ardhi yenye migodi lakini hawajui. Unakuta tu mtu umeajiriwa pale, hujui sheria, mikataba yote imekuja kwa Kiingereza, wewe unajikuta unafanya kazi unakuwa mtumwa katika nchi yako. Hili naomba mlifanyie kazi na lipate ufumbuzi, tukibaki kwenye Kiswahili tujue tumebaki kwenye Kiswahili, na tukibaki kwenye Kiingereza basi tujue tumebaki kwenye Kiingereza, siyo tunachanganya lugha mbili hatujui tuko kwenye Kiingereza au kwenye Kiswahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, naomba tuangalie zinapotokea nafasi za kwenda kufundisha Kiswahili kama ni Uganda, Kenya au wapi, tuhakikishe wanapata hawa Watanzania ambao wana sifa ya Kiswahili. Najua Kiswahili kipo na hawa walimu kila siku wanahangaika lakini wengine hawajui waanzie wapi. Naomba mtangaze kwa makini kabisa na zichangamkiwe na Watanzania ambao wana fursa waende kusoma huko, kujifunza na kuwafundisha wengine. Najua tukisema sasa Kiswahili tumekipa kipaumbele, tutafanikiwa kwa mambo



mengi, tutapata maendeleo bila kuiga lugha za wenzetu na bila kuwa watumwa kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Maryam. Sasa namwita Mheshimiwa John Shibuda, Mbunge wa Maswa.

**MHE. JOHN M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwa dhamira ya kutoa maangalizo, mahimizo na kutoa vidahizo vyenye dhamira ya kung'arisha matarajio ya Kamisheni hii kuwa ya tija kwa maslahi ya Watanzania. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusesitiza ya kwamba, kuanzishwa kwa Itifaki hii ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ni mchakato wa dhamira njema kwa ustawi na maendeleo yetu. Tanzania tunaweza kuwa chemchemi ya kuhakikisha kwamba Afrika inatuiga kwa fahamu za maneno fasaha. Kamisheni hii ningeomba iende sambamba na uanzilishi wa tunzo kwa waasisi wetu kama Shaaban Robert, walioasisi lugha fasaha na sanifu kwa maslahi ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzo hizo zitakuwa kichocheo kwa maslahi ya ustawi na maendeleo ya Kiswahili. Wakale husema "Bundi hawezi kuvaa Njiwa", vivyo hivyo hakuna anayeweza akawa chemchemi ya Kiswahili murua katika Afrika kama siyo Watanzania. Tuache visingizio vya ulimi na utelezi pale unapomkuta mtu anazungumza Kiswahili huku

anachanganya na Kiingereza, kujinasibu na kujitambulisha ya kwamba, ustaarabu ni kujua Kiingereza na uungwana ni Lugha ya Kiswahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanze kuwa na mifano ya kuacha kutumia vidahizo vya Kiingereza unapozungumza Kiswahili; hivyo basi, ukafanya ya kwamba Bunge hili au semina au Mihimili ya Serikali ili ujing'arishe ya kwamba unazungumza maneno fasaha lazima uweke vidahizo.

Viarifu hivyo ni najisi kwa Lugha ya Kiswahili na ni najisi kwa watu hasa makini ambao wamebobeza kwa tabia na desturi za udhu katika mustakabali wa Lugha ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunaweza kuanza kusambaza Lugha ya Kiswahili pamoja na majukumu ya Kiswahili. Pamoja na majukumu ya wajibu wa Itifaki ya Kamisheni lakini naomba kusema ya kwamba, Bunge hili la Tanzania tujiulize sisi tutakuwa wadau na wabia wa njia ipi ya kuendeleza Lugha ya Kiswahili; hivyo Bunge hili na Wabunge tuwe mfano wa kuigwa na Bunge la Kenya, Uganda na Mabunge mengine katika nchi ya Afrika ya Mashariki? (*Makofi*)

Tujihoji, tujigundue, tujidadisi, tuhakikishe kwamba tunakuwa na mnyumbuliko wa fikra ili tuweze kuhakikisha ya kwamba Kiswahili tunaking'arisha sisi wenyewe kuanzia hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea maneno yanayoongelewa na wataalam na wasomi wetu. Tujiulize hivi ni fumbo la kwamba tuna upungufu wa kujua Lugha ya

Taifa? Unamkuta msomi kwenye semina ili aweze kujieleza vizuri katika ajenda anayozungumza anatafuta vidahizo vya Kiingereza. Ukinyumbulisha mantiki ya maneno yale na Kiswahili, unakuta kwamba viarifu na viota vya maneno hayo haviko sambamba katika mustakabali wa Lugha ya Kiswahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta kuna neon, kwa mfano, posho, malipo ya posho ya kujikimu, sijui utakuta anazungumzia posho ya mazingira magumu, lakini Kiswahili posho ni malipo ya vibaba. Kwa nini wewe usizungumze tu malipo ya ujira wa mwiha? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli za maneno hujenga utulivu wa fikra na kuondosha ghasia na ghadhabu kwa wale wanaosikiliza. Kwa nguvu sana unapozungumza posho fulani inaweza ikajenga ghadhabu kwa sababu, kwa mfano wa posho za mazingira magumu ungesema malipo ya mwiha, inajenga kwamba hapa mtu anajengewa utulivu wa fikra. Kwa hiyo, malipo ya ujira wa mwiha ni malipo ya kujenga utulivu wa fikra kwa taaluma, mwanataaluma na mtu mwenye majukumu ambaye mara kwa mara anakuwa na mtafaruku wa mahimizo ya kuombwaombwa misaada mbalimbali. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno fasaha huondoa viota ambavyo vina ghadhabu kwa wasikilizaji. Mti ukikosa mbolea na ukakosa maji hupukutika. Kwa hiyo, basi ili na sisi tafakari zetu za Kiswahili tuziondolee uchokonozi wa kinungunungu ni muhimu tukajitambua je, maneno

unayotaka kuyaumba yatakuwa na utaarifu wa ujumbe upi ambao unajenga ufasaha wa kuthaminika Lugha ya Taifa? (*Makofi*)

**MJUMBE FULANI:** Pambanua.

**MHE. JOHN M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utasikia vijana wa siku hizi wanasema: "Huyo mzee ni soo, lakini siyo noma, sasa tumfanyie dili huyo mzee kazidi kuwa bahiri." Mwenzake anaitikia, "sawa, mambo poa, mshikaji." Sasa hicho Kiswahili cha wapi? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utakuta kwamba, hivi sasa Kiswahili cha nchi yetu, kizazi kipya wanajaribu kukivuruga. Utasikia, "Demu huyu alishwe mtama ili pochi yake bukinaa tumeshapona." Sasa bukinaa tumeshapona maana yake nini? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipingi haki za ujana, japo kale wakale walisema ya kwamba, asiyefunzwa na mzazi hufunzwa na dunia na akaambiwa ujana ni giza nene la msitu ambao usipong'arishwa mtoto umleavyo basi anaweza akawa na tabia za ajabu. Vijana wetu kwa nini wanakuwa na kauli na lugha za ajabu? Sababu ni moja kwamba, sisi wenyewe walezi na wazazi nyumbani tukijitambulisha ya kwamba wewe ni mtu mstaarabu na mwendelevu, *Hallow my baby! Hallow son!* Maana yake nini na wewe ni Msukuma mwanone mulemola ng'wanone, maneno gani hayo? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Kwa hiyo, naomba majumbani wazazi tubadilike, tuwang'arisha watoto wetu kupenda Lugha ya Taifa. Hilo kama tutalifanya nina uhakika tutasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki, sasa hivi Tanzania tupo katika janga la tabia nchi ya usanii wa malezi wa mapokeo ya tabia za kutoka nchi za nje.

Mtu akienda kusoma Ujerumani basi Wajerumani wameshapata mtwana wa kuleta mapokeo ya tabia za Ujerumani. Sasa ubepari wa hulka na silika tusipouondosha watoto wetu tunaowazaa watakuwa hawana ujasiri wa uzalendo, uaminifu na utiifu kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wa dhamana mbalimbali ndiyo sisi ambao tunazorotesha na kutorosha thamani ya Kiswahili. Mazalia ya vitungwa hivyo kwa Kiswahili cha machukizo ni sisi. Mapokeo ya uboi wa utwana wa fikra na kutumia Kiswahili na Kiingereza ni sisi. Viongozi ndiyo viaga uaminifu kwa Lugha ya Kiswahili. Wazazi wanoitwa waendelevu ndiyo viaga uaminifu kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii tutaipeleka wapi kama sisi wenyewe tutashindwa kujisahihisha? Wakale husema mbwa akipaliwa nyama ya pilipili hubweka hovyoo. Utakuta ya kwamba, watoto siku hizi wanasema, "Aah, umemwona yule mzee, mzee wetu mwezi sana lakini mambo poa." Tunawafundisha nini watoto wetu? Kwa nini hatukemei?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupongeza mashairi ya taarabu, taarabu asilia, yaani si chakacha; taarabu asilia na umakini wa taarifu za mashairi, vionjo vyake ni kisomo cha fasaha ya kisomo cha kuelimisha na kutambulisha kama si kukosoa. Chakacha ni somo la sononeka mwanana au msemu wa burudani inayochokonoa, sasa anatoa mchokonoo basi akachokoneke na aliyechokoneka aumie, aliyepata faradhi afurahie na kushangilia. Tunakwenda wapi? Chakacha ni vua milonge mvishe janga huyo aliyekuchokonoa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi nawaomba tuachane na vimbwanga vya kauli vitungo vya Kiswahili na Kiingereza. Hifadhi ya adaui ujinga kutambua vyema Lugha ya Kiswahili na kuchanganya Kiingereza wewe unajinasibu hujui Kiswahili na hujui Lugha ya Taifa. Napongeza wazo la hoja ya kuwepo Kamisheni hii na natoa wito tuwe na watu makini na tuwe Watanzania wa kuigwa na Afrika Mashariki. Kamisheni hii ipanue wajibu wake, hivyo basi iweze kuwa na shabaha na malengo ya kukuza lugha licha ya kwamba ina jukumu la Itifaki za Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu ya kujitambulisha kuwa ni waungwana kwa sababu unajua kiingereza, naomba kuitoa hofu hiyo. Ungwana ni kauli na vitendo vya busara na hekima. Kujua Kiingereza lakini matendo yako ya mtu mzima hovyoy, hayajengi hata kidogo. Kwa hiyo, napenda kushawishi sisi Wabunge basi tuwe watu wa kuhabarisha kwa lugha fasaha na redio na vyombo vingine vya habari vipindi vyake vihakikishe wanakuwa wabia wa kuendeleza Lugha ya Kitaifa Tanzania, kiwe kivutio cha soko la Watanzania kuajiriwa mahali pengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manyambua ya fikra na mawazo yetu yawe na ustawi wa lengo la kuhakikisha kwamba, Lugha ya Taifa kila tunapozungumza tunaenzi Lugha ya Kiswahili kwa sababu ni Lugha ya Taifa. Savaa yoyote inayotendwa maana yake ni kwamba, Kunguru hafugiki hata ukimlisha ubwabwa wa pilau. Ombwe la maana ya lengo la fikra laweza kuwa na azma njema. Kwa mfano, leo asubuhi tumetumia neno kauli ambayo haistahiki. Unapozungumzia uchi ni tafsiri ya lugha ambayo inazungumzia viwiliwili vya binadamu, ni kauli faragha.

Unapotamka neno uchi ni kauli faragha, lakini ukiitumia bayana basi unatengua usawa wa utulivu wa fikra za mtu mstaarabu ambaye ana maono ya kutambulisha ya kwamba huko tuendako ni giza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa John Shibuda, kwa umahiri katika Lugha ya Kiswahili. Sasa namwita Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Juma Ali Juma, tutamalizia na Mheshimiwa Janet Mbene na baadaye mtoa hoja atahitimisha.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika Azimio na Itifaki kuhusu Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimefarijika sana kuona Wabunge wote wameunga mkono. Ningeshangaa sana kumwona Mbunge ambaye haungi mkono kwa

sababu tunatambua kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya ukombozi, ndiyo lugha ambayo imelipatia Taifa hili Uhuru, kwa maana hiyo sisi kama Watanzania tunapaswa kukienzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nianze kwa kuhoji maswali kadhaa kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni kweli kwamba, tunaona waliosaini Itifaki hii ni pamoja na Mawaziri watatu wa nchi waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, yaani Kenya, Uganda na Tanzania, nikitambua kuwa kwa wakati ule Burundi na Rwanda walikuwa hawajajiunga. Sasa nilipenda tu kujua katika nchi hizi tano je, Mabunge mangapi yamesharidhia Itifaki hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu tunaona pamoja na kwamba wamesaini mwaka 2008 mpaka leo ndiyo sisi tunasaini. Kwa hiyo, tumechelewa wakati sisi Tanzania ndiyo nchi pekee ambayo tunaweza kusema kwamba kwa kweli Kiswahili kimeanza kwetu na ni Watanzania wengi au wote wanaongea Lugha ya Kiswahili; kwa hiyo, tulitakiwa tuchangamkie fursa hii mapema sana ili Kamisheni hii iwe imeshaanza. *(Makofi)*

Vilevile niipongeze pia Serikali kwa kuhakikisha kwamba, Kituo cha Kamisheni hii kinakuwa Tanzania na hususan kule Zanzibar. Pamoja na mambo mengine, vilevile itaweza kuhakikisha kwamba tunapata ajira zaidi kwa Watanzania. Pamoja na kupitisha au kukubaliana na itifaki hii, tunairidhia; kuridhia ni kitu kimoja, lakini utekelezaji ni jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa nchi ambayo inaridhia mambo mengi au tunakuwa na mipango mingi mizuri, lakini hatuitekelezi, matokeo yake nchi nyingine



wanaiga kutoka kwetu na wanatekeleza na mifano ipo wazi. Kwa hiyo, naomba tunaporidhia jambo muhimu kama hili ambalo lina maslahi makubwa sana kwetu kama Watanzania, lakini kwetu kama Wanajumuiya ya Afrika Mashariki, ni vyema basi kuwe na utashi wa kisiasa ili tuweze kuhakikisha kwamba utekelezaji unafanywa kwa wakati ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yameongelewa mambo mengi kuhusiana na Lugha ya Kiswahili kwamba Viongozi hasa tunapokwenda nchi za nje, tuongee kwa Kiswahili. Niliweke wazi kwamba ni kweli Watanzania tunakipenda Kiswahili na tungependenda sana hata tunapokwenda nje tuongee Lugha ya Kiswahili, lakini ni wazi kwamba, tuna tatizo kubwa sana la wakalimani wa Kiswahili katika Makongamano ya Kimataifa. Mfano mzuri ni kwenye mikutano ya *IPU* ya *UN*, hakuna Wakalimani wa Kiswahili. Kwa hiyo, hata kama Mtanzania utapenda sana kuongea kwa Kiswahili bado hutaweza kuongea kwa sababu tu hakuna wakalimani, jambo ambalo linashangaza sana. Vilevile siku hizi kuna nchi pamoja na kwamba hawana Wakalimani wa Kimataifa, wanachokifanya wanaenda na wakalimani kutoka nchini mwao, kwa hiyo yule mkalimani anatafsiri halafu wale wengine wanatafsiri ile lugha kwa Kiingereza au kwa lugha nyingine.

Kwa hiyo ni mategemeo yangu kwamba, siku za usoni katika mikutano mikubwa wanaweza wakapelekwa

wakalimani, Serikali itawalipia ili Watanzania wanaoenda katika mikutano hiyo waweze kuongea kwa ukamilifu. Kwa sababu ni kweli kama walivyosema wenzangu, tumekuwa na tatizo kubwa la lugha kwamba Kiswahili hatukijui vizuri, lakini na Kiingereza vilevile hatukijui vizuri, jambo ambalo linaleta aibu kwa Taifa hasa tunapokwenda katika mikutano nje ya nchi. Kwa hiyo ni vyema Serikali ilianganalie hili ili iweze kuwasaidia wale ambao wanashiriki katika mikutano mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mategemeo yangu kwamba, sisi kama Bunge, kama Taasisi, ni vyema tukawa mfano tukaanza kuongea Kiswahili sanifu siyo tu ndani ya Bunge hata nje ya Bunge kwenye mikutano ya kawaida. Jambo la kushangaza unakuta Wabunge kwenye mikutano ya hadhara wanaongea na watu ambao hawajui kabisa Lugha ya Kiingereza, lakini utakuta wanachanganya na Kiingereza, jambo ambalo wapiga kura hawalipendi sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sisi tuwe chachu. Vilevile Mabunge mengine yote ya Afrika Mashariki likiwemo na Bunge la Afrika Mashariki; nazungumzia Mabunge ndani ya nchi husika, yaani Bunge la Rwanda, Burundi, Kenya na Uganda, wazungumze pia Kiswahili kwa sababu naamini kabisa tukiangalia katika mikutano ya hadhara sasa hivi kuna kampeni kubwa za uchaguzi nchini Kenya wanaongea kwa Kiswahili, lakini ndani ya Bunge hawaongei Kiswahili. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki yuko hapa ni vyema basi waweze kuhamasisha Mawaziri wenzao watumie Lugha ya Kiswahili katika

Mabunge yao ili tuweze kuhakikisha Kiswahili kinapata Hadhi ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini najiuliza; pamoja na kwamba Kiswahili kinaongelewa na watu wengi ni kwa nini hatuna wakalimani katika mikutano na hilo nimekuwa najiuliza mara kwa mara? Kama alivyosema Mheshimiwa Mkuchika ni kwamba, Watanzania hatujawa na ujasiri au hatuko *aggressive* kama wenzetu wa Kenya; wamekuwa wanaongea Kiswahili kibovu, lakini unaona mahali pote ukienda wao ndiyo wanaongea Kiswahili na ndiyo walimu.

Ukienda Korea kwenye Vyuu Vikuu, Wakenya ndiyo wanafundisha Kiswahili wakati Maprofesa wetu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wapo tu wanadodea pale; kwa nini Tanzania kama nchi haipeleki wataalamu wake? Kwa nini hawawatafutii masoko wakati wana vyombo vyote vya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamisheni hii itasaidia sana kuwapatia ajira Walimu wa Kiswahili. Kubwa zaidi, itafute soko la ajira kwa Watanzania kwa sababu naamini Kiswahili sahihi kipo Tanzania, Kiswahili sanifu kipo Tanzania. Kwa hiyo, naomba sana wajitahidi, lakini pamoja na hilo nilikuwa naangalia pia bajeti. Ni vizuri kama nilivyosema, utashi wa kisiasa ni muhimu sana na utashi huu utapelekea pia kuwa na bajeti ya kutosha ili Kamisheni hii iweze kufanya kazi hasa ukizingatia iko ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni kwamba tukiwa na hii Kamisheni watu wataweza kutuandikia vitabu, kwa hiyo, tutakuwa na

waandishi wengi wa vitabu. Nizungumze kwamba, Kiswahili kama walivyosema wenzangu, kimekuwa kikiharibiwa sana na wenzetu. Kwa mfano, unakuta watu wanashindwa kutafsiri Kiswahili vizuri kwa sababu tu lugha hiyo hawajazaliwa nayo. Naomba hii ni fursa pekee ambayo Watanzania tumeipata lazima tuichangamkie ili tuweze kufaidika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo kwa mchango wako. Namwita Mheshimiwa Ali Juma Haji na Mheshimiwa Janet Mbene ajiandae. Mheshimiwa Ali Juma Haji hayupo, basi naomba Mheshimiwa Janet uendelee na hatimaye mtoa hoja aje ahitimishe.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba niwaunge mkono walioleta hoja hii hapa Bungeni na kusema kuwa pamoja na kwamba inaweza kuwa imechelewa, lakini kwa kweli ni itifaki muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Kwanza, nataka kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuwa, itifaki hii imeletwa kwetu sisi ili kwanza tuikubali, lakini vilevile tuitolee maoni yetu, jinsi gani ifanye kazi vile ambavyo tumeitegemea. Kwa maana hiyo, tutoe mapendekezo ya jinsi ya kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakuzwa, lakini vilevile tutoe mapendekezo juu ya jinsi gani ya kuisimamia itifaki hii ili ifanye kazi yake sawa sawa, kwa maana ya kutoa mafunzo, kusambaza na vilevile kutumia Kiswahili kwa ufasaha zaidi na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge katika kujiepusha zaidi na kulaumu wakati wote na kuona sisi Watanzania hatujafanya hiki, hatujafanya kile, kuna mambo mengi tumeyafanya hasa katika lugha; kwa hiyo, tukubali kuwa kuna upungufu lakini pia kuna mambo mazuri tuliyoyafanya na kufuatana na itifaki hii tunaweza tukajenga juu ya msingi uliopo kuboresha itifaki yetu. Nafikiri tufike mahali tuanze kuenzi vitu ambavyo tumevifanya vizuri, tusiwe tunafikiria kama sisi ni watu ambao hatujafanya chochote na kila siku tunalaumiana tu. Kama Wabunge, itifaki hii imeletwa kwetu tutoe mawazo, maoni na mapendekezo ya jinsi ya kuitumia na kuiboresha. Nafikiri hayo ndiyo yatatusaidia zaidi katika kuhakikisha itifaki hii tutakapoipitisha jioni ya leo au kesho itakuwa imefanya kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukumbusha tu kuwa, lugha ni kitu ambacho kinakua na kinakua polepole. Hata mkifikiria lugha ambazo zinajulikana kuwa zimeendelea sana sasa hivi tukianza na Kiingereza, Kiingereza mpaka leo bado kinakua na Kiingereza kiko kwenye soko au kiko kwenye jamii miaka mingapi ukilinganisha na Kiswahili chetu. Kwa hiyo, tuangalie jinsi gani tutaendeleza mifumo ya kuboresha Kiswahili kama Lugha ya Taifa na Lugha ya Afrika na mwisho Lugha ya Dunia nzima badala ya kuendelea tu kukashfiana na kuona kuwa hatuitumii vizuri au hatuijui. Lugha hii inakua polepole, turekebishe pale ambapo tunaitumia vibaya ili tusije tukaambukiza watoto wetu na vizazi vijavyo na wao kutumia lugha vibaya. Ni jukumu letu sisi wote kuhakikisha lugha hii inaboreshwa na

inatumika. Kwa kweli inapendeza mkiwa na lugha yenu wenyewe mnaitumia sehemu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupendekeza kuwa, itifaki hii ieleze jinsi gani tutakavyoiboresha kwa maana ya kuwa kuwe na mpango mkakati wa jinsi gani itakavyoendelezwa hadi itakapofikia mahali ambapo tutasema sasa tuna Lugha ya Kiswahili inatumika dunia nzima. Baada ya hapo ndiyo tuangalie sasa tunawajengea uwezo vipi wananchi, vijana wetu na jinsi ya kutumia zile fursa ambazo zinatokana na lugha hii, pamoja na kujifunza lugha nyingine. Nina hakika vilevile kama sitakuwa nakosea kuzungumza kwa niaba ya Serikali, kwa sababu najua aliyeleta mada yuko mbele yangu hapa kuwa, Serikali kwa kuleta Azimio hili la Itifaki hii, wana dhamira kuhakikisha kuwa Kiswahili kitaboreshwa na kusambazwa duniani pote, kwa kupitia mapendekezo yaliyotolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge. Nchi za jirani ni kweli wanaweza kuwa na Wataalamu wengi wa Kiswahili hata na lugha nyingine, lakini huo ni ulinganishwaji tu, kuna mambo mengine hata sisi tunaweza kuwa tumewazidi.

Kiswahili kinatumika zaidi na Wakenya au kinafundishwa zaidi nchi za nje na Wakenya, ni kwa sababu pengine kufuatana na kuwa hata kwa takwimu za kielimu wao wana vyuo vingi kuliko vya Tanzania na kwa uwiano huo huo utakuta wanatoa wataalamu wengi zaidi wa lugha kuliko sisi, lakini hiyo haituzuii sisi sasa hivi kuweka mkakati wa makusudi kuhakikisha kuwa kitengo chetu cha lugha kinaanza kuimarishwa zaidi kutokana na fursa hii ambayo imejitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge tufahamu kuwa kuna masuala mengi yaliyojificha katika masuala haya ya ajira kati ya nchi zetu hizi za Afrika Mashariki hata nchi za Afrika. Tunapozungumzia kuwa watu wengi wa Kenya wanafanya kazi Tanzania, lakini sisi Watanzania hatuendi Kenya, Rwanda na kadhalika, tukumbuke kuwa kuna masuala mengine yamejificha. Wenzetu wanaweza kuwa siyo wepesi sana kuwapokea Watanzania kufanya kazi kwao kama ambavyo sisi tunawapokea wa kwao.

Hili ni jambo ambalo linatakiwa lifanyiwe kazi katika *Protocol* ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Suala hili lisilaumiwe kwenye lugha, ni suala la *Protocol* nzima ya Afrika Mashariki. Ni kweli kuna haja ya kuwa na uwiano kati ya Watanzania wanaoenda kufanya kazi nchi nyingine za Afrika Mashariki kama ambavyo wa nchi nyingi za Afrika Mashariki wanavyokuja kufanya kazi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na fursa kuwa hazitangazwi au watu hawaambiwi, ningependa kukumbusha kuwa, fursa nyingi za ajira huwa zinatangazwa na wanaohitaji wanaajiriwa. Ni jukumu letu kama alivyosema Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga na M-NEC kuwa, sisi Watanzania tujenge utamaduni wa sisi wenyewe kuwa wadadisi wa mambo wa kutambua kuna fursa wapi ili tuzifuate fursa hizo na kuzitumia. Haiwezekani kuitegemea Serikali ndiyo ianze

kusema Shirika fulani au nchi fulani imetangaza kazi ya Walimu jamani jitokezeni. Kila mtu ana wajibu na mwenye shida ya hiyo ajira kuitafuta. Kwa hiyo, tujaribu kwa kiasi kikubwa na sisi wenyewe kujenga utamaduni wa kutafuta taarifa. Serikali ikipata kwa kupitia mifumo ya Kiserikali, kwa vyovyote vile lazima itatangaza kama ambavyo inatangaza fursa nyingi za ajira na fursa nyingine zinazojitokeza zinapitia katika mfumo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa kuwa naamini mambo mengi sana yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, napenda kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuwa, hili ni jukumu letu wote kuhakikisha kuwa lugha yetu ya Kiswahili, kwanza, tunaitukuza, tunaikuza, tunaiboresha, tunaisambaza na tunasimamia matumizi yake kwa ukamilifu, isiwe ni jukumu la Serikali peke yake bali ni sisi wote. Mapendekezo yaliyotolewa hapa ninayaunga mkono kwa sababu yatatusaidia kujaribu kurudi nyuma na kutafakari kama hii lugha kweli tunaikuza jinsi ambavyo inapaswa.

Kwa hiyo ni jukumu letu sisi sote, hakuna kunyoosheana vidole wala kulaumiana bali sote tusimame kwa pamoja. Nimefurahi sana leo kuona Kambi zote tunakubali kuunga mkono hii Itifaki kuonesha kuwa tuna umoja huo katika kusimamia lugha yetu. Basi kwa mwendo huo huo, tuendeleo katika kuhakikisha kuwa lugha hii inakua, fursa zilizojitokeza tunatumia wote kwa ajili ya watoto wetu na vizazi vijavyo na sisi sote tunakuwa wamoja katika kuisimamia lugha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.



**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Janet Mbene, kwa mchango wako na ufafanuzi wako. Kabla sijamwita mtoa hoja, kwanza, napenda kuwataka radhi sana wale wote ambao walikuwa wameomba kuchangia, lakini kutokana na ufinyu wa muda haikuwezekana. Naamini mtakuwa mmechangia kwa maandishi.

Baada ya kusema hivyo, napenda kumwita Mheshimiwa Amos Gabriel Makala, Naibu Waziri, kwa ajili ya majumuisho. Mheshimiwa Karibu.

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawapongeza Waziri na Naibu wake, kwa kuleta Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili ni Lugha ya pekee Afika, yenye maneno mengi ya asili yetu ya Kibantu. Pia imeteuliwa kuwa Lugha ya Afrika, kwa kuwa Tanzania bado ni Mwanachama wa Jumuiya za Nchi za *SADC* na lugha zinazotumika kule ni Kiingereza, Kireno na Kifaransa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lugha hii inazungumzwa na nchi nyingi Barani Afrika hasa kwa wale ambao pia walikuwa katika harakati za kudai Uhuru. Je, ni kwa nini sasa

Tanzania isiongeze juhudi ya kuzishawishi Nchi za *SADC* kukikubali Kiswahili kuwa mojawapo ya Lugha zake rasmi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi watakaopata fursa ya kueneza Kiswahili nchi mbalimbali walindwe kimaslahi na kiusalama na pia wafundishwe masuala ya kiusalama kwa faida ya nchi.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili kimeanzia kwetu na ni Lugha ya Kitaifa, kifundishwe kuanzia Shule za Msingi hadi Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu sana la kuridhia Itifaki; hivyo, Mihimili yetu yote ikiwemo Mahakama na Bunge vitumie Kiswahili.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ieleze sababu za Itifaki hii ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki kuchelewa kuletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa tangu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais wa wakati huo, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, aliposaini tarehe 13 Septemba, 2008. Ni muhimu Serikali ikaweka mfumo wa Bunge kupewa taarifa katika Mkutano wa Bunge unaofuatia, baada ya Serikali kusaini Mkataba wowote wa Kimataifa. Hata kama Serikali itakuwa na sababu za msingi za kuvuta muda kabla ya kuwasilisha Bungeni Mkataba au Itafaki iweze kuridhiwa, Bungeni na Wabunge, watakuwa na nafasi ya kuishauri na kuisimamia Serikali katika wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuridhiwa kwa Itifaki hii kuwe chachu ya kufanya maboresho ya Kisera, Kisheria na Kitaasisi kuhusu ukuaji wa Lugha ya Kiswahili hususan kuwa na mfumo wa kuhakikisha Kiswahili kama Lugha ya Taifa kinatumiwa, ikiwemo katika Mihimili muhimu ya Dola, yaani Bunge na Mahakama katika utungaji wa sheria na uandikaji wa hukumu katika ngazi zote. Aidha, mapitio (*review*) ifanyike katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa kuweka suala la uendelezaji wa Lugha ya Kiswahili kama sehemu ya mambo ya msingi katika ukuzaji wa utamaduni. Katika mpango wa mwaka wa Serikali utakaowasilishwa kwenye mkutano wa kumi mwezi Februari 2013, Serikali iweke maendeleo ya Kiswahili kama sehemu ya masuala ya kipaumbele.

Serikali itambue kwamba, Lugha ya Kiswahili ni kati ya bidhaa na huduma ambazo nchi yetu inaweza kuuza nje na kuliongezea Taifa pato la kigeni. Bidhaa na huduma hizo ni pamoja na walimu, utafiti, machapisho na mazao mengine ya Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, Tanzania iwe kipaumbele katika kuhakikisha Ibara ya 119(2)(d) na 37 za Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki inatekelezwa. Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, wawasilishe Muswada binafsi wa Sheria kuwezesha matakwa na masharti hayo kuwekewa mfumo thabiti wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kiswahili kuanza kutumika kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Nchi za Afrika (AU) ni muhimu sasa ushawishi ukafanyika kuwezesha matumizi kama hayo katika Umoja wa Mataifa (UN). Kamisheni hii ifanye pia ukuzaji wa Kiswahili Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika Mashariki inakabiliwa na ushindani wa Kimataifa Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii. Katika mazingira ya ushindani huo, yapo Mataifa yenye malengo ya kuendeleza ukoloni mamboleo na ubeberu wa kiuchumi na kijamii. Ubeberu na ukoloni huo unajipenyeza pia kupitia tamaduni za kigeni, lugha ni nyenzo katika kufikia malengo yao. Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki iwe ni chombo cha kulinda na kuendeleza maslahi ya Afrika kiutamaduni, ikiwemo kusimamia umajinuni wa Kiafrika.

Jitihada za Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ikiwemo ya kutengeneza Kamusi za Kiswahili kwenda lugha mbalimbali za kwenye simu ya mkononi ziendelezwe ili Watanzania wengi wawe na njia rahisi ya wananchi kuwa na kamusi kama sehemu ya uendelezaji wa lugha. Wizara ieleze ni kwa kiwango gani imesaidia mradi huo kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono wazo la kuwa na Programu Maalum ya Muda Mfupi ya Kufundisha Walimu wa Kiswahili. Hata hivyo ni muhimu walimu hao wafundishwe lugha zingine hususan Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kijerumani, Kihindi, Kihispania, Kireno na Kichina. Hii itawezesha kujipenyeza katika nchi zote zinazoshindana

kiuchumi Duniani ambazo zipo katika makundi matatu; Nchi za Ulaya, Nchi za Amerika na nchi zinazoendelea kwa kasi kiuchumi (BRICS - Brazil, Urusi, India na Urusi). Aidha, Kamisheni hii ishirikiane na Taasisi nyingine kuhusu lugha kuu nyingine za Afrika ili lugha hizo kubwa mathalani Lugha ya Kifaransa, walimu wa lugha ya Kiswahili wawepo kwenye ujuzi pia wa lugha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati wa mpango huo, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje na Mahusiano ya Kimataifa ili kuwahusisha Watanzania waishio nje (*Diaspora*), katika kuwafanya baadhi yao kuwa walimu katika nchi ambazo wanaishi au wanafanya kazi. Haya yatawezekana iwapo bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, itaongeza kiwango cha fedha kwenye mwaka wa fedha wa 2013/2014 katika uendelezaji wa Kiswahili.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kauli ya masikitiko, nasikitika kwa sababu Itifaki ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ilitiwa saini tarehe 13 Septemba, 2008, lakini imechukuwa miaka minne Bunge letu la Tanzania kuridhia Itifaki hiyo! Hii ni ishara ya utashi mdogo wa kisiasa wa Serikali yetu kuhusiana na suala la lugha yetu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kauli hiyo, ninapenda sasa nijielekeze kwenye Itifaki yenyewe.

Napenda kuanza kwa kusema kwamba, uanzishwaji wa Tume au Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ni

hatua muhimu katika maendeleo ya Kiswahili na umuhimu wake unalingana kwa kiasi fulani na hatua ya kuanzishwa kwa Taasisi au Idara za Kiswahili zinazofundisha Isimu na Fasihi katika Vyuo Vikuu mbalimbali Afrika Mashariki. Lugha ya kufundishia katika Taasisi au Idara za Kiswahili ni Kiswahili chenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ina madhumuni thabiti kuhusiana na ukuzaji, uenezaji, usimamizi wa mitaala na uandaaji wa vifaa vya kufundishia na pia usimamizi na uelekezi wa asasi zilizo chini ya Tume (Mabaraza, Taasisi na zinginezo). Madhumuni ya Itifaki yako wazi kuhusiana na dhima ya Tume kwenye ngazi ya Kitaifa, Jumuiya na Kimataifa. Tume itakuwa Mshauri Mkuu wa Jumuiya kuhusiana na masuala yote yahusuyo Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya madhumuni kuwa wazi na thabiti lakini yana ufinyu unaotokana na upungufu ulio katika Mkataba ulioanzisha Afrika Mashariki mwaka 1999. Katika Mkataba huo, fungu 137, Kiswahili kinachukuliwa kuwa ni *lingua franca* tu na Kiingereza ndiyo lugha rasmi ya Jumuiya. Jambo hili nalisema hapa ili Tume ikianza kazi ilichukulie kuwa ni changamoto na iandae mipango au mikakati ili hatimaye Kiswahili kiweze kupandishwa hadhi na kuwa lugha rasmi ngazi zote husika. Changamoto nyingine ambayo inatokana na ufinyu wa madhumuni ulio katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Afrika Mashariki (1999) ni suala la Kiswahili kuwa lugha ya

kufundishia ngazi zote za elimu. Kihistoria, Tanzania ndiyo ilikuwa na fursa nzuri ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia ngazi zote za elimu, lakini Serikali iliacha fursa hiyo ikapita na sasa hivi Kiingereza ndicho kinachoshabikiwa. Hii ni changamoto muhimu ambayo Tume itabidi kuishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napeda kumalizia kwa kutaja changamoto kuu ambayo inawahusu Viongozi wetu wa Kisiasa. Toka nchi za Afrika zipate Uhuru, Viongozi wengi wa Kisiasa (ukiondoa wachache), bado wametawaliwa na kasumba ya kikoloni ya kukihusudu Kiingereza na kutokithamini Kiswahili ikiwa ni lugha yetu ya Taifa na Kikanda. Ninapenda kusema kuwa, pamoja na madhumuni mazuri ya Itifaki, kama Viongozi wetu wa Kisiasa hawatakuwa na utashi wa dhati wa kisiasa na kuisimamia, basi Tume haitafanikiwa katika madhumuni yake mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninapenda kusema kuwa ninaunga mkono Azimio la Kuridhia Itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono uanzishwaji wa Itifaki ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kasi ya Uanzishwaji wa Itifaki hii iharakishwe zaidi.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa siku ya leo kwa kunijalia afya na uzima kuchangia hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa kuletwa mbele yetu Itifaki ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki, ingawa imechelewa, tunashukuru sana imefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya kuanzishwa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri baada ya kuridhia, Tanzania tujitahidi kuboresha ufundishaji wa lugha ya Kiswahili, kwani Watanzania wengi wanaongea Kiswahili, lugha ambayo inatuunganisha, lakini Kiswahili cha kuandika ni tatizo kwa Watanzania wengi. Hata Kiswahili tunachoongea ni mchanganyiko wa maneno ya lugha nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama lugha ya Kiswahili itaenea katika Kanda hii ya Afrika Mashariki, basi itatupa fursa Watanzania kupata ajira, biashara na kuunganisha Kanda hii yetu ya Afrika Mashariki kilugha na kutoa fursa kwa wanaoleta bidhaa zao Afrika Mashariki kuleta vielelezo kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa nyingi sasa zina vielelezo vya Kiswahili na inarahisisha Watanzania kusoma vielelelezo katika bidhaa bila tatizo. Kwa mfano, katika



madawa ya binadamu na mifugo, vyakula, bidhaa za *kielektroniki*, leo hii hata *Google* inatafsiri kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru muda wa kuboresha Kiswahili umewadia na kukieneza kwa kanda yetu ya Afrika Mashariki na baadaye Afrika na duniani kote. Tunashauri pia Kamisheni hii iendelee na kusimamia Kiswahili fasaha kwa kuandika na kuongea.

Ahsante. Naomba kuunga mkono tena.

**MHE. SUSAN A. L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na azimio hili kuchelewa sana kuletwa Bungeni na kwa leo tunalipitisha na kuridhia hapa Bungeni ni muhimu iwekwe kwenye sheria mama ili kufanya lugha ya Kiswahili ipate nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili kama lugha nyingine, kikifanyiwa kazi vizuri kitaongeza ajira kwa Watanzania wengi ambao kwa miaka mingi kimeonekana kama siyo bidhaa kwa wageni wanaokuja na waliopo nchini mwao.

Hivyo kuwepo na mpango wa makusudi kuandaa wanafunzi na walimu wa Kiswahili na kuwatafutia ajira ndani na nje ya nchi ili kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo tutakitangaza Kiswahili katika matangazo ya ndani na ya nchi kwa bidhaa/vivutio vilivyopo nchini, tulazimishe na tuongeze nguvu katika kukikomaza Kiswahili na kitumike kwa nguvu, na hii itafanya watoto kuwa wadadisi na wagunduzi kwa kutumia Kiswahili na kuwafanya Watanzania kukipenda, kukithamini na kujivunia Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kukitumia Kiswahili kwa wawekezaji kuwa kivutio kama ilivyo kuwekeza kwenye madini, misitu, maeneo yote ya uwekezaji kama sehemu ya lazima. La sivyo, kama hujui Kiswahili, hakuna uwekezaji eneo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ione haja ya kuanzisha madarasa ya Kiswahili ndani kwa kila mgeni anayeingia nchini kwa nia ya kuishi, kuwekeza au katika Balozi zetu. Hii itasaidia kukuza Kiswahili na kuongeza ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili ni lugha tamu na inapendwa sana, lakini sisi ambao ni waasisi wa Kiswahili hatukithamini. Kwa kuchelewa huko, lazima tuweke mkazo. Haiwezekani tukionee aibu Kiswahili chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuletwa itifaki hapa Bungeni ni jambo moja na kuitekeleza ni jambo linguine. Je, Serikali imejiandaa vipi kiutekelezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukuza Kiswahili, tukazie ufaulu wa wanafunzi uwekewe katika somo la Kiswahili na kuwepo na tuzo kwa walimu wa Kiswahili na wanafunzi wanaofanya vizuri ili kukuza Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili ni tunu ya Taifa, tuwe na mpango maalum wa miaka mitano mitano na tujipime, tupaze sauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kiswahili kufundishwa Darasa la Awali hadi la Saba na baada ya hapo shule zetu kuanzia Darasa la Tisa, masomo hufundishwa kwa Kiingereza, tunaharibu elimu yetu na kulivuruga Taifa. Tubadili haraka mitaala yetu, Kiswahili iwe lugha ya kufundishia Awali hadi Elimu ya Juu na Kiingereza na lugha nyingine za nje ziwe na masomo kama yalivyo mengine.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa uwasilishaji wake. Pia naunga mkono hoja na kushauri kuweka msisitizo na kutokibeza na ni vema kuacha kutumia maneno ya lugha ya kigeni wakati wa mijadala ya Kiswahili. Pili, mikutano yote inayoendesha ikiwa ni pamoja na warsha hapa nchini zinazogusa wazawa, Kiswahili kitumike bila kuchanganya na lugha zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mikutano ya Kimataifa, Kiswahili kitumike na kuwepo kwa Wakalimani ili kukipa heshima zaidi na nchi nyingine zivutike na kujifunza Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi zinahitajika katika utunzi wa vitabu mbalimbali na tafsiri za vitabu vingi ili kukuza Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Serikali ikaandaa sera ya kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wananchi ili waweze kuchangia katika sera hiyo na pia kuifanikisha na kuwa sheria ambayo itakuwa ndio mwongozo wa kukuza, kueneza na kuhifadhi lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali kutaka kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili, Serikali katika kuandaa sera ya lugha hii isisahau kwamba, kwa sasa yaani katika wakati huu tuliopo yaani ni dunia ya sayansi na teknolojia. Tupo kwenye zama ya utandawazi, hivyo ni vyema pia Serikali ikaangalia ni vipi hata lugha zingine zikapewa umuhimu, kwani kwa sasa dunia ni kama Kijiji. Hivyo, ni vyema lugha zingine zisipuuzwe kwani ni muhimu katika dunia ya sasa hivi, kwa mfano, lugha ya Kiingereza, Kichina, Kifaransa na hata Kihispaniola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio la kuridhia Itifaki ya uanzishwaji wa Kamisheni ya Afrika Mashariki kwa kuwa Azimio hili lina faida kubwa sana kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamisheni hii iwapo itatumika vizuri kwa Watanzania tutapata faida zifuatazo:-

Kwanza, kiuchumi; uchumi wetu utaboreka kwa kupata soko la vitabu vya Kiswahili na wataalam na kupata ajira kwa vijana wetu wenye utaalam wa Kiswahili.

Pili, kiutamaduni; kukuza na kuendeleza na kuienzi lugha yetu ya Kiswahili iliyotuletea uhuru.

Tatu, kijamii; Kiswahili kitapanua wigo wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, Serikali itoe msukumo kwa Taasisi za Kiswahili kupata fursa za kupeleka wataalam wa Kiswahili nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa kuwa Tanzania sidhani kama tuliweza kupeleka Walimu nchini Gabon, nchi ambayo ilihitaji Walimu wengi wa Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa hii kuchangia hoja hii ya uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Mashariki mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmojawapo wa Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii ambao tumepitisha Azimio hili na kuomba liridhiwe na Bunge hili Tukufu. Pamoja na mapendekezo na maoni yaliyotolewa, ningepomba mambo yafuatayo yaangaliwe kwa ukaribu sana:-

(1) Je, mpaka leo hii Tanzania tuna idadi ya wataalam wangapi ambao sasa watakuwa mstari wa mbele kuanzisha wigo huu?

(2) Je, mpaka leo hii tunao wataalam wangapi ambao wanafanya kazi nje ya nchi ya kufundisha Kiswahili?

(3) Je, mpaka sasa tuna chombo gani kinachowaleta pamoja wataalam hawa kwa pamoja na kuwa na chombo cha kusimamia shughuli zao?

(4) Je, mpaka sasa ni juhudi zipi zimefanywa za kuwaleta wataalam hawa na kuwakutanisha na wataalam wetu wa ndani ili kukuza misingi ya Kiswahili?

(5) Mwisho, ni utayari gani tumeuandaa kulinda heshima na mvuto wa lugha hii kwa kuliandalia shirikisho hili mazingira bora kwa maana ya kuliwezesha shirikisho kufanya kazi yake vizuri sana? Mfano bajeti ya uendeshaji shirikisho, Ofisi iko wapi ambapo shirikisho watafanyia kazi na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza yote haya, naomba kuunga mkono hoja na shirikisho hili sasa likuze Kiswahili ili sasa tuweze kuwa na wigo mkubwa wa utumiaji wa lugha hii. Shirikisho lihakikishe lugha hii inafundishwa hata katika Mabara ya Amerika, Ulaya na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nasisitiza na natilia mkazo uwepo katika mitaala ya vyuo vyetu au kuwepo na vyeti maalum vya ufaulu kwa ngazi mbalimbali kulingana na uhitaji wa soko.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ningependa kuona Kiswahili kama lugha ya Taifa kiwe ndiyo lugha rasmi ya kufundishia katika ngazi zote za elimu nchini kwetu. Nasema haya kwa sababu Tanzania ni nchi huru, hivyo basi lugha yetu ya Taifa Kiswahili ikiwa kama lugha rahisi inayoeleweka kwa Watanzania wote

itarahisisha vijana wetu kuelewa vizuri bila kutumia nguvu tofauti na sasa ambapo Kiswahili kinatumika kana kwamba hatuna shida nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama shida ni upungufu wa misamiati isiwe tatizo, hata Kiingereza kinachopendelewa kina baadhi ya maneno yamekopwa kuliko kukiua Kiswahili na sisi pia ni bora kukopa ili tuweze kutumia lugha yetu ambayo binafsi naamini ni lugha bora zaidi. Hivyo namwomba Waziri aseme lini lugha ya Kiswahili itatumika katika ngazi zote za elimu nchini kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuona Bunge letu Tukufu linakuwa mstari wa mbele katika kukuza na kukitukuza Kiswahili hasa katika kutekeleza majukumu yake hususani kuletwa kwa Miswada na Sheria zote za nchi hii ikiwemo mikataba yote ya nchi hii iwe katika lugha ya Kiswahili ili kutoa fursa kwa Watanzania walio wengi waweze kufuatilia na hata kuchangia kwa ufanisi bila shaka juu ya mambo muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, itakuwa vizuri kama Waziri ataeleza wazi hapa Bungeni ni lini Waziri ataleta Azimio la kutaka shughuli zote Bungeni zifanywe kwa lugha ya Kiswahili ikiwemo uletwaji wa Miswada na uchambuzi wa Sheria mbalimbali za nchi yetu ikiwa ni pamoja na mikataba yote ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili kiwe chachu ya kuleta haki na usawa katika chombo chetu cha kutafsiri sheria na kutoa haki yaani Mahakama. Hii ni kwa sababu Kiingereza kinaonekana kutawala hasa katika hukumu licha

ya kwamba, wahukumiwa wengi hawajui Kiingereza hali inayopelekea wahukumiwa wengi kutojua nini kinaendelea wakati wa hukumu na hivyo kukosa haki yao ya kujua ukweli juu ya kesi yake kwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini iweje kuwa Taifa huru kama Tanzania ambapo kuna lugha ya Taifa Kiswahili tuamue kutumia Kiingereza ambacho Watanzania wengi hawakijui kwenye ngazi muhimu ya haki kama Mahakama. Hii ni aibu kwa Taifa. Kwa hiyo, Waziri aseme wazi aibu hii tutaikwepa lini na Kiswahili Mahakamani kitatumika lini ikiwa ni pamoja na kuzitafsiri sheria ziwe kwa Kiswahili ili kuwapa fursa Watanzania kujua sheria zao kwa lugha yao halisi ya Kiswahili.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara ya Habari kwa maono yao ya kuanzishwa kwa Tume ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imechelewa sana kulingana na mahitaji yaliyopo, naishauri Serikali imaanishe katika hili kwani ni kitu muhimu sana kwa ustawi wa Taifa letu, Kimataifa lakini pia kwa ustawi wa jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna eneo ambalo ni kero kubwa kwa ajili ya matumizi ya lugha ya Kiingereza ni Mahakamani, wengi wamepoteza haki zao kwa kutojua lugha hiyo.

Naiomba Serikali irekebishe maeneo yote ambayo yamekuwa kero kwa matumizi ya Kiingereza. Mahakamani Kiswahili kitumike, matangazo ya kazi yawe ni kwa Kiswahili, waombaji wa kazi wasailiwe kwa Kiswahili.



Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi za Kimataifa (*English Medium School*) ziondolewe masomo ya Kiingereza yafundishwe kwa Kiswahili, Kiingereza kifundishwe kama somo tu sio somo la kufundishia masomo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tujijenge vema kiuchumi, Watanzania na Taasisi zote muhimu zianze kutumia Kiswahili katika Nyanja zote, Miswada Bungeni iletwe kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma ili mtu atambulike ama kupewa cheti cha kufaulu kidato cha nne ilikuwa ni lazima ufaulu Kiswahili na Siasa, hivi sasa hilo halipo bali somo la hisabati ndilo limepewa hadhi. Napendekeza hilo la ufaulu wa Kiswahili kama kigezo cha kupatiwa cheti cha kufaulu kidato cha nne lirudishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote ambayo yanaonekana kama kusonga mbele basi yapewe uwezo ama kujengewa mazingira ya kukiendeleza Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Naibu Waziri kwa kuleta Azimio hili muhimu na ambalo limechelewa, lilitakiwa kuja mapema, napongeza hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kutumia Kiswahili lakini nina tatizo na hiki Kiswahili kigumu kinachotumiwa kila siku chenye misamiati ambayo Mswahili wa kawaida anashindwa kuelewa. Hadi maneno mengine yanayobuniwa huwa ni matusi katika makabila mengi. Kiswahili kilichokuwepo ni kizuri, kinaeleweka labda maneno mapya yatokane na teknolojia mpya kama *blogs*, lakini pawe na mafunzo maalum ambayo yatajumuisha wananchi walio wengi. Niombe tu tuache Kiswahili kiwe kinaeleweka na wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafarijika sana kuwa Tanzania imeteuliwa kuwa Makao Makuu ya Kamisheni. Pamoja na heshima hiyo, napenda kuuliza tumejiandaaje kibajeti kukidhi jukumu hilo? Utashangaa hata fedha za kuendesha kituo hicho kionekane na sura ya Afrika Mashariki hazitapatikana. Aidha, miundombinu na wataalamu stahiki utaambiwa hakuna fedha. Nasema kwa uzoefu kwani mambo mengi mazuri, makubwa, yanaanzishwa hapa nchini kwetu ila yanaishia hewani, kama tuna nia ya dhati tumejiandaaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, hapa tunatetea hilo, kwa vijijini naelewa linatekelezeka, je, kwa mijini na kwa watu wa ngazi ya kati kwenda juu na sisi humu ndani, tuna nia ya dhati kwa hilo? Jamaa zetu, watoto wetu, fikra zetu ziendane na Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linawezekana wote tukiamini hivyo na kutimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuleta Bungeni Azimio la Itifaki ya Uanzishaji wa Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri yafuatayo:-

- (i) Taasisi za Kiswahili nchini ziongeze jitihada za kukuza Kiswahili hapa nchini ili sisi ambao ndio waasisi wa Kiswahili tuwe mfano;
- (ii) Kwa sasa Kiswahili kinazidi kumomonyoka hivyo basi kama nchi tukishindwa kudhibiti hali hiyo basi Kiswahili fasaha kitapotea na nchi zingine kupuuza lugha yetu. BAKITA wawezeshwe zaidi kutoa elimu ya Kiswahili fasaha na waendeleo kukosoa pale ambapo lugha ya Kiswahili inapomomonyoka;
- (iii) Kama nchi ni vema mifumo yetu ya elimu hapa nchini ibadilike toka Kiingereza na kurudi kuwa lugha yetu ya Kiswahili. Wizara iangalie hili na kuliwekea mkakati maalum wa kufanya Kiswahili kuwa lugha maalum katika shule zetu nchini; na
- (iv) Mifumo yote ya utoaji taarifa katika Serikali, Bunge na Mahakama haina budi sasa kuwa katika lugha moja tu ya Kiswahili ili lugha ya Kiswahili iendelee kuthaminiwa na kukuzwa. Hii ni sambamba na suala la sheria zetu na uendeshaji wa kesi Mahakamani uwe kwa Kiswahili ili wananchi walio wengi waelewe na

kuzijua sheria husika na mienendo ya kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio hili.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyekuwa Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa George Mkuchika, alitoa agizo kwamba Bodi zote zilizoko nchini zitumie Kiswahili katika vikao vyake vyote. Je, utaratibu huo umefikia wapi au ni maneno tu? Kukienzi Kiswahili, hilo nalo lingezingatiwa.

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa kunijaalia afya, salama na amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya Kiswahili ni muhimu na itifaki hii ni busara sana kuridhiwa, inayo faida nyingi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya kuzingatia ni kuwa hapa ndani Kiswahili bado hakijafanikishwa kwa mfano, lugha ya Kiswahili ni "*phonic*" kwa maana kwamba kinatamkwa kama kinavyoandikwa. Kanuni hii hatujaitilia maanani. Tunaruhusu Taasisi zetu kuchafua lugha yetu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuna bango limeandikwa "Taasisi ya Bahali", bahali sio Kiswahili bali ni bahari ndio neno sahihi. Tunapaswa kuandika kwa usahihi na tuwaache watu ambao wanaathiriwa na lahaja (*vilugha*) vyao waigize kutamka hilo neno, wakishindwa wakitamka bahali

hapana kosa kwa sababu tutafahamiana uandishi hauwi sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata waandishi wa habari wanapotosha Kiswahili, mfano Wanahabari wamevumisha mpaka limetumika neno “kasheshe”, halina asili ya Kiswahili lakini limepigwa debe na Wanahabari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kunaingizwa neon “Lisaa Limoja” hiki sio Kiswahili, Kiswahili ni “Saa Moja”. Hivyo Wizara inayohusika ni muhimu kusimamia ufasaha wa Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanaa zetu katika michezo ya kuigiza na mashindano ya Umisi, zinaharibu lugha na utamaduni kwa kuvaa mavazi yanayoharibu utamaduni wetu. Ni vema Mabaraza husika yatathmini filamu zetu na lugha za michezo hii kabla ya kuruhusu kuoneshwa au kurekodiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi hapa Bungeni wakati tunapitisha bila kujali lugha. Hii itifaki imeanza kwa kusema: “kwa kuwa dhumuni mojawapo...”, neno dhumuni sio Kiswahili bali neno madhumuni ndio Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema moja ya faida nyingi ni ajira. Hizo ajira ni muhimu kuzingatia Muungano wa Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar kwa zile nafasi tutakazopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale BAKITA inapotafuta neno la kutumia katika Kiswahili ni muhimu kushirikiana na BAKIZA. Maneno mengi yanaingizwa katika lugha na kutolewa bila kuzingatia lahaja za Kizanzibari, wakati zipo, mfano “kukarabati” lipo neno “kutengeneza”. Hivyo, kuonekana kama kuna mvutano wa kilugha jambo ambalo halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijitahidi kujisafisha wenyewe humu ndani ya nchi, tutakuwa imara na lugha itaimarika na nchi za wenzetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki wataiga mfano wetu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia kwa maandishi na ninaunga mkono hoja.

**MHE. SULEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana kwa nia njema ya kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili na napendekeza yafuatayo:-

- (i) Kiswahili kizungumzwe rasmi kila mikutano yote ya Kitaifa na Kimataifa inayofanyika hapa nchini; na
- (ii) Bajeti ya uhakika itengwe katika bajeti za kila mwaka ili kueneza lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naandika kuunga mkono hoja ya uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoielezwa na Serikali, ni kweli Tanzania itapata faida kubwa kwa kuanzishwa Kamisheni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili kinatumika nchi nyingi Duniani na hasa katika vyo vikiu lugha ya Kiswahili imekuwa moja ya *electives* katika *universities* za Amerika. Kuenea kwa Kiswahili kutakuwa na faida katika mauzo ya vitabu na majarida, lakini pia kitafanya *communication* kuwa rahisi kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na wafanyabiashara wa nchi nyingine katika Afrika Mashariki na baadaye Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Kamisheni itafanya kazi vizuri, nafasi za ajira zitapatikana hata katika nchi za Afrika Mashariki. Inawezekana kabisa wataalam wa Tanzania wakaajiriwa katika Taasisi za nchi wanachama wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa angalizo kwa Kamisheni, maneno mapya yatakayowekwa katika lugha ya Kiswahili (*vocabulary*) yatafsiriwe na yawekwe wazi kwa wananchi ili wananchi wayafahamu. Sasa hivi kumekuwa na tabia ya kutumia maneno yasiyo rasmi katika lugha ya Kiswahili kwa sababu ya wananchi kutofahamu maneno mapya, wakati mwingine wananchi wanatafsiri maneno ya Kiingereza na kuyaongea Kiingereza – Kiswahili, mfano, akajikomiti ikimaanisha *he/she committed her/himself*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Kamisheni itakayoanzishwa ishauri pia wataalamu wa kutunga *vocabulary* ya Kiswahili watunge maneno marahisi (*should use easy words*) ili iwe rahisi na kueleweka na hatimaye lugha hiyo isambae haraka na kwa ufanisi zaidi.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii muhimu ya kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijua kulaumu lazima ujue na kusifu, nichukue nafasi hii adhimu kuwapongeza Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana sana wanayofanya japo bado kuna changamoto nyingi sana zinazowakabili na kuwafanya viongozi wa Wizara hii kufanya kazi katika wakati huu mgumu kwa kuwapa bajeti ndogo sana ambayo haikidhi mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mtera lina Kata 19 katika Kata zote hakuna hata moja yenye maabara hivyo kuwafanya watoto wote kupata nusu elimu. Ombi kwa Serikali yetu kutujengea mabweni na maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya yetu ya Chamwino yenye Majimbo mawili hakuna Chuo cha ufundi stadi. Naomba Wizara itujengee *VETA* katika Kijiji cha *Mvumi Mission*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.



**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi niungane na Wabunge wenzangu, kuunga mkono hoja. Nimesimama kwa heshima kubwa hapa baada ya kuwezesha na Wananchi wa Jimbo la Mvomero, kwa heshima hiyo kubwa waliyonipa ndiyo maana nimesimama hapa na naendelea kuwashukuru na nawaahidi kwamba, nitaendelea kuwa nao katika kupambana na changamoto mbalimbali katika Jimbo letu la Mvomero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru sana Kamati ya Mheshimiwa Mama Margareth Sitta, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kwa namna ambavyo walitupa ushirikiano wakati wa mchakato wa kufanikisha hoja hii kufika hapa Bungeni. Wametoa michango mingi na zaidi waliwahusisha wadau mbalimbali wa Kiswahili. Nataka niwaahidi kwamba, Wizara kama Serikali, pia haya yote ambayo walishauri sisi tutayafanyia kazi. Pia namshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa michango aliyoitoa. Kwanza, niseme tu kwamba nimefarijika sana kwa hotuba yake ambayo naye ameunga mkono hoja. Ushauri aliutoa tutaazingatia na nitaendelea kuutolea ufafanuzi kadiri nitakavyopata muda hapa wakati ninajumuisha.

Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango mingi sana. Yote hii imeonesha ni namna gani ambavyo tunakithamini Kiswahili na Itifaki hii mmeipokea kwa mshiko mzuri sana. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, michango mliyoitoa tutaifanyia kazi na tutatoa majibu kwa hoja zote ambazo mmezisema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majadiliano hapa tumepata wachangiaji ambao wamezungumza kwa mdogo wako 21 na kwa maandishi wako 21. Naomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii kwa kuzungumza hapa Bungeni ambao ni Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrea Kigwangala, Mbunge wa Nzega, aliongea kwa niaba ya Kamati, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mbunge wa Nyamagana, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, Mheshimiwa Eugen Mwaiposya, Mbunge wa Ukonga, Mheshimiwa Mariam Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John Shibuda Magalle, Mbunge wa Maswa Magharibi, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti

Maalum na Mheshimiwa Janet Mbene, Mbunge wa Kuteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa njia ya Maandishi ni Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mbunge wa Mtoni, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mbunge wa Kilindi, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Pudensiana Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mbunge wa Meatu, Mheshimiwa Salvatory Machelili, Mbunge wa Ukerewe na Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, wote waliozungumza hapa na waliochangia kwa maandishi, wameeleza

umuhimu wa kukuza Lugha ya Kiswahili nchini na kuisitiza umuhimu wa kuridhiwa Itifaki hii. Kwa hiyo, nataka niseme kuwa nashukuru Wabunge wote tulioongea hapa, tumekubali kwamba tumechelewa na tuko tayari kuridhia Itifaki hii. Nawaomba sana turidhie Itifaki hii kutokana na faida ambazo Tanzania itazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii. Hoja zilizotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, zimepokelewa na Wizara itaendelea kuzifanyia kazi kwa umakini mkubwa. Kamati imetoa hoja na maoni kadhaa na ninapenda kuyarejea na kuyatolea ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Moja ni Muundo wa Wajumbe wa Kamisheni kujumuisha makundi yote ya Wadau wa Kiswahili. Nataka kusema kwamba, hoja imepokelewa na Tanzania itawasilisha pendekezo hili pindi fursa ya kuipitia na kuiboresha Itifaki itakapopatikana. *Article 28* inaeleza kwamba, baada ya Itifaki hii kuridhiwa, yale marekebisho nchi mwanachama wanao uwezo wa kuyapeleka na yakapokelewa na yakaboreshwa kama ambavyo mmependekeza.

Pili ni kuwa, Serikali iandae mikakati mahususi ya kuwezesha wananchi kukipenda na kukienzi kwa dhati Kiswahili. Ushauri huu pia tumeupokea na hivi sasa vyombo vyetu vya habari vinafanya kazi hiyo, tukianza na TBC wanafanya kazi hiyo na ninyi mmekuwa mashahidi hapa mmesema wana vipindi, lakini pia niwapongeze sana Radio One, wanafanya kazi nzuri sana ya kukieleza Kiswahili.

Lingine ni umuhimu wa kutangaza ndani na nje ya nchi, fursa zilizopo za kufundisha na kutafsiri Lugha ya Kiswahili. Ushauri huu ni muhimu sana na Wizara yangu itafanya kila linalowezekana, kuwajua Wataalamu na Wadau wa Kiswahili kuhusu upatikanaji wa fursa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kuandaa Sera ya kuendeleza Lugha ya Kiswahili ili kutoa mwongozo wa ustawishaji na uenezaji wa Kiswahili; tayari mwongozo wa ukuzaji na uenezi wa Kiswahili nchini na nje ya nchi, umezingatiwa katika Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997, ambayo imo katika hatua za mwisho za kupitiwa upya. Serikali iziwezeshe kifedha Taasisi za Kiswahili ili zitekeleze kwa ufanisi kazi zake. Serikali inapokea ushauri huu na kwamba ni jambo muhimu sana kuziwezesha Taasisi za BAKIZA na BAKITA ili ziweze kutekeleza majukumu yake vizuri ya kukuza Kiswahili. Hili niwaombe tu mwaka wa fedha unaokuja, basi katika bajeti sisi tutaleta mpitisho bajeti hiyo ili kuziwezesha Taasisi hizi ziweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lugha ya Kiswahili itumike katika makongamano, mikutano, warsha na semina mbalimbali zinazofanyika nchini. Huduma ya ukalimani itolewe kwa wageni wasioweza kufuatilia mijadala kwa Kiswahili. Serikali inakubaliana kabisa na ushauri huo na niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge, nanyi muwe Mabalozi wazuri na mifano mizuri kuona kwamba tunatumia Lugha yetu ya Kiswahili katika mikutano mbalimbali. Imeonekana hata hapa kwamba Kiswahili bado ni kigumu,

kwa sababu hata Mwalimu aliyekuwa anatufundisha hapa, Mheshimiwa Mkuchika, naye alisema kwamba, alipokuwa *News Room* ambacho ni chumba cha habari, alisema kwamba alikuwa *temporary* kwa maana kwa muda; kwa hiyo, kila mmoja anatumia neno la Kiingereza katika kufikisha ujumbe na wote hapa hakuna hata mmoja ambaye amesimama ameongea Kiswahili moja kwa moja labda Mheshimiwa John Shibuda Magalle, lakini wengi nimeona wameongea kwa Kiswahili na Kiingereza. Kwa hiyo, bado ni tatizo na sisi basi tuwe Mabalazi wazuri wa kuweza kuona kwamba tunakitumia Kiswahili ipasavyo, lakini pia Kiswahili ni kigumu.

Yupo mtu amenitumia ujumbe akasema kwamba, hata neno lugha wengine wanasema lugha na wengine wanasema lugha, mwingine anasema kula, kumbe kura. Kwa hiyo ni mambo mengi, Kiswahili kumbe bado ni kigumu lakini msisitizo ni kwamba, tutumie lugha yetu ya Kiswahili katika mikutano yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ielekeze taasisi zote za utoaji wa elimu nchini, pamoja na shule binafsi, zifundishe somo la Lugha ya Kiswahili kama sharti la msingi. Tunaahidi kulifanyia kazi suala hili na tutashirikiana na Wizara ya Elimu na Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Amali kule Zanzibar, kuona suala hili tunalifanyia kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Jamhuri ya Muungano, liwe la mfano kwa kutekeleza shughuli zake zote kwa Lugha ya Kiswahili, ikiwemo kuwasilisha Miswada na Mikataba iliyoandaliwa kwa Lugha ya Kiswahili. Wizara yangu inaunga mkono hoja hii na wito huu wa Kamati ya

Huduma za Jamii na ipo tayari kuratibu upatikanaji wa Wataalamu wa Kiswahili ili kufanikisha azma hii. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa, Wizara tayari imetafsiri kwa Kiswahili, Itifaki hii ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili, tayari Wizara imefanyia kazi kuweza kuitafsiri iwe katika lugha ya Kiswahili, lakini itifaki yenyewe wakati wanasaini ilikuwa imeandikwa kwa Lugha ya Kiingereza na ndiyo maana tumeweza kuiwasilisha hivyo. Kamati iliposhauri, tumeifanyia kazi kwamba Itifaki hii sasa itafsiriwe kwa Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kambi ya Upinzani kama nilivyosema, nashukuru kwa kuunga mkono hoja hii na hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani nazo tumezipokea na tutazifanyia kazi na hizi ni baadhi tu ambazo tunaweza tukazitolea ufafanuzi mbalimbali. Moja, kuhusu Tanzania kushindwa kutumia nafasi yake ya kinara wa Kiswahili Barani Afrika na Duniani katika kusaka fursa mbalimbali katika soko la ajira. Wizara imepokea changamoto hii na tutaendelea kuifanyia kazi. Wizara yangu inawahimiza wataalamu na wadau kuwa na uthubutu wa ushindani katika masoko ya ajira za Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuwepo kwa milioni kumi tu ya kutoa elimu kwa umma kuhusu Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni fedha ndogo sana. Ni kweli bajeti ni ndogo, lakini hii imelenga kutoa elimu kwa umma na pia bajeti itatengwa katika mwaka ujao wa fedha kuona kazi hii inafanyika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mbinu zitakazotumika kutoa elimu kwa umma juu ya Kamisheni na

majukumu ya nchi wanachama katika kutoa elimu hiyo. Serikali itatumia vyombo vyake vya habari kutoa elimu hii na mijadala ya moja kwa moja kwa wananchi. Aidha, kila Nchi Mwanachama wa Jumuiya itatoa elimu hii ya kuitangaza Itifaki ya Kamisheni kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia hoja mbalimbali za Kamati na Kambi ya Upinzani, sasa nitumie fursa hii kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Moja la ujumla ni kwamba, Tanzania tumekuwa nyuma sana katika fursa za ajira, kwa maana ya Walimu na Wataalam wa Kiswahili na wenzetu Wakenya wako mbali sana, ni kama vile wametuzidi na kinachoonekana hapa ni kama vile sisi hatujafanya kitu chochote.

Ninachoweza kusema ni kwamba, katika mjadala wa Kamati na Wadau, mimi mwenyewe nimefaidika kwa kumsikia Dkt. Mtembei, ambaye ni Mwalimu Chuo Kikuu; ametueleza na hili nafikiri Mheshimiwa Profesa Kahigi atakuwa anaelewa kwamba, sisi walimu wengi wa Kiswahili wanakuwa ni wale ambao wanasoma na masomo mengine. Kwa mfano, *History, Geography*, labda na Kiswahili, unaenda kufundisha. Hatukuwa na digrii ya moja kwa moja kwamba unapata Shahada hii ya Kiswahili, haikuwepo. Kwa hiyo ni kwamba, mtu anasoma masomo labda matatu na Kiswahili likiwa ni somo anakwenda kufundisha, lakini wenzetu Wakenya wao walianza kutoa hizi shahada za Kiswahili moja kwa moja na unapotaka kwenda kufundisha nje ya nchi hutakwenda kuonesha kwamba mimi ni mwalimu na nimesoma masomo matatu na Kiswahili kikiwa kinatajwa, bali watakuona kama



mwalimu mwenye kuelewa Kiswahili fasaha na kufundisha pale ambapo una shahada yako ya Kiswahili.

Kwa hiyo, wenzetu Wakenya walifanya mapema sana na akatuambia kwamba Shahada ya Kiswahili rasmi ilianza kutolewa mwaka 2009 na *Masters* imeanza kutolewa kwa mara ya kwanza 2010.

**MWENYEKITI:** Ni Shahada ya Uzamili.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Shahada ya Uzamili. Kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo kwa nini tumefika hapa, Wakenya wametuzidi. Tuelewe tu kwamba sisi tumechelewa kutoa Shahada za Kiswahili, wenzetu walikuwa wajanja waliweza kutoa na ndiyo maana wanapata nafasi kufundisha Kiswahili nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niliweke sawa hilo.

Lingine ni kwamba, Itifaki hii ilisainiwa 2008 na nchi tatu na nimeulizwa kwamba je, ni nchi ngapi mpaka sasa zimeridhia Itifaki hii? Ni kwamba, katika nchi tatu, Kenya ndiyo wa kwanza kuridhia, wameridhia mwaka 2010 na Tanzania na Uganda ndiyo sasa tupo kwenye mchakato na ninyi mkishapitisha hii mkiridhia na Uganda kule wakiridhia, basi tutakuwa nchi tatu wanachama tumeweza kuridhia. Kwa hiyo, Kenya wametutangulia kuridhia wameridhia mwaka 2010 na Uganda na Tanzania ndiyo tupo katika mchakato huu wa kuweza kuridhia.

Hoja nyingine ilitolewa hapa kwamba kwa nini *Article* Namba 14 ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri umeulizwa hapa Rwanda na Burundi vipi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Rwanda na Burundi, baada ya sasa kuridhia nchi tatu na wao wataomba katika kukaribishwa na wachama waanzilishi watatu kuingia katika hiyo Itifaki. Kwa hiyo, kwanza ni nchi hizi tatu wanachama wataridhia na maombi yote yataendelea kupokelewa kwa nchi yoyote itakayotaka kuingizwa katika Kamisheni hii ya Kiswahili.

Lingine, nilieleza kwa nini *Article 14* inaeleza kwamba, Makao Makuu ya Kamisheni yataamuliwa na *Council*. Matokeo yake ni kama vile imekiukwa na mimi nimkumbushe rafiki yangu Mheshimiwa Wenje kwamba, aliposoma *Article 14* angesoma pia *Article* Namba Moja; kwamba, *definition* ya *Council* means the *Council of Ministers of Community established by Article Nine of the Treaty*. Kwamba, ni hilo hilo Baraza la Mawaziri ndilo lililoridhia Makao Makuu ya Kamisheni yawe Zanzibar. Kwa hiyo, hakuna mahali ambapo kama Tanzania tuliweza kupotoka. Angesoma *Article 14* na *Article* Namba Moja ile iliyokuwa inaeleza maana hasa ya *Council* ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ya jumla, sasa nipitie hoja mbalimbali ambazo zimetolewa

hapa na Mheshimiwa Profesa Kalikoyela Kahigi na Mheshimiwa John Mnyika; wametoa ushauri mzuri sana kuhusiana na Itifaki kuendelea kuridhiwa, walikuwa wana wasiwasi kwa nini Zanzibar inatajwa.

Nasema inatajwa kwa sababu mwaka 1960 ilikuwa bado hakujawa na Muungano, kwa hiyo, lazima Zanzibar ilikuwa itajwe kwa maana ya Tanganyika, Uganda, Kenya na Zanzibar. Pia Mheshimiwa John Mnyika amesema kwamba, Kiswahili kitumike katika Bunge la Afrika Mashariki, Umoja wa Afrika na hata Umoja wa Mataifa. Hilo pia ni wazo zuri tumelipokea katika kulipigania hilo.

Mheshimiwa John Mnyika anasema kiridhiwa iwe ni fursa ya kufanya marekebisho ya kisera, kitaasisi, kuhusu utunzaji wa Lugha ya Kiswahili. Serikali itafanya hivyo kwa kushirikiana na Wataalam wengine wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Betty Machangu anashauri Kamisheni iombe Wataalam wa kutunga misamiati ya Kiswahili watunge maneno rahisi ambayo ni rahisi kueleweka. Tunakubaliana na pendekezo hili hasa la kutumia Kiswahili chenyewe na hoja zake kubuni misamiati mipya badala ya kutumia maneno ya kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna michango ambayo imetolewa kama nilvyosema, Wabunge wengi

wamechangia, lakini sasa nitapitia mmoja baada ya mwingine na kama muda utaruhusu basi nitakuwa najibu. Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba aliuliza ni watu wangapi ambao wana vyeti vya kufundishia Kiswahili. Kama nilivyosema kwamba, bado Watanzania ni wachache sana na kama Mwenyekiti wa Kamati alivyosema, pana upungufu mkubwa wa Walimu wa Kiswahili na kwamba ni majuzi tu ndiyo tumeanza kutoa Shahada ya Kiswahili na Shahada ya Uzamivu ya Kiswahili.

Pia Mwenyekiti wa Kamati amesema kwamba, fursa zitakazopatikana kuwe na uwazi kwa maana ya wataalam na kazi zitakazokuwa zinatangazwa kuwe na uwazi.

Mimi nataka niahidi tu kwamba, baada ya kuridhiwa kwa Itifaki hii basi fursa zitakapokuwa zinapatikana, kwanza, Tanzania ndiyo Makao Makuu ambapo Kamisheni hii itafanya kazi. Mimi naamini kabisa kwamba kutakuwa na uwazi katika kupata wataalam hawa na Watanzania watafaidika na fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, amesema kwamba, sisi kwa miaka mitano tulikuwa wapi? Ni kwamba, tumechelewa kwa sababu katikati hapa palipatikana maombi ya Burundi na Rwanda, kwa hiyo, hayo kidogo wenzetu wanajadili yaliweza kutuchelewesha. Kama ilivyo kawaida, Serikali ilikaa kulitafakari na kuangalia Itifaki hii na hatimaye baada ya kujiridhisha ndiyo maana tumeweza kuileta hapa. Mimi nawaomba turidhie ili Kamisheni hii ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Kombo, kwanza, nakushukuru sana kwa somo lako hapa ndani, umetueleza mambo mengi na

tumejifunza mambo mengi na umetupa misamiati mingi na kwamba tukienzi Kiswahili na tuweze kutumia Kiswahili fasaha. Ushauri huo sisi tutaufanyia kazi, tushirikiane katika kufanikisha jambo hili.

Mheshimiwa James Mbatia ameeleza namna ambavyo changamoto zipo na upungufu mbalimbali katika kukiendeleza Kiswahili. Nataka niseme tu kwamba, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, tumepokea changamoto hizo na upungufu huo tutaufanyia kazi. Mwisho wa yote ametuasa Watanzania kukiendeleza Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Luckson Mwanjale amesema tufungue Vituo vya Kiswahili nje ya nchi. Mimi nataka niseme tu kwamba, Vituo vya Kiswahili ni muhimu vifunguliwe nje ya nchi kwenye Ofisi zetu za Ubalazi na kituo cha kwanza kimeshafunguliwa tayari Addis Ababa, Ethiopia. Hicho ndiyo kituo cha kwanza kipo kule, Watanzania wanasaidia kufundisha Kiswahili.

Mheshimiwa Leticia Nyerere anasema Tanzania imejiandaa vipi kutumia fursa za uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili? Serikali imeshawahimiza Wataalam wake wa Kiswahili kujiandaa kugombea nafasi za juu za Uongozi katika Kamisheni hii.

Umuhimu wa Kiswahili kutumika kufundisha elimu badala ya kuendelea kushabikia Shule za *English Medium*. Wizara ingependa Kiswahili kipewe fursa pana zaidi katika utoaji wa elimu nchini. Hivyo, itashirikiana na Wizara ya Elimu kwa Tanzania Bara na Zanzibar kuona Kiswahili kinapatiwa

hadhi sahihi katika eimu, lakini pia hata Kamati ilishauri kwamba, hata shule binafsi kuwepo na ulazima wa kufundisha somo la Kiswahili maana zipo shule binafsi zingine hawafundish. Kwa hiyo, kuwepo na ulazima wa kufundisha somo la Kiswahili.

Lingine ni kuunga mkono hoja Serikali ya Awamu ya Nne kupata Makao Makuu, ilikuwa ni pongezi kwa Wizara. Wizara inapokea pongezi hizi za kufikisha Itifaki katika hatua hii ya leo ya kuridhia.

Tuwe makini katika kujifunza Kiswahili sanifu kama ilivyo Kenya. Rai hii ilitolewa na Mheshimiwa George Mkuchika. Nataka niseme tu kwamba, suala hili litazingatiwa kwa dhati kabisa mara baada ya kuridhiwa kwa Itifaki hii.

Mheshimiwa Felix Mkosamali alizungumzia juu ya umuhimu wa Sera ya Lugha kueleweka vizuri zaidi kwa wananchi na nafasi yake kielemi. Ni kwamba, jitihada kubwa zinafanyika kuitangaza Sera ya Utamaduni iliyopo na baada ya kukamilisha mapitio yake, kipengele chake kinachohusu lugha kieleweke zaidi.

Lugha ya Kiswahili itumike kama kitega uchumi cha Taifa. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Mendrad Kigola. Wizara inakubaliana na hoja hii kwamba, Kiswahili ilikuwa ni lugha ambayo ilitusaidia katika ukombozi, ni Lugha yetu ya Taifa, tunaitumia lakini sasa Kiswahili kitumike kwenye kuliingizia Taifa pato, kiuchimi zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, pia waliuliza kuhusu usaili kuendeshwa kwa Kiingereza. Unatoa kauli gani kuhusu eneo hilo? Kama Waswahili tunahitaji kufanyiwa usaili kwa Lugha ya Kiingereza au Kiswahili? Serikali inasemaje?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachoweza kusema ni kwamba, hayo yote ni matumizi ambayo hata leo watu wameongelea pia kwamba hukumu zitolewe kwa Kiswahili. Mimi nataka niseme tu kwamba, kwa wale wa Mahakamani wanaelewa kwamba, Sheria inasema unaweza ukaendesha kesi kwa Kiswahili au kwa Kiingereza. Ninachokiomba ni kuridhia Itifaki hii na suala la matumizi ya Kiswahili tuliyopokea katika mijadala hii yatatusaidia sisi katika kuyafanyia kazi mara baada ya Itidaki hii kupitishwa. Kwa hiyo, hapa tunachoomba kwenu ni kuridhia kwa Itifaki hii. Michango tuliyopokea tumefaidika zaidi kama Wizara, lakini ni mambo ambayo ni angalizo kwa maana ya matumizi ya Kiswahili.

Hayo yote sisi tumeyazingatia, kwa hiyo, kuja kwa maana ya tafsiri kwamba usaili au *interview*, mimi nasema ni matumizi ya lugha. Kwa hiyo, hayo ni mambo mengine kabisa, lakini niseme tu kwamba, mengine yatatajwa katika Katiba, mmesema mchakato unaokuja itamkwe kwenye Katiba kwamba Kiswahili kiwe Lugha ya Taifa na Sheria zote ziandikwe kwa Lugha ya Kiswahili. Yote hayo ni matokeo ya matumizi ya lugha tunayotaka kuikusudia hapa na hasa baada ya Kamisheni kuanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema hapa ni msisitizo tu kwamba sisi tunachokiomba kwenu mridhie kupitishwa kwa Itifaki hii lakini mambo mengine haya ya matumizi yatakuja wakati wa kutaka kwamba wote tumekusudia kukiendeleza Kiswahili chetu.

Lingine ndiyo hilo ambalo nilikuwa naligusia, umuhimu wa Lugha ya Kiswahili kutumiwa rasmi katika Katiba ya Nchi kuwa ni Lugha ya Taifa la Tanzania na kuitumia kwa dhati katika shughuli rasmi za Kiserikali. Hili lilisemwa na Mheshimiwa Tundu Lissu. Niseme tu kwamba, Wizara yangu inakubaliana na hoja hii, tushirikiane kupata Katiba mpya. Suala hili litajwe kwamba Kiswahili kitatumika katika kuandika Sheria za nchi na itajwe katika Katiba kwamba Kiswahili ni Lugha ya Taifa.

Lingine Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoa nafasi finyu kwa Kiswahili, yaani *lingua franca* tu, yaani lugha ya mawasiliano. Hili lilitolewa na Mheshimiwa Profesa Kahigi. Anasema hatua ya kukitambua Kiswahili kuwa ni *lingua franca* ni hatua ya mwanzo kukipatia hadhi kubwa Kiswahili. Kwa kawaida lugha zenye hadhi hii ndizo hatimaye huwa lugha rasmi. Hivyo, Serikali yetu itaendelea kukipigania Kiswahili kuwa lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Lingine ni kwamba, kuridhia iwe ni fursa ya kufanya maboresho ya kisera, kisheria na kitaasisi kuhusu utunzaji wa Lugha ya Kiswahili. Serikali itafanya hivyo kwa kushirikiana na Wataalam wengine wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.



Kuhusu suala la ukuzwaji wa Kiswahili iwe moja ya kipaumbele katika Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano. Majibu ni kwamba, hili litazingatiwa katika mipango yetu ya maendeleo ya miaka mitano. Kiswahili pia kisaidie kukuza Pato la Taifa kwa kukiiza nje. Ni kweli watakoajiriwa katika Sekta ya Kiswahili Kimataifa watafanyiwa mpango wa kuchangia Pato la Taifa kwa kukatwa kodi.

Mheshimiwa Faki alisema uandishi wa Lugha ya Kiswahili uwe sahihi. Wizara inakubali hoja hii. Ni muhimu Kiswahili kiandikwe kwa usahihi wake na wote waliosema maneno hapa namna ya Kiswahili kinavyokosewa, ushauri wote tutauzingatia kwamba, tuandike na kuongea Kiswahili fasaha. Taasisi nchini ziongeze jitihada za kukukuza Kiswahili.

Wizara itaendelea kuongeza bajeti ya BAKIZA na BAKITA kadiri uwezo wa kifedha utakavyopatikana ili kuziwezesha Taasisi hizi kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, Wabunge wote wameongea; la kwanza, wanakubali kwamba Itifaki hii iridhiwe. La pili, Wabunge wote kwa pamoja wameonesha namna ambavyo wanakipenda Kiswahili, wanapenda lugha yao na wanataka lugha hii idumishwe na kuenziwa.

Kwa hiyo, michango ipo mingi na kama kawaida, Wizara itaandaa kabrasha zuri ambalo litatoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, walizotoa kuhusiana na Itifaki hii. Nami nawashukuru sana na niwaombe tu, kama ambavyo mmeonesha kuridhia kwa maneno na kwa maandishi, niwaombe sasa kwa kauli moja mnisaidie kuridhia Itifaki hii na wenzetu wa Uganda waridhie

ili Kamisheni hii ianzishwe na iweze kufanya kazi. Tanzania tumepewa kipaumbele cha kuwa Makao Makuu, Watanzania watapata fursa mbalimbali za ajira. Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kuwaomba sana kwamba mridhie Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika  
Mashariki liliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawapongeza kwa kuridhia Azimio hili kwa pande zote mbili, kwa kuona umuhimu wa kuridhia Azimio hili kwa manufaa ya nchi yetu. Kabla ya kuahirisha shughuli hizi, napenda kuwakumbusha Wabunge wa CCM, tangazo la Mheshimiwa Jenista Mhagama mlizingatie.

Baada ya hapo, naomba kuahirisha shughuli hizi hadi kesho saa tatu asabuhi. Jioni njema.

*(Saa 1.26 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 2 Novemba, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*

